

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Pili – Tarehe 28 Januari, 2009

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 16

Fedha za Maendeleo ya Mkoa

MHE. MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH aliuliza:-

Kwa kuwa, Ofisi za Wakuu wa Mkoa nchini zimekuwa zikitengewa fedha kila mwaka kwa ajili ya kuchangia shughuli za maendeleo ya Mkoa:-

- (a) Je, katika kipindi cha mwaka 2001 hadi Juni, 2008 Mkoa wa Pwani ulitengewa kiasi gani?
- (b) Je, katika kipindi hicho Wilaya ya Mafia imechangiwa kiasi gani na Mkoa husika kwa ajili ya Maendeleo ya Wilaya?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdulkarimu Esmail Shah, Mbunge wa Mafia, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Fedha za Mfuko wa Maendeleo wa Mkuu wa Mkoa hutolewa na Mkuu wa Mkoa kuchangia, kuhamasisha na kuunga mkono juhudi za wananchi katika kujiletea maendeleo yao. Kila mwaka fungu hili hupatiwa shilingi milioni 10. Mchango huu mara nyingi hutolewa wakati wa ziara za Mkuu wa Mkoa

Wilayani pale alipotembelea walengwa na kuridhika na juhudi zao na hivyo kuwaunga mkono kwa msaada wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2001 hadi Juni, 2008 ili kuhamasisha juhudi za wananchi Mkoa wa Pwani ulipata kiasi cha shilingi milioni 70 kama fedha za Maendeleo kutoka katika Mfuko wa Mkuu wa Mkoa.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho Wilaya ya Mafia ilichangiwa kiasi cha shilingi milioni 4,810,000/= katika maeneo mbalimbali na miradi mbalimbali ya maendeleo.

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Nilikuwa naomba nifahamu kwamba ni vigezo gani, na kama kigezo ni maendeleo je, sisi wananchi wa Mafia kwa kipindi cha miaka hiyo aliyoitaja ya kupata shilingi milioni 4,810,000 anaweza akatupatia mchanganuo toka kipindi hicho hadi leo kila mwaka tulipata kiasi gani?

(b) Nilikuwa naomba kuuliza kwamba kwa nini fedha kama hizo zisiongezwe na kuwapa Wakuu wa Wilaya na wao wakati wanapotembelea katika vijiji, kata na sehemu zingine Wilayani wakapata na wao kuchangia ili waonekane na wao kwamba wanachangia badala ya kwenda kuhimiza na kuondoka na kutokuwa na mchango wa aina yoyote zaidi ya kutoa fedha zao mfukoni? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu sijui la sehemu (a) linahitaji takwimu basi endelea.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, mwaka wa 2001 kiasi cha shilingi 250,000/= zilitolewa kwa *DED* kwa ajili ya ujenzi wa shule ya msingi Msimbani. Mwaka huo huo 300,000/= zilitolewa tena kwa *DED* kuchangia ununuzi wa kompyuta na uchimbaji visima. Mwaka 2002 zilitolewa shilingi milioni moja kwa *DED* kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa shule ya sekondari ya Tarafa ya Kaskazini. Mwaka 2003 zilitolewa shilingi 500,000/= kwa Baraza la Vijana kwa ajili ya kuchangia shule na shughuli za maendeleo ya vijana. Mwaka 2003 shilingi 500,000 zilitolewa kwa kikundi cha akinamama Juhudi kuimarisha Mfuko wa kikundi. Mwaka 2003 huo huo shilingi 200,000 zilitolewa kwa ndugu Mohamed Salim Kariro kuchangia gharama za matibabu Mafia. Mwaka 2004 shilingi 300,000 zilitolewa kwa Umoja wa Wazee wa Mafia kuchangia Mfuko wa Wazee.

Mwaka 2004 shilingi 500,000 zilitolewa kwa ajili ya Msikiti kuchangia maendeleo ya Msikiti. Mwaka 2005 shilingi 100,000/= zilitolewa Bi. Mwanaida Simba kuchangia gharama za matibabu na mwananchi anayetoka Mafia. Mwaka 2006 shilingi 200,000 zilitolewa kwa Mshikamano Vikoba kuchangia maendeleo ya vikundi. Mwaka

2008 shilingi 500,000 zilitolewa kwa DED Mafia kuchangia Mfuko wa Elimu wa Wilaya ya Mafia. Mwaka 2008 shilingi 240,000 zilitolewa kwa kikundi.

Mheshimiwa Spika, kama unavyoona ninazo takwimu zote hapa kama atahitaji mimi naweza nikampatia nakala hii ili aweze kujiridhisha, lakini kwa maana ya swali hilo la (a) hayo ndiyo majibu yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la (b) anazungumzia suala la kwamba kwa nini tunaziacha hizi fedha zinaishia kwa Mkuu wa Mkoa tu, kwa nini zisiongezwe sasa zikaenda mpaka kwa Wakuu wa Wilaya nadhani hata kwa Wabunge na watu wengine. Sasa hili ni jambo ambalo linatakiwa lifanyike humu ni maamuzi sasa hapa yatakayofanywa na Bunge hili na kwa kupitia sera za Serikali na kama itaamuliwa kwa sababu itakuwa na *budget implications* zake. Mimi sidhani kama mimi hapa mwenyewe hivi ninaweza kujibu kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini nafikiri ni jambo ambalo tunaweza tukalitafakari sisi sote kwa pamoja, halafu tukaliingiza katika bajeti kama itakuwa imekubalika hivyo. (*Makofi*)

Na. 17

**Uhitaji wa Waganga na Wauguzi
Kwenye Zahanati – Songwe**

MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA aliuliza:-

Kwa kuwa ni Sera ya Serikali kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 ya kupeleka huduma za Afya kwa kujenga Zahanati na Vituo vya Afya Vijijini; na kwa kuwa Kata zote kumi katika Jimbo la Songwe zina Zahanati, lakini katika Zahanati za Udinde. Kapalala, Sanza, Galula na Ngwala hakuna Waganga na baadhi yake hakuna Wauguzi wa kuwahudumia wagonjwa kwenye maeneo hayo:-

(a)Je, ni lini Serikali itatekeleza Ilani ya Uchaguzi kwenye Zahanati hizo?

(b)Kwa kuwa tatizo hilo ni la muda mrefu na Serikali bado halijapatia ufumbuzi. Je, kutopeleka Waganga na Wauguzi kwenye Zahanati hizo sio ukweli kwamba Serikali imeshindwa kutekeleza matakwa ya Ilani ya Uchaguzi 2005 kwenye Sekta hiyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, Mbunge wa Songwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imedhamiria kuboresha huduma za Afya kwa kupeleka huduma za Afya karibu na wananchi kwa kujenga Zahanati na Vituo vya Afya. Sambamba na kuongeza Zahanati na Vituo vya Afya Serikali pia imekuwa ikiongeza watumishi wa Kada ya Afya kwa awamu katika Zahanati na Vituo vya Afya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watumishi wa Kada ya Afya kwenye Zahanati za Udinde, Kapalala, Saza, Galula na Ngwala, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna upungufu kulingana na Ikama halisi inayotakiwa. Hali hii imekuwa ikitokana na baadhi ya watumishi wanaopangiwa kufanya kazi katika Wilaya ya Chunya kutokuripoti. Katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2007/2008, jumla ya watumishi 92 wa Kada mbalimbali za afya walipangiwa kwenda kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya. Kati ya hao ni watumishi 25 tu walioripoti ambapo watumishi 5 waliondoka baadaye bila maelezo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2008/2009 Halmashauri ya Wilaya ya Chunya imeidhinishwa jumla ya nafasi 48 kwa Kada mbalimbali zilizo chini ya Idara ya Afya. Tayari Halmashauri ya Wilaya ya Chunya imeomba kibali kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili nafasi zilizoachwa wazi ziweze kujazwa.

Natoa rai kwa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kuzipa kipaumbele Zahanati zisizo na watumishi wa kutosha ikiwa ni pamoja na Zahanati za Udinde, Kapalala, Saza, Galula, na Ngwala pindi watakapojiri watumishi wapya.

MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, pamoja na majibu mazuri yenye kuleta matumaini ya Naibu Waziri kuna vituo ambavyo kwa kweli kama tutafuata huo utaratibu ambao sasa hivi Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza, kuna hatari kwamba mwaka unaweza ukaisha bila kupata watumishi, na vituo hivyo ni vile ambavyo haviko karibu ya hospitali, navyo ni Ngwala, Namfukwe, Dinde. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, hauwezi wakati huu akatoa kipaumbele kwa hivyo vituo angalau kupeleka wale ambao mnafikiri wanaweza wakawa kule kwa muda?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, mimi nataka kwanza niridhike kwamba kuna tatizo hapa na jambo linalozungumzwa na Mheshimiwa Mbunge hapa linahusu maisha ya watu. Kwa hiyo, siwezi kutoa majibu hapa kwa niaba ya Serikali ya kubabaisha hapa. Kwa hiyo, kwa sababu haya ni maisha ya watu kama tunazungumza habari za maisha ya watu lazima tuwe na seriousness kubwa na niseme kwamba ni kweli kwamba kuna hilo tatizo na ndiyo maana nimetoa hizi takwimu hapa kuonyesha jitihada ambazo zinafanyika. Mimi ninamuomba Mheshimiwa Mbunge aje kwa sababu hapa kuna wadau watatu, kuna sisi TAMISEMI, kuna Wizara ya Afya na kuna Utumishi. Wote kwa pamoja tunaweza tukaangalia kwa pamoja kwamba ni kwa namna gani kwa sababu tatizo hili liko nchi nzima hivi tunavyozungumza. Sasa ni suala la kuangalia ni wapi ambapo tunasema kwa sababu unaweza ukaondoa hapa ukakuta umesababisha tena tatizo lingine kubwa. Siwezi kulitolewa maelezo hapa wala majibu hapa lakini namuomba Mheshimiwa Mbunge, tukae wote kwa pamoja tuone jinsi ambavyo tunaweza tukasaidia kwa dharuru wakati tukisubiri hii idadi kubwa ambayo imepangiwa kwenda kule. *(Makofi)*

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo hili la watumishi limekuwa sugu kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba ni karibu ni tatizo la nchi nzima. Je, isingekuwa vema kwa Serikali sasa kuangalia uwezekano wa kuwachukua vijana wanaotoka kwenye maeneo yale wakapewa mafunzo ili warudi kuhudumia pale kuliko hawa watumishi ambao wanagoma kwenda? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri unaonaje ukichangia hapo?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, utaratibu uliopo ni kwamba Tanzania ni moja na tungependa vijana waweze kufanya mahali popote pale Tanzania vinginevyo tutakuwa tunaweka tabaka la watu ambao wanao wengi wakafanya kazi mahali pale. Nikizidi kuongeza jibu zuri alilotoa Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba utaratibu uliopo ni kwamba Halmashauri zinaainisha mahitaji yao. Baada ya kuainisha wanatenga fedha. Nimesema hilo kwa sababu kuna maeneo tumepeleka watumishi lakini wakienda huko wanakuta fedha hazikutengwa. Vile vile kuiomba Serikali kuu ipeleke wafanyakazi wa dharuru maeneo fulani itakuwa vigumu kwa sababu tunapeleka wafanyakazi Halmashauri wao ndiyo wanajua mahali gani pana matatizo na wao ndiyo wanawapangia maeneo yale. Kinachotokea ni kwamba wanahitaji vivutio. Maeneo aliyoyasema Mheshimiwa Sigonda mengine mimi nimefika na ni lazima kuwa vivutio kama nyumba na vitu kama hivyo ambavyo vinaweza vikawafanya wakae mahali pale.

Vile vile sisi kama Serikali tunaangalia incentive package kwa mtu ambaye anakaa mahali pagumu basi aweze kupewa cha ziada ili avutiwe kwenda kule na kukaa kule.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi sasa kuna upungufu mkubwa wa mahitaji ya watumishi katika vituo vya afya au zahanati na kwa kuwa malengo ya Serikali hivi sasa ni kwamba kila kijiji na kila kata kuwe na vituo vya afya na zahanati. Je, Serikali kwa upungufu huu haioni umefika wakati sasa isitopishe malengo hayo ili vituo vilivyopo viwezi kupata huduma ya madaktari na waganga kama ilivyokuwa inatakiwa? (*Makofi*)

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, jana tulipitisha Muswada na hata asubuhi kulikuwa na swali ambalo tulilijibu lote lilikuwa linahusu upungufu wa wafanyakazi. Masuala yote ya MAM wote tumeyapitisha na wote wameyakumbatia kwamba ni mazuri. Nadhani tutakuwa tunarudi nyuma kama tunasema kwamba tuache hii shughuli ya kujenga hivi vituo. Tumeleza jitihada za Serikali na hadi sasa kuanzia awamu hii ilipoingia madarakani tumeajiri vijana zaidi ya 11,000 matatizo ni kwamba wengi hawataki huko mahali, tulilenga zaidi maeneo ambayo kulikuwa na upungufu wakati tunaanza hii awamu tulikuwa na *dispensary 652* ambazo zilikuwa zimejengwa na wananchi lakini zilikuwa hazijafunguliwa.

Mpaka mwisho wa mwaka jana ni karibu dispensary ni karibu 450 ambazo tulikuwa tumezifungua baada ya kupeleka wafanyakazi. Tumeleza kwamba tumebadilisha mitaala ili kada ya wasaidizi kama *Clinical Assistants, Health Assistants*

na Laboratory Assistants pia tuendeleo kuwafundisha ni kada ambazo zilikuwa zimefutwa hawa tuna imani watakwenda vijijini. Tungeomba kupewa muda na tupewe *support* ya mama Mchemba na Wabunge wenzangu wengine. (*Makofi*)

SPIKA: Nashindwa kujizuia hapa kuelezea furaha yangu kwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo na Madiwani wenzetu huko ambao wameamua katika suala hili kutembelea vyuo vyote vinavyofundisha watumishi wa afya na kuwaeleza hivi kwamba ukienda Urambo utapewa samani bure na utapewa chakula cha miezi sita ya kwanza ili uweze kukaa vizuri natumaini hatua hii itazaa matunda. (*Makofi/Kicheko*)

Na. 18

**Ahadi ya Kukamilisha Bwawa la Manchira na Kuwapatia
Wananchi Maji Safi na Salama**

MHE. JUMA H. KILIMBAH (K.n.y. MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI)
aliuliza:-

Kwa kuwa, wakati wa kampeni za uchaguzi wa mwaka 2005 wananchi wa Serengeti waliahidiwa na Mheshimiwa Rais kwamba ifikapo mwaka 2007 wangepatiwa ufumbuzi wa tatizo la maji kwa kupatiwa maji safi na salama kupitia bwawa la Manchira; na kwa kuwa, mwaka huu 2008 bwawa hilo limekamilika kwa asilimia 90 (90%):-

(a)Je, Serikali inasemaje kuhusu kutokamilika kwa ahadi hiyo kwa wakati?

(b)Je, ni lini kazi ya utandazaji wa mabomba na uchimbaji wa mitaro ya kutolea maji toka bwawani kwenda vijiji husika itaanza?

(c)Je, ni lini wananchi waliokuwa wanaishi maeneo lilipochimbwa bwawa hili watalipwa fidia kwani mpaka leo hawajalipwa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, ahadi ya Serikali ya kuwapatia maji safi na salama wananchi wa Serengeti kupitia bwawa la Manchira bado ipo palepale. Kutokamilika kwa ujenzi wa bwawa katika mwaka 2007 kulisababishwa na uhaba wa fedha. Hata hivyo, hadi mwezi Juni 2008, ujenzi wa tuta la bwawa ulikuwa umekamilika kwa asilimia 100. Kazi zinazoendelea kwa sasa ni ukamilishaji wa ulipuaji wa mawe kwenye utoro wa maji na uimarishaji wa Utoro kwa kuweka nondo na kumwaga zege katika sehemu mbalimbali za Utoro. Kazi hizo zinatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2009. Utoro ni *spillway*.

(b)Mheshimiwa Spika, kazi ya kuchimba mitaro na kufunga bomba za kutoa maji bwawani na kusambazwa katika Vijiji vya Rwamchanga, Morotonga, Kebosongo, Kisangura, Rung'abure na Nyamoko pamoja na mji wa Mugumu zitatekelezwa chini ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Maji (*WSDP*) inayofadhiliwa na Serikali na Washirika wake wa Maendeleo. Mchakato wa kumpata Mhandisi mwelekezi wa kufanya usanifu unaendelea. Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Musoma tayari imewasilisha katika Wizara yangu hadidu za rejea kwa mapitio na tayari zimewasilishwa Benki ya Dunia kuomba ridhaa ili kazi ya usanifu ianze. Ni matarajio yangu kwamba kazi ya usambazaji wa bomba itanza katika mwaka wa 2009/2010.

(c)Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia ujenzi wa bwala la Manchira, tarehe 12 Julai, 2008 Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, alikagua ujenzi wa bwawa na kuzungumza na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, Viongozi wengine wa Serikali, Mkandarasi wa ujenzi wa bwawa na Wananchi. Aidha, tarehe 17 Januari, 2009 Waziri wa Maji na Umwagiliaji naye alitembelea bwawa la Manchira na kutoa maelekezo ya hatua za utekelezaji zinazofuata kwa Watendaji.

MHE. JUMA H. KILIMBAH: Mheshimiwa Spika, nashukuru majibu mazuri ya Serikali yaliyotolewa na Naibu Waziri. Lakini kazi hii ya ukamilishaji wa utengenezaji wa hili bwawa itakuwa ni moja tu ya kazi ambayo bado wananchi kupata maji itakuwa bado hawajafikia.

Je, baada ya hiyo kazi kukamilika na ahadi ya Serikali ni kupeleka maji vijijini kwa asilimia 65 itakapokamilika 2010 ni asilimia ngapi zitakuwa tayari zimeshafikia kwa Wilaya ya Serengeti?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kazi za ujenzi wa bwawa na Manchira na usambazaji kama nilivyosema kweli bado ni kubwa zilizoko mbele yetu. Hata hivyo pamoja na kwamba hatutakuwa tumemaliza kusambaza maji ifikapo mwaka 2009/2010 Serikali imechukua tahadhari na hatua zingine za dharura kwamba wakati huo tutakuwa tunatafuta njia zingine mbadala zitakazoweza wananchi wa Mji wa Mgumu na vijiji hivi kupata maji angalau katika hatua za muda mfupi. Kule Mgumu visima si *solution* kwa sababu mimi mwenyewe nimetembelea nimeona visima vingi havitoa maji. Lakini wanayo bahati ya kuwa chemichemi ambazo zinaweza zikatoa maji kwa hiyo Serikali itaendelea kutumia utaratibu wetu huu hasa ule wa *quick win* kuhakikisha kwamba katika kipindi hiki basi asilimia angalau hata 70 tuwe tumefikia katika ule Mji wa Manchira wakati mradi huu mkubwa wa *World Bank* nao utakuwa unakamilishwa kwa ajili ya kukamilisha miradi au sehemu zilizobaki.

Na. 19

Serikali kutoa Fedha za Kutatulia Kero ya Maji Mhunze

MHE. FRED M. TUNGU aliuliza:-

Kwa kuwa Rais wetu wa Tanzania alipotembelea Wilaya ya Kishapu mwezi Agosti, 2007 aliwaahidi wananchi wa Mji wa Mhunze kwamba Serikali itatoa shilingi milioni 156 kwa ajili ya kutatua kero ya maji kwenye mji huo:-

Je, mpaka sasa Serikali imekwishatoa kiasi gani cha fedha na utekelezaji wa utatuzi wa kero ya maji Mhunze umefikia hatua gani?

NAIBUWAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fred Mpendazoe, Mbunge wa Kishapu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mji wa Mhunze ulikadiriwa kuwa na jumla ya wakazi 5,990 na mahitaji ya maji ni mita za ujazo 300, lakini kwa sasa uzalishaji ni mita za ujazo 120 tu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Rais alipotembelea Kishapu mwezi Agosti, 2007 aliahidi kusaidia mradi wa maji katika Mji Mhunze kwa ajili ya kutatua kero ya maji katika mji huo. Hivyo, katika kutatua kero ya maji katika mji wa Mhunze mpango ulikuwa ni:-

- Ununuzi wa mitambo miwili ya kusukuma maji;
- Ununuzi wa dira za maji 200;
- Ujenzi wa chanzo cha maji kipya;
- Ukarabati wa Bomba Kuu na mabomba ya kusambaza maji; na
- Ujenzi wa vioski 15.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais, Serikali kwa mwaka wa fedha 2007/2008 ilitumia shilingi milioni 57 kufanya kazi zifuatazo:-

- Ununuzi wa mitambo 2 ya kusukuma maji (*1 surface pump & 1 submersible pump*);
- Ununuzi wa dira za maji 24;
- Ukarabati wa mabomba ya usambazaji maji na chanzo cha maji; na
- Ujenzi wa vioski 7.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kazi zilizotekelezwa, huduma ya maji kwenye Mji wa Mhunze ambayo ilikuwa imesimama kwa zaidi ya mwaka mmoja imeboreshwa na sasa kufikia takriban asilimia 40 ya watu wanaopata maji.

Mheshimiwa Spika, kwa kazi ambazo hazikutekelezwa katika mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali itaendelea kutenga fedha zaidi kwa utaratibu tuliojiwekea wa kutekeleza miradi inayoweza kutoa matokeo haraka (*Quickwin Schemes*).

MHE. FRED M. TUNGU: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri yaliyotolewa na Serikali, lakini nina maswali mawili madogo tu.

La kwanza, kwa kuwa wakati Rais akiahidi kutoa shilingi milioni 156 tayari Mji wa Mhunze pamoja na vijiji vingine tisa vilikuwa kwenye utaratibu wa *Quickwins* kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri; na kwa kuwa mpaka sasa zimetolewa milioni 57 tu.

Je, Serikali itakuwa na maoni yangu kwamba ni vyema zaidi kazi zilizobaki zenye gharama ya shilingi milioni 100 ziingizwe kwenye Bajeti ya mwaka huu yaani 2009/2010 ambapo itakuwa *quickerwins* kuliko utaratibu ambao ameueleza Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Makofi*)

La pili, kwa kuwa karibu na Makao Makuu ya Mji wa Kishapu kuna chanzo kizuri sana na kinaweza kikawa endelevu kama kitafanyiwa ukarabati na chanzo hicho kuna Bwawa.

Je, Wizara itazingatia maoni yangu kwamba upo umuhimu wa kukarabati Bwawa hilo lililopo ili liweze kuwa chanzo cha pili na endelevu zaidi katika zile kazi ambazo zimebaki za karibu shilingi milioni 100 na ziingizwe katika mpango wa Bajeti wa mwaka huu 2009/2010. Ahsante sana.

NAIBUWAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa nimshauri kwamba hizi *quickwins* tunazozitungumza ni utaratibu ambao tumeuweka ili angalau watu waweze kupata matokeo au waweze kupata huduma ya maji kwa haraka zaidi.

Shilingi milioni 100 zinaweza kabisa hata sasa hivi zikatengwa katika utaratibu huu wa *quickwins* badala ya kusubiri mpaka ifike muda wa Bajeti.

Mheshimiwa Spika, kinachojitokeza ni kwamba tuna upungufu na utaratibu mzima katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya kwa sababu wataalam wanapoleta maombi ya fedha mara nyingi unakuta inachukua muda mrefu sana mpaka yapitishwe na Wizara kwa ajili ya kupewa fedha.

Sasa hivi tumebuni utaratibu mpya kwamba tunapeleka vikosi kazi katika Halmashauri za Wilaya ya Wahandisi wetu kwenda kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata katika Mji wa Mhunze Mheshimiwa Fred Tungu napenda nimhakikishie kwamba ni vizuri basi nako tupeleke wataalam wetu wasaidie kuandaa Bajeti hizi za *quickwins* kusudi tuweze kuzipata fedha hizi, na kama kutakuwa na masalia ya kazi basi tutauingiza katika utaratibu wa bajeti inayokuja.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo kwa chanzo cha bwawa jipya ambalo analipendekeza Mheshimiwa Fred Tungu, mimi ninakubaliana na mawazo yake kwamba itakuwa ni vizuri bwawa hilo nalo likawekwe katika utaratibu.

Lakini kama ilivyo kawaida Bwawa halianzi Mheshimiwa Fred Tungu huku Bungeni, basi litaanzia Wilayani wao ndiyo watuambie kwamba Bwawa hilo ni kipaumbele katika Halmashauri yao. Halafu tutaangalia uwezekano wa kuliweka katika Bajeti ya mwaka 2009/2010.

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi ya kuuliza swali ndogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, mimi napenda tu kurejea kwamba Mheshimiwa Rais amekuwa na nia njema sana anapotembelea sehemu mbalimbali na hasa anapoguswa na matatizo yanayowakabili wananchi.

Mheshimiwa Spika napenda kuelezea kwamba Mheshimiwa Rais alitembelea Mji wa Lamadi uliopo katika Jimbo la Busega mwezi Mei 2007 na alishangaa kuona kwamba Mji ule hauna chanzo chochote cha Maji. Kufuatia hali hiyo, aliahidi kwamba Serikali ingejitahidi kuweza kuwapatia chanzo cha maji. Sasa sijui katika utaratibu aliozungumzia Naibu Waziri kwamba anaweza kutuma kikosi kazi. Je, anaweza kutuma kikosi kazi kwenda Lamadi katika Wilaya ya Magu kikusaidia kuanisha kupata chanzo cha maji kufuatia ahadi ya Mheshimiwa Rais?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika majibu ya mwanzo utaratibu unaanzia katika Halmashauri ya Wilaya lakini hatuna tatizo kabisa Wizara yangu itatuma wataalam kutoka Wizarani kuwasaidia wataalamu wale waliopo katika Halmashauri ya Magu ili waweze kuangalia ni vyanzo gani vipya vinawezekana kuangaliwa na hatimaye kutusaidia kupata maji. Ziko aina mbalimbali za vyanzo vya maji na vingine huwa haviwezekani na vingine vinawezekana. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatuma wataalamu kutoka Wizarani kwenda kumsaidia kuangalia suala hili la vyanzo vipya vya maji.

Na. 20

Mikataba Iliyofungwa

MHE. ATHUMANI S. JANGUO (K.n.y. MHE. MOHAMED H. MISSANGA) aliuliza:-

Kwa kuwa, mikataba mingi iliyofungwa kati ya Serikali au Taasisi za Serikali na Kampuni za Kimataifa kutokana na zoezi la ubinafsishaji imedhihirika kuwa ni mibovu na haikuzingatia maslahi ya Taifa kiasi cha kulalamikiwa na wananchi walio wengi; na kwa kuwa, mfano wa Kampuni hizo ni kama *IPTL, CITY WATER, ATCL,*

TTCL/DETECON, TICTS, TRL, NET GROUP SOLUTION/TANESCO, RICHMOND/DOWANS, Mikataba ya Madini na kadhalika:-

(a) Je, ni sababu zipi zilizoifanya mikataba hiyo ifungwe bila kuzingatia maslahi ya Taifa?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kuwa, makosa yaliyofanyika hayarudiwi tena ili kuokoa rasilimali za Taifa letu?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Kila mara Serikali au Shirika la Serikali linapoingia Mkataba na chombo au mtu mwingine yeyote, msingi wake mkubwa huwa ni kuweka mbele maslahi ya Taifa kwa wakati ule na kwa wakati ujao. Maslahi ya Taifa nayo hubadilika kulingana na hali inavyojiri wakati wa mkataba, hali hii inavyobadilika basi mtu anayeuangalia Mkataba huu wakati mwingine, labda miaka kumi baadaye anaweza akasema kwa urahisi kabisa kuwa Mkataba fulani haukuzingatia maslahi ya Taifa, bila kuzingatia hali ambayo ilikuwapo wakati wa kuingia Mkataba ule. Mikataba yote hufungwa kuzingatia maslahi ya Taifa.

(b) Kwa sasa Serikali imeunda timu ya majadiliano ya mikataba – “*Government Negotiating Team*” ambayo ina wataalamu wa fani mbalimbali. Na pale ambapo Serikali haina utaalumu katika fani husika, basi Serikali ipo tayari kuajiri wataalamu kutoka popote pale ili kushiriki katika majadiliano ya mkataba husika.

Aidha, Serikali ina makubaliano na Mashirika ya Kimataifa ya Benki ya Dunia na UNDP ili kutoa mafunzo kwa maafisa wetu katika nyanja ya majadiliano ya mikataba na kufuatilia utekelezaji wake. Hali hii itaboresha uwezo wa Serikali katika kujadili na kuingia mikataba.

MHE. ATHUMANI S. JANGUO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri kwa nini Serikali haikutambua kutoka mwanzo kwamba wanahitajika wataalamu kutoka nje wasaidiane na wa kwetu kwa sababu ninaamini kwamba moja ya sababu ni uwezo mdogo wa wataalamu wetu.

Je, kwa mikataba ambayo Mheshimiwa Missanga ameorodhesha hapa Taifa hili limepata hasara kiasi gani?

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuliambia Taifa hasara tuliyoipata?

WAZIRI WA KATIBU NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwanzo katika jibu langu la msingi mikataba inapoingia kitu kinachozingatiwa ni hali halisi ya wakati ule na huko nyuma tulikuwa tunaamini kabisa tulikuwa na uwezo ila sasa mikataba imezidi kuwa mingi na sio mingi tu pia imezidi kuwa ya katika nyanja ambazo tulikuwa hatuzijui sasa hivi tunaingia mikataba katika nyanja za gesi, nyanja za petroli, mambo ambayo zamani tulikuwa hatuna. Sasa tunahitaji wataalamu kweli ndio maana tumeamua tuwafundishe watu wetu na pia tutafute *consultants* waje watusaidie katika masuala kama hayo. Kwa sasa siwezi kuliambia Taifa ni hasara kiasi gani imeingia na mikataba ambayo Mheshimiwa Missanga ameitaja kwanza mikataba yenyewe ni mingi na si kweli kwamba yote imeleta hasara kwa Taifa, lakini tunaweza tukalifanyia kazi swali hilo ili tujue mkataba upi umeleta hasara na kiasi gani na kama Mheshimiwa Missanga atataka basi tutafanya kazi hiyo tutakuja kuileta baadae hapa Bungeni.

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Katika swali la msingi taasisi zinazoonyeshwa hapa kwamba mikataba yake haikufanyika vizuri ni taasisi zile ambazo ni za msingi na Serikali ndiyo inategemea kwa ajili ya kuendesha uchumi wake, na mikataba yake kila inapowekwa kila baada ya miaka miwili unakuta tayari kuna matatizo. Kutokana na hilo wananchi wameanza kupoteza imani kwa Serikali kwa sababu mikataba inayowekwa kwa siri lakini baada ya muda inafichuka. Je, Serikali haioni kwamba hili ni jambo la hatari ambalo linalipeleka Taifa mahali pabaya kwa wananchi wanaopewa dhamana wanaweka mikataba mibovu na kuitia Serikali hasara kubwa?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, ni kweli taasisi ambazo Mheshimiwa Missanga amezitolea mfano katika swali lake la msingi ni taasisi ambazo ni za msingi katika maendeleo ya Taifa letu. Na kwamba kunajitokeza matatizo ya mara kwa mara msingi wake ni kwamba kila unapoingia mkataba unajikuta katika hali misingi ya mkataba ule inakuwa *dictated* na ile hali halisi ya wakati ule. Unapoingia mkataba kwa mfano wa kununua mtambo wa kuzalisha umeme wakati nchi yako inakaa giza wakati huo unapoingia mkataba huo nchi ipo giza masaa 16. Kwa hiyo, wewe unakuwa umeshika makali mwenzako ameshika mpini. Kwa hiyo, mnaingia mkataba katika hali hiyo baada ya muda *on hind sight* ndio watu wote tunakuwa *wise* tunasema pale tulikosea.

Lakini tukitizama mazingira ya wakati tunapoingia mkataba ule tungeu-*appreciate* jinsi ya ukweli wake hasa.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba kinachoangaliwa ni maslahi ya Taifa, na kwa kuwa amesema vile vile kwamba maslahi ya Taifa yanaangaliwa kwa wakati ule ambapo kuna shida au kunahitaji kubwa. Lakini Mheshimiwa Waziri anajua kwamba mikataba kama ya *TTCL/DETECON*, mkataba wa

RITES, mkataba wa *TANESCO*, ni baadhi ya mikataba ambayo ilisemewa sana katika hatua ile ile ya awali ikiwemo na Bunge lenyewe. Je, ni nani sasa ambaye Waziri anataka kuiambia nchi hii kwamba ana mamlaka ya kuamua kinachoitwa maslahi ya Taifa. Je, hao ambao wameamua hayo kwa maslahi ya Taifa na kuacha kuwasikiliza Watanzania ikiwemo Bunge lao wakasababisha hasara kubwa wanachukuliwa hatua gani sasa?

SPIKA: Sasa hayo ni mawili kinyume na Kanuni. Kwa hiyo nitakuachia Waziri uchague lipi kati ya hayo mawili? (*Makofi/Kicheko*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, nizungumzie hili la maslahi ya Taifa. Kimsingi maslahi ya Taifa yanaelekezwa yanakuwa *represent* na Serikali iliyoopo madarakani wakati ule. Serikali hii ndio Serikali ya wananchi, ndio Serikali ya Taifa. Kwa hiyo, yenyewe ndio itakuwa inachagua nini maslahi ya Taifa na ndio itaingia mikataba kwa misingi hiyo. Sasa inawezekana watu kule nje wakasema haya si maslahi ya Taifa na watu wengine mahali pengine popote wakasema pia kwamba haya si maslahi ya Taifa lakini Serikali ile inakuwa na jukumu na ndio inakuwa *responsible* kwa kweli.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa ruhusa yako

Mheshimiwa Spika, Waziri wakati anajibu swali alisema kwamba wakati mwingine mikataba inaingiwa kutokana na mazingira yaliyopo pale ndio makosa yanatokea. Je mazingira hayo hayatengenezwi? Kwa sababu kwa mfano tatizo la ukame Tanzania, kwamba tutahitaji umeme linajulikana mapema sana inakuwaje Serikali inaingia kwenye mkataba mbovu kwa kutumia mazingira ya wakati huo wakati mazingira ya hali hiyo inajulikana mapema. Hivi sasa tuna tatizo la ukame na kesho kutwa tutakuwa na tatizo tena la umeme. Kwa hiyo, mazingira haya hayaonekani kama yanatengenezwa kwa makusudi Mheshimiwa Spika? (*Makofi*)

SPIKA: Sijui ni ya hali ya hewa ama sidhani.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, kwa kweli matatizo ya mambo ambayo hatuwezi kuyatabiri matatizo ambayo ni ya kiasilia si rahisi ukayapangia mkataba. Utaingia mkataba baada ya tatizo maana mkataba unatakiwa ku-*solve* tatizo mkataba hauji hivi hivi tu. Hata sheria tunavyozitunga tunatunga sheria ili kutatua tatizo fulani au kutatua hali fulani. Sasa si rahisi kwa Serikali kujua kwamba mwaka ujao hakutakuwa na mvua au mwaka huu hakutakuwa na mvua sidhani kama kuna mtu anaweza akafanya kazi hii pamoja na kwamba tunacho chombo chetu cha kutuambia hali ya hewa. Lakini vyombo hivi vimegundulika si Tanzania tu dunia nzima kutokuwa sahihi sana kwa kumfanya mtu akaingia mkataba kwa sababu yao.

Na. 21

Mahakama ya Mwanzo Wilayani Lushoto

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO aliuliza:-

Kwa kuwa, wakati wa kutunga Sheria Na. 3 ya Mwaka 1998 ya kuanzisha Chuo cha Mahakama Lushoto (*Institute of Judicial Administration (IJA)*), kwa kupitia michango ya Wabunge, Serikali ilikubali kuwa, kuna umuhimu wa kuboresha majengo ya Mahakama ya Mwanzo zilizo karibu na *IJA* ili ziweze kuwa mfano bora kwa mazoezi ya wanafunzi:-

(a) Je, Mahakama za Mwanzo zipi zimeboreshwa tangu mwaka 1999 Wilayani Lushoto?

(b) Je, ni lini majengo ya Mahakama za Mwanzo za Bumbuli, Soni, Mgwashi na Vuga yataboreshwa?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna umuhimu wa kuboresha majengo ya Mahakama za Mwanzo zilizo karibu na *IJA* ili ziweze kuwa mfano bora kwa mazoezi ya wanafunzi.

Hadi sasa Mahakama ya Mwanzo Dochi, Wilayani Lushoto imeboreshwa kwa kujengwa chini ya mpango endelevu. Aidha, majengo ya Mahakama ya Mwanzo za Bumbuli, Soni, Mgwashi na Vuga yataboreshwa kwa kadiri Bajeti yetu itakavyokuwa inaruhusu. Hata hivyo, tunaomba uongozi wa Wilaya ya Lushoto akiwemo Mheshimiwa Mbunge, uwahamasishe wananchi wa maeneo ya Mahakama hizo waweze, kuweka nguvu zao, kuchangia uboreshaji wa majengo hayo kama inavyofanyika katika ujenzi wa majengo mengine ya utoaji huduma kwa umma.

SPIKA: Tunaendelea, sasa tunaingia kwenye swali la Mheshimiwa Nyami wa Jimbo la Nkasi, kwanza ebu nisaidie hii inaitwa Nkasi au Nkansi?

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, hii inaitwa Nkasi, kama ilivyoandikwa.

SPIKA: Hivi hivi Nkasi?

MHE PONSIANO D. NYAMI: Ndiyo Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Ahsante sana.

Na. 22

Hesabu za Serikali Kutolewa Katika Mfumo wa Kimataifa

MHE. PONSIANO D. NYAMI aliuliza:-

Kwa kuwa, Tanzania kupitia *NBAA* imeridhia kuwa hesabu zake zitatolewa kwa viwango vya Kimataifa “*International Public Sector Accounting Standards (IPSAS)*” na *International Financial Reporting Standards (IFRS)*” na kwa kuwa, ili Mhasibu aweze kuwa makini ni lazima ajue mifumo hiyo:-

- (a) Je, ni kwa nini mifumo hiyo haijawekwa kwenye mitaala ya vyuo vyote vinavyofundisha mambo ya uhasibu/fedha na ni lini itawekwa?
- (b) Je, kuna mpango gani wa kurekebisha Sheria ya Fedha Na. 6 ya 2001?
- (c) (*Public Finance Act 2001*) ambayo haitoi ruhusa au haiagizi utumiaji wa viwango vya Kimataifa?
- (d) Je, Mhasibu Mkuu wa Serikali atasaidiwa je kuhakikisha kuwa, anatengeneza hesabu za Serikali kwa mfumo huo uliotajwa kwenye swali hili?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI) alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Damiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mwezi Julai 2007 Tanzania iliamua kutumia viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa Taarifa na Hesabu Fedha “*The International Public Sector Accounting Standards*”, (*IPSAS*) na “*International Reporting Standards*” (*IFRS*). Katika utekelezaji wa uamuzi huo, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Bodi iliendesha semina kwa wanachama wake kuhusu utumiaji wa viwango hivyo katika utayarishaji wa mahesabu.

(ii) Bodi imeweka vitabu na nyaraka nyingine za viwango hivyo katika duka lake la vitabu ili kuwezesha vyuo na watu binafsi kuvipata kwa urahisi.

(iii) Mwezi Agosti 2007 Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi iliendesha mafunzo kwa walimu (*Training of Trainers*) kuhusu viwango hivyo. Jumla ya walimu 48, na mshiriki mmoja kutoka *TRA* walihudhuria mafunzo hayo, ambayo yalishirikisha wawezeshaji kutoka *Institute of Chartered Accountants of Scotland (ICAS)*. Mafunzo ya aina hiyo yanatarajiwa kutolewa kwa walimu wengine mwaka huu, 2009.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tayari Vyuo vya Elimu ya Juu vinatumia viwango hivyo katika mitaala yake.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha na Uchumi iko kwenye mchakato wa kufanya mapitio ya vifungu mbalimbali katika Sheria ya Fedha Na. 6 ya Mwaka 2001, (kama ilivyorekebishwa mwaka 2004), na kuainisha vipengele vya mfumo wa “IPSAS” na “IFRS”, ili kukidhi mahitaji ya kuwezesha kuandaa Hesabu za Fedha kwa mfumo wa kisasa na wa Kimataifa. Baada ya kukamilisha zoezi hilo, Wizara yangu itawasilisha Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria hiyo.

(c) Mheshimiwa Spika, ili Mhasibu Mkuu wa Serikali aweze kuendelea kuandaa Hesabu za Serikali kwa Mfumo huo:-

(i) Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) itahakikisha kwamba mfumo wa “IPSAS” unaeleweka na unafanikiwa katika kufikia malengo yake.

(ii) Juhudi zitafanywa za kuongeza fedha ili kutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa Wahasibu na wadau wengine kwa ajili ya kuendelea kufanikisha utekelezaji wa Mfumo huo.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, lakini hata hivyo nina maswali mawili tu ya kupata ufafanuzi.

Kwa kuwa Halmashauri zetu zinapewa fedha nyingi takriban asillimia 90 kutoka Serikali Kuu, lakini kimahesabu haziko chini ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Je, ni utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba hesabu za Halmashauri zitakubaliana na za Serikali Kuu.

Pili, je ni nani atakayehakikisha kuwa hesabu za Halmashauri zinakubaliana na kufuata vigezo vya Kimataifa kama itakavyokuwa katika Serikali Kuu?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli Halmashauri zetu kimahesabu haziko chini ya Mhasibu Mkuu. Lakini ziko chini ya Wizara ya TAMISEMI ambako Afisa Maduhuli ambaye ni *Accounting Officer* Katibu Mkuu ni afisa wa Serikali Kuu. Kwa hiyo, kwa namna hiyo hesabu zao zinatunzwa na hata hivyo Mkaguzi na Mdhhibiti Mkuu wa Serikali ambaye na yeye vile vile anazikagua zile hesabu anahakikisha kuwa viwango hivyo ambavyo vimeanza kutumika kufundishwa katika vyuo vyetu toka mwaka 2004 vinatumika. Kwa taarifa tu hesabu za mwaka huu 2008 ambazo zinatengenezwa zinatengenezwa chini ya mfumo huu mpya wa *IPSAS*.

MHE. ZUBEIR ALI MAULID: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi kuuliza swali dogo sana la nyongeza.

Kwa kuwa katika utekelezaji wa mfumo huu wa *IPSAS* kwanza inatekelezwa kwa kupitia mfumo wa *cash basis*. Napenda kujua ni lini Serikali itakuwa inautumia kwa ukamilifu yaani *a cruel basis IPSAS*?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Mheshimiwa Spika, kwamba mpango huu na utaratibu huu wa viwango vya *IPSAS* utanza kutumika kwenye hesabu za mwaka 2007/2008. Kwa hiyo katika taarifa tutakaziona baada ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu tutakuta kwamba viwango hivi vimeshaanza kutumika.

Na. 23

Huduma za Benki ya NMB – Unguja

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR aliuliza:-

Kwa kuwa, Benki ya *NMB* ni muhimu sana kwa jamii katika kuwapatia huduma za mikopo, misaada na kadhalika; na kwa kuwa Kisiwa cha Unguja hakina huduma ya Benki hiyo.

Je, Serikali imefikia wapi katika uanzishwaji wa huduma ya Benki ya *NMB* Kisiwani Unguja?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli *NMB* haina tawi katika kisiwa cha Unguja. Kutokana na kwamba huduma za kibenki zinahitajika katika maeneo mengi hapa nchini, *NMB* inaendelea kufanya tathmini katika maeneo mbalimbali hapa Tanzania, ikiwa ni pamoja na maeneo ya Kisiwa cha Unguja. Katika kufikia uamuzi wa kufungua tawi la Benki katika eneo husika, vigezo vifuatavyo hutumika:-

- (i) Mzunguko wa fedha katika eneo husika;
- (ii) Uwezo wa jamii wa kulipia huduma mbalimbali za Kibenki; na
- (iii) Kuwepo kwa miundo mbinu kama vile umeme, barabara, mawasiliano ya simu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Benki zinaendesha shughuli zao kwa ushindani, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuwahamasisha wananchi kuanzisha Benki za Wananchi katika maeneo yao. Ni matarajio yetu kuwa wananchi watakapoanzisha Benki zao wataziendesha kwa ufanisi mkubwa na hivyo kutoa huduma za Kibenki kwa gharama nafuu zaidi. *NMB* tayari imeshapata kibali kutoka Benki Kuu cha kufungua matawi zaidi na imeanza mkakati wa kutafuta viwanja au majengo muafaka

katika maeneo mbalimbali ya nchi ikiwa ni pamoja na Unguja. Namwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa wengine wanaohitaji huduma za Benki katika maeneo yao tuvute subira na tuendeleo kusaidiana ili tuweze kufanikisha azma hiyo.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza masuala mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Benki ya *NMB* inasaidia sana miradi ya wananchi. Na kwa ushahidi mzuri ni pale iliposaidia shule yetu ya Wawi kule Chake Chake Pemba ilipowapatia shilingi milioni 8 katika ujenzi wa madarasa matatu.

Hiki ni kitendo kizuri sana kwa Benki hii. Lakini kwa kufanya vizuri Benki hii kwa kuwasaidia miradi ya wananchi je, Serikali inachukua hatua gani ya kuunga mkono Benki hii ili isichoke kusaidia nguvu za wananchi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa Benki hii ya *NMB* ina wateja wengi sana hasa wafanyakazi ama wafanyabiashara wadogo wadogo hawa tunaojiita walalahoi hasa wanawake.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha *ATM* zake kwa sababu wafanyabiashara wadogowadogo wanapenda kuchukua fedha zao pale kwenye *ATM* lakini ukienda *queue* za *ATM* ni kubwa. je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza vituo vya *ATM* zaidi katika maeneo mbalimbali ya Tanzania ili kuondosha usumbufu kwa wateja wake. Ahsante?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE): Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali huiunga mkono Benki hii ya *NMB* ili iweze kusaidia miradi ya wananchi katika maeneo mbalimbali. Nataka nimhakikishie kwamba Serikali tunaiunga mkono Benki hii na huduma nyingi za Serikali zinapelekwa chini ya Benki hii.

Mheshimiwa Spika, pili kuboresha *ATM* zake. Nataka nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli hasa nyakati za mwisho wa mwezi kunakuwa na *queue* ndefu sana katika *ATM* za Benki hii. Tayari Benki hii imeshaliona hilo tatizo na tayari wameshaanza kuandaa mkakati wa kuongeza zaidi *ATM* zao katika maeneo mbalimbali.

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Benki ya *NMB* wameshaweka jengo katika Wilaya ya Bukombe, na kwa kuwa Benki hii waliahidi kufungua tawi toka mwaka jana na sasa hivi shule zote za kata wameambiwa wazazi walipe kupitia Benki. Na Benki kutoka Bukombe, kijiji cha mwisho kabisa mpaka Kahama kuliko na Benki ni kilomita kama 200.

Je, ni lini Serikali itafungua hilo tawi pale Bukombe ili kurahisishia shida ya wazazi kulipa karo pamoja na walimu kwenda kupanga foleni muda mrefu na kuacha kufundisha?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE)
Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba huduma za Benki zinahitajika katika maeneo mbalimbali.

Pale amba po *NMB* itakapokuwa imeshakamilisha tathmini katika eneo husika basi haraka iwezekanavyo wataweza kufungua pamoja na eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliongelea. (*Makofi*)

SPIKA: Hilo ndilo la msingi tathmini. Kwa hiyo, tuendeleo.

Na. 24

Kujenga Minara ya Simu Kata ya Kizara – Korogwe

MHE. ENG. LAUS O. MHINA aliuliza:-

Kwa kuwa, vijiji vya Kizara, Kwemkote, Bombo Majimoto pamoja na vitongoji vyao katika Kata za Kizara vina wakazi zaidi ya elfu kumi (10,000) na kwamba kuna hali nzuri ya kiuchumi katika kilimo na biashara ya magulio makubwa mawili kwa wiki ambayo hukusanya wafanyabiashara kutoka maeneo mbali mbali ya Mkoa wa Tanga:-

Je, ni lini minara ya mawasiliano itajengwa katika maeneo hayo kwani kuna baadhi ya kampuni za simu zimekwishatembelea maeneo hayo lakini mpaka sasa hazijachukua hatua zozote?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Laus Mhina, Mbunge wa Korogwe Vijijini, napenda kutoa maelezo ya ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo huduma ya mawasiliano ya simu katika maeneo yote nchini hususan maeneo ya vijijini ambayo ndiyo yenye wakazi wengi.

Kwa kutambua umuhimu huo, hivi sasa Serikali ipo katika mchakato wa kuanza ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano ambao lengo kuu la mradi huu ni kuimarisha mawasiliano ya aina zote (simu za mezani, simu za viganjani pamoja na mawasiliano ya mtandao-*Internet*) hadi maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo mafupi sasa napenda kujibu swala la Mheshimiwa Eng. Laus Omar Mhina, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo:-

Kampuni ya simu ya Viganjani ya *ZAIN* tayari imeyabaini maeneo mbalimbali ya nchini ikiwa ni pamoja na maeneo ya vijiji vya Kizara, kwemkote, Bombo Maji Moto na vitongoji vyake Wilayani Korogwe ili kuweza kuwafanyia utafiti wa kimasoko na kiufundi na kisha kujenga minara na kuwezesha mawasiliano ya simu ifikapo mwishoni mwa mwaka huu 2009.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya simu ya *VODACOM* tayari imefanya utafiti wa kimasoko kwenye maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge na kuridhishwa kuwa maeneo hayo yanakidhi vigezo vya kibiashara vya kuwa na huduma ya mawasiliano.

Aidha, Kampuni hiyo imefanya utafiti wa kiufundi na kubaini sehemu ya kuweka minara, na hatua mbalimbali za utekelezaji zimeanza.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *ZANTEL* iko kwenye mkakati wa kupanua mtandao wake katika maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa minara ya mawasiliano katika Wilaya ya Korogwe. Tayari Kampuni hiyo imejenga minara katika maeneo ya Gomba, Segera, Maurui, Mazinde, Mulembule Kibaoni na Mombo Marembwe.

Aidha, Kampuni hiyo iko mbioni kupeleka huduma zake kwenye maeneo mengine Wilayani humo ifikapo mwishoni mwa mwaka huu wa 2009.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia itaendelea na jitihada zake kuyashawishi Makampuni ya Simu za Viganjani kuongeza na kuboresha huduma za mawasiliano nchini hasa maeneo ya vijijini ambako mahitaji ya Maendeleo ni muhimu sana.

MHE. ENG. LAUS O. MHINA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Shirika la Simu Tanzania (*TTCL*) linatoa huduma simu za viganjani katika miji mkuu ya Mikoa na baadhi ya miji ya Wilaya. Je, ni lini huduma hii itafika kwenye mji wetu wa Korogwe pamoja na vitongoji vyake?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mhina kwamba baada ya

kumaliza shughuli ya utafutaji fedha kwa ajili ya Kampuni ya *TTCL* mradi wao ambao waliuanza wa *CDMA* utanza tena na namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo yote ambayo hayajafikiwa yatafikiwa. Nia ya Makampuni ya simu ni kutoa huduma na pia kufanya biashara.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa matatizo yaliyozungumzwa na Mheshimiwa Eng. Mhina yanafanana sana na matatizo ya eneo la Ifinga, Muhukuru na eneo la Mgazini katika Jimbo la Peramiho; na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri analitambua tatizo hilo na amesema sasa Serikali kupitia makampuni hayo wapo mbioni kukamilisha na kuondoa hizo kero katika maeneo aliyoyataja.

Je, mbio hizo zinafanana na mbio za kuelekea kuondoa kero katika maeneo niliyoyataja kama nilivyowasilisha tatizo hilo kwenye Wizara yake?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mhagama ameleta swali Bungeni na ambalo tunategemea tutalijibu katika Kikao hiki cha Bunge. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama tulivyomwahidi kwamba kama tulivyowasiliana na Makampuni ya Simu kuona mawasiliano ya simu yanafika Peramiho hasa maeneo yale ambayo ni ya mpakani shughuli hiyo inaendelea.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Spika, kero ya Korogwe na Peramiho inafanana kabisa na kero ya Mbinga Magharibi hasa kwa Shirika la *TIGO*. *TIGO* limejenga mnara pale Lituhi sasa ni mwaka wa tatu, lakini hawajafungua mawasiliano. Ni lini mawasiliano hayo yatafunguliwa?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, sipendi nijibu lini mnara huo utafunguliwa kwa sababu sina hakika kama kweli huo ni mnara wa *TIGO* au ni ile minara iliyojengwa na *TTCL* kwa ajili ya kusambaza simu za *CDMA*. Sasa naomba nilichukue hilo suala ili nilifanyie kazi ili niweze kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwa usahihi zaidi.

Na. 25

Dawa bora ya kutibu ugonjwa wa malaria

MHE. DR. ALI TARAB ALI (K.n.y. MHE. KHALIFA SULEIMANI KHALIFA) aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imekuwa ikitoa matamko mbali mbali kuhusu dawa za kutibu ugonjwa wa malaria hapa nchini:-

- (a) Je, ni dawa gani bora iliyopo nchini iliyothibitishwa na Serikali kuwa inafaa kutibu malaria?
- (b) Je, Serikali inashirikiana vipi na Watanzania wanaotumia dawa za asili ili kukabiliana na tatizo la malaria hapa nchini?
- (c) Je, Serikali inaelewa kuwa, dawa mseto hasa *Amodiaquine* inawadhuru watumiaji?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa, Mbunge wa Gando, lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Dawa Mseto inayounganisha dawa ya *Artemether lumefantrine* au *ALU* kama inavyojulikana kwa kifupi ndiyo dawa bora ya safu ya kwanza iliyothibitishwa na Shirika la Afya Ulimwenguni (*WHO*) na Serikali yetu kwa ajili ya kutibu malaria isiyo kali.

(b) Serikali inatambua kuwa wapo baadhi ya Watanzania wanaotumia dawa za asili kutibu magonjwa mbalimbali. Kwa kutambua na kuthamini mchango wa waganga wa tiba asili katika kukabiliana na magonjwa mbalimbali ikiwemo malaria. Serikali ina kitengo maalum cha Tiba ya Asili pale Wizarani na imekuwa ikishirikiana na waganga wa tiba za asili katika kufanya utafiti wa kisayansi wa dawa mbalimbali za asili zikiwemo za malaria.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu naomba kutoa wito kwa waganga wote wa tiba asili nchini wanaofahamu dawa za magonjwa mbalimbali kuziwasilisha kwenye taasisi zetu za utafiri wa magonjwa ili ziweze kufanyiwa utafiti wa kisayansi.

Endapo dawa hizo zitathibitika kisayansi kuwa na uwezo wa kutibu magonjwa husika, na kwamba upatikanaji wake ni rahisi zitasaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza mzigo wa magonjwa na vifo.

Aidha, kwa mujibu wa sheria za kimataifa wavumbuzi wa dawa hizo wanahakikishiwa kupewa hati miliki ya uvumbuzi wao pale dawa hizo zitakapothibitika kuwa na uwezo wa kuponya.

(c) Mheshimiwa Spika, *Amodiaquine* si dawa mseto. Hata hivyo Serikali ina taarifa kuwa dawa mseto zenye mchanganyiko wa *Amodiaquine* zinaweza kuleta madhara madogo (*side effects*) kwa asilimia ndogo ya watumiaji kama vile uchovu, kizunguzungu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa dawa mseto ya *ALU* ndiyo iliyopitishwa kwa ajili ya tiba ya malaria nchini, naomba kupitia Bunge lako Tukufu kulisitiza matumizi ya dawa hiyo kwa ushauri wa daktari katika kutibu malaria isiyo kali.

MHE. DR. ALI TARAB ALI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza nataka kujua ufanisi wa utafiti huu wa madawa ya kienyeji katika kutibu ugonjwa wa malaria. Swali la pili, ninavyoelewa kulikuwa na jaribio ya chanjo ya ugonjwa wa malaria. Sijui jaribio hilo limefikia wapi?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hatujapata dawa ya malaria kutokana na malaria. Lakini bado utafiti unaendelea katika kitengo cheto cha utafiti wa magonjwa ya binadamu na vilevile katika *Institute ya Traditional Medicine* pale MUHAC.

Chanzo inaendelea vizuri na wiki tatu au mwezi mmoja uliopita taarifa za awali zilizotolewa na wenzetu wanaofanya utafiti huo Ifakara walipewa tuzo kwa shughuli hiyo inayoendelea na niombe tu kama atakuwa na subira Mheshimiwa Tarab kuna swali hapa la Bunge ambapo tunaweza tukatoa na takwimu katika kipindi cha Bunge hili.

MHE. ZAINAB M. VULLU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema dawa ya *Amodiaquine* inaasilimia ndogo sana pamoja na kwamba hakutaja kiwango cha *Side effects*. Lakini kuna madhara makubwa ambayo huwakuta watoto na mama wajawazito na mengine ya madhara hayo hupelekea vifo. Je, ni lini Serikali itahakikisha kwamba itatolewa elimu ya kutosha kwa wauguzi na madaktari kuwa na kipimo cha awali kabla ya dawa hizo hazijatolewa kwa akina mama na watoto ili kupunguza vifo na madhara mengine?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, *side effects* kama nilivyosema ni madhara madogo madogo. Unalenga kutibu kutu fulani lakini haya madhara ambayo hayatabiriki yanaweza yakatokea kwa mtu mmoja au mtu mwingine. Kwa hiyo hivyo vipimo anavyovisema ni vigumu kisayansi kutabiri. Lakini hii dawa ya *Amodiaquine* hatuitumii tena kwa sababu tunazo dawa za *ALU* ambazo zinatoa matokeo mazuri kwa wagonjwa, watoto na wamama wajawazito kama nilivyosema. Kwa hiyo nisisitize tu kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba watu watumie *ALU* kwa sababu imeonyesha mafanikio na hata sasa hivi mwelekeo wa ugonjwa wa malaria unapungua na sasa hivi tunafanya vipimo tuweze kuwa na takwimu.

SPIKA: Mheshimiwa Lucy Owenya, swali la mwisho. Nilikupa nafasi kwa sababu natambua mumeo ni Daktari Bingwa. (*Kicheko*)

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza. Malaria ni ugonjwa ambao unaua watu wengi sana hapa Tanzania; na kwa kuwa dawa za mseto ni ghali sana ambazo mtu wa kawaida hawezi kuzinunua. Dawa zinauzwa kati ya shilingi 6,500/- mpaka 10,000/- na katika Hospitali za Serikali wakati mwingine wagonjwa wakienda huwa hawapati zile dawa zinazotoka *MSD*.

Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka sasa kuhakikisha kwamba dawa zote za malaria zinatolewa bure kama ilivyo kwenye *ARV's* kwa sababu huwa tunapata misaada mingi sana kwa sababu ya ugonjwa wa malaria?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Lucy ni Mke wa Daktari Bingwa ambaye ni mwanafunzi wangu. Ni kweli dawa hiyo ya *ALU* ni ghali karibu dola 10.

Lakini nakubaliana na rai ambayo ameitoa, lakini utaratibu uliowekwa ni kwamba karibu dawa zote ingawa na sisi tunachangia zinatokana na pesa tunazopata kutoka kwenye *Global Fund*. Katika vituo vya Serikali inatolewa bure. Sasa itakuaje katika vituo binafsi ambako ni watu wengi pia wanakwenda huko.

Kwa hiyo, mchakato uliopo ni kwamba tunajaribu kupunguza kufanya hizi dawa zipatikane katika vituo binafsi na Serikali na wiki mbili zijazo tutakuwa na mkutano Nairobi kuzungumzia suala hili.

Lakini niseme tu kwamba mchakato ambao umefanyika kidunia na Shirika la Afya Duniani ni kwamba tujaribu kupunguza hii bei kwa kupunguza dawa yoyote itakayotoka kwenye kiwanda iwe imepunguzwa bei. Inaitwa *global subsidy* na napenda kutangaza kwamba mimi nilikuwa Mwenyekiti wa hilo suala ambalo linazaa matunda sasa hivi.

Kwa hiyo nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Lucy Owenya kwamba hizo dawa zinatolewa bure na Serikali lakini asilimia 40 ya watu wetu wanatibiwa katika hospitali binafsi na haiwezekani tukasema tuwape hospitali za Serikali bure ni lazima twende kwenye hospitali za binafsi vilevile.

Na. 26

Kutengeneza barabara kwa kiwango cha changarawe

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali hutumia fedha nyingi sana kwa kutengeneza Barabara za Mikoa kwa kiwango cha changarawe; na kwa kuwa kila mwaka kiwango cha fedha hizo hizo au zaidi ya fedha za mwaka uliopita hutengwa na Serikali kwa ajili ya kutengeneza barabara zile zile tena:-

Je, Serikali inaonaje hali hiyo.

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mbunge ya kuwa Serikali hutumia fedha nyingi kwa kutengeneza Barabara za Mikoa kwa kiwango cha changarawe na kuendelea kuzifanyia matengenezo kila mwaka. Pamoja na Serikali kutambua umuhimu wa kutengeneza barabara imara za kiwango cha lami ambazo hazihitaji matengenezo ya kila mwaka kwa kutumia fedha nyingi; lakini uwezo wa Taifa kifedha ni mdogo kuweza kumudu kutengeneza barabara nyingi zinazoweza kukidhi ukubwa wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Nchini inahudumia mtandao wa Barabara za Mikoa wenye jumla ya kilometa 19,246. Kati ya hizo kilometa 18,922 sawa na asilimia 98.3 ni za tabaka la changarawe na udongo na kilometa 327 ni za lami sawa na asilimia 1.7. Barabara hizi ni muhimu sana kwani ndizo zinazopita katika maeneo ya uzalishaji na huduma muhimu na kuunganisha Barabara Kuu na pia kuunganisha Makao Makuu ya Wilaya mbalimbali. Kwa hiyo, kutokana na ukubwa wa mtandao wa barabara za Mikoa, Serikali inalazimika kutenga fedha kila mwaka ili kuzifanyia matengenezo barabara hizo kwa lengo la kupitika. Wakati huo huo Serikali inaendelea kutenga fedha katika bajeti ya kila mwaka kujenga kwa kiwango cha lami barabara zetu kwa kadiri bajeti inavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa kwa kiwango cha lami ndiyo, maana imejiwekea *program* ya kujijenga barabara zote zinazounganisha Mikoa kwa kiwango cha lami, ambapo kwa sasa utekelezaji wake unakaribia kukamilika.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Miundombinu lakini nina swali moja la nyongeza. Ukiangalia fedha zinazotumika ni nyingi sana na ukiangalia maisha au *life span* ya barabara zinazotengenezwa ni kati ya miezi sita hadi 10. Barabara zile mvua zikinyesha zinaharibika.

Kwa hiyo, tunatenga fedha nyingine kufanya kazi ile ile. Teknolojia zinabadilika, kuna teknolojia inaitwa *Ota seal surface road*, kuna hii *surface dressing* ambayo lami yake ni lami ya kawaida ambayo ingeweza kutusaidia sana ku-save hizi fedha. Serikali haioni kuna haja ya kufikiria njia mbadala sasa kuliko kuendelea kupoteza mabilioni ya fedha hizi ambazo kila mwaka hatuoni ile thamani yake? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, kimsingi kama tulivyojibu katika swali la msingi kwamba Serikali inaona umhimu wa kutengeneza barabara za kudumu nchini lakini tatizo kubwa sana kama nilivyosema ni uwezo mdogo wa kifedha. Kusema kweli tungependa kama fedha zingetosha kujijenga barabara zote kwa kiwango ambacho hakitengenezwi mara kwa mara ili kuweza kuokoa hizo fedha.

Lakini pili hata katika mapendekezo anayotoa Mheshimiwa Mbunge hapa inawezekana pia kama uwezo wa kufedha unakuwa umepatikana kwa sababu kwa

kufanya hivyo inawezekana kusema kwamba tunaweza kutumia hii teknolojia mpya lakini maana yake tujaribu kuelekeza nguvu zetu katika barabara chache na zingine zikawa hazipitiki. Kwa hiyo, nia na madhumuni hapa ni kuendelea kuzifanyia matengenezo ya mara kwa mara ili ziweze kupitika wakati huo tukijaribu kuendelea kuzitengeneza ambazo ni za lami ambazo ni barabara ya kudumu zaidi.

SPIKA: Natambua Kiongozi wa Upinzani lakini Mheshimiwa Lubeleje halafu wewe utafuatia.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja la nyongeza.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anajua kwamba barabara ya kutoka Mbande, Kongwa, Mpwapwa ni muhimu sana na kwa sababu Mpwapwa sasa hivi kuna madini aina ya rubi. Je, wakati tunasubiri kujengwa barabara hii kwa kiwango cha lami Serikali ina mpango gani wa kufanya matengenezo makubwa kuliko sasa kutenga milioni 100 ambazo hazitoshi?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbande. Kongwa hadi Mpwapwa umuhimu wake Serikali inautambua na kusema kweli barabara hii ni kiungo kikubwa katika uchumi wa Mkoa wa Dodoma si katika hayo madini aliyoyasema ambayo yamegunduliwa hivi karibuni lakini vilevile uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula yanatoka kule Mpwapwa. Sasa swali la kwamba Serikali inafikiria nini kuitengea fedha ya kutosha ni kwamba tatizo letu kubwa hapa ni Bajeti finyu lakini kwa vyovyote vile Serikali itaendelea kuitazama barabara hii kwa jicho la karibu sana kadri itakavyowezekana kuitengea fedha ili iweze kuitengeneza kwa kiwango cha kudumu.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na hizi barabara za changarawe kweli zinatengenezwa mara kwa mara.

Lakini hata hizi barabara za lami zinazoitwa za kudumu, angalia ile barabara ya Sam Nujoma ile ya Chuo Kikuu pale ni barabara mpya haijafunguliwa. Hivi sasa ukipita utakuta ina mawimbi, inamabaka mabaka ya lami tofauti, barabara ile ya *Surrender Bridge* na kadhalika.

Je, Tanzania hatuna *TBS* ya kusema kwamba hii ndiyo *standard* ya barabara inayotakiwa lami ya Tanzania kiasi cha kwamba barabara hizo zinatengenezwa kila siku au ni tatizo lilelile la mikataba ya dharura na kadhalika?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, moja *TBS* tunayo na viwango vya barabara kufuatana na barabara ambazo tunazijenga, kufuatana na viwango mbalimbali vinajulikana. Lakini kwa bahati mbaya sana tumekuwa na matatizo ya wakandarasi wanaofanya kazi.

Mfano ambao ameutoa Mheshimiwa Hamad Rashid wa barabara ya Sam Nujoma tumeuona katika uongozi wa Wizara na tayari mimi mwenyewe nimeshawapa maelekezo *TANROAD* waweze kutathimini kwa kina utendaji katika barabara ile ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa pale ambapo mkandarasi hakufanya kazi vilivyo.

Kila barabara ina darala lake na lazima tupate kazi ambayo inafanana na daraja ambalo tumelitaka lijengwe. Kuhusu utumiaji wa teknolojia ya *Ota-seal* tunajenga kufuatana na ukubwa wa barabara na magari mangapi yanategemewa kupita na ya ukubwa upi.

Teknolojia kama ya *Ota-seal* ni ya muda mfupi na magari machache haiwezi kukidhi kwenye hizi barabara ambazo tunaziita barabara za mikoa. Kwa hiyo, tupo makini kuhakikisha tunaendelea kuwadhibiti kikamilifu ili tuwe na kazi ambazo zinafanana na fedha nyingi ambazo taifa hili tunazitumia.

Na. 27

Kutengeneza Barabara ya Mlowo – Kamsamba

MHE. DR. LUKA J. SIYAME aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Mlowo – Kamsamba ambayo ipo chini ya *TANROADS* imeanza kutengenezwa lakini sehemu kati ya Itumbula na Kamsamba yenye urefu wa kilomita 46 imekosa mkandarasi kutokana na uchache wa fedha zilizotengwa kwa ajili hiyo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha sehemu hiyo inapatiwa fedha ili kuwezesha matengenezo ya barabara hiyo inayounganisha mikoa ya Mbeya na Rukwa bila kulazimika kupitia Tunduru na Sumbawanga kwa usafiri wa Mpanda Urambo na Kigoma.

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame, Mbunge wa Jimbo la Mbozi Magharibi, napenda kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mlowo – Kamsamba ni barabara ya Mkoa (*Regional Road*) yenye urefu wa kilomita 130 ambayo inahudumiwa na Wakala wa Barabara (*TANROADS*). Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Serikali ilipata fedha za kuifanyia matengenezo barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe chini ya mradi wa *Road Sector Programme Support (RSPS-3)* unaofadhiliwa na Serikali kupitia *DANIDA*. Ili kukamilisha utekelezaji wa mradi katika muda mfupi barabara imegawanyika katika sehemu za vipande vitano na kila kipande kutakiwa kipewe Mkandarasi wake. Vipande hivyo vitano ni vya.

Mlowo – Halungu (km 25) Halungu – Nambizo (km 25), Nambizo – Ntungwa (km 30); Ntungwa – Itumbula (km 25) na Itumbula – Kamsamba (km 25). Vipande

vinne vya mwanzo vilivyopo kati ya Mlowo na Itambula vyenye jumla ya urefu wa kilomita 105 vilikwishapata mkandarasi ambapo kazi za matengenezo zinaendelea na zinatazamiwa kugharimu Shilingi 2,179,755/- milioni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kumpata mkandarasi kwa ajili ya matengenezo ya kipande kilichobakia cha Itumbula –Kamsamba, mfadhili ameshauri kuwa mchakato wa kupata mkandarasi usitishwe kwanza hadi Mhandisi Mshauri, *Inter consult Ltd* wa Dar es Salaam anayefanya kazi ya usanifu wa daraja kwenye mto Momba unaotenganisha mikoa ya Mbeya na Rukwa atakapotoa maamuzi ya kitaalam kuhusu eneo linalofaa kwa ujenzi wa daraja. Ushauri unaozingatia lengo la mradi ambalo ni kuunganisha Mikoa ya Mbeya na Rukwa bila kupitia Tunduma na Sumbawanga kama swali la Mheshimiwa Mbunge lilivyogusia.

Serikali kwa kushirikiana na mfadhili wa mradi huo ambaye ni *DANIDA* itahakikisha fedha za matengenezo ya kipande cha barabara kilichobakia kuanza Itumbula hadi Kamsamba zinapatikana pindi gharama halisi za matengenezo zitakapojulikana hasa baada ya eneo linalofaa kwa ujenzi wa daraja litakapobainishwa kitaalamu.

MHE. DR. LUKA J. SIYAME: Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri sana lakini pamoja na majibu yake mazuri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mchakato huu wa usanifu wa daraja la Kamsamba mto ambao unatenganisha Mkoa wa Rukwa na Mbeya hivi sasa limeshachukua zaidi ya miaka mitatu. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kulieleza Bunge lako Tukufu hatua au kiwango cha usanifu kilichofikiwa hadi hivi sasa ili kuwapa matumaini wananchi wa Tarafa ya Kamsamba wapatao 80,000/- ambao kwa zaidi ya miezi sita kwa mwaka hulazimika kutumia zaidi ya siku mbili kutembea huu umbali wa kilomita 25 alizosisema?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, tumesema hapa kwamba fedha hizi za ujenzi wa barabara hii zilitengwa katika mwaka wa 2007/2008. Kwa hiyo, mpaka hivi sasa ninavyozungumza ni mwaka wa fedha mmoja umeshapita. Kwa hiyo, ushauri huu kama ulitolewa si miaka mitatu iliyopita kama ambavyo swali linajaribu kuelekeza. Ni katika kipindi hiki hiki ambacho fedha hizi za mradi zimetolewa. Lakini napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kadri muda unavyozidi kuwa mrefu wananchi wanashindwa kupata uvumilivu. Nimhakikishie tu kwamba katika hatua yoyote ambayo itakuwa imefikiwa hadi sasa Wizara yangu itakuwa karibu sana kufuatilia huo usanifu na kuhakikisha unakamilika haraka iwezekanavyo ili kazi hiyo ikamilike na wananchi waitumie hiyo barabara.

Na. 28

Kusitishwa kwa Michezo ya Majeshi Kila Mwaka

MHE. AMEIR ALI AMEIR aliuliza:-

Kwa kuwa katika historia ya michezo nchini vipaji vingi vya wanamichezo hupatikana katika vikosi vya ulinzi na usalama na hii inatokana na utaratibu wa majeshi kuandaa michezo ya kila mwaka ikishirikisha vikosi vyote vya ulinzi bara na visiwani na kwa kuwa michezo hiyo kwa sasa haifanyiki tena:-

- (a) Je, ni sababu zipi zilizosababisha michezo hiyo isifanyike?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa kutokufanyika kwa mashindano hayo ni njia mojawapo ya kudumaza michezo katika majeshi na kusababisha nchi kutokufanya vizuri katika mashindano ya Kimataifa?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ameir Ali Ameir Mbunge wa Fuoni lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, sababu ya msingi ya kutofanyika kama ilivyokuwa siku za nyuma kwa michezo ya majeshi ni uhaba wa fedha. Fedha kidogo zinazotengwa katika bajeti ya kila mwaka kwa ajili ya michezo hazikidhi mahitaji halisi ya gharama za kuendesha mashindano katika ngazi ya Kombania, Vikosi na hatimaye Kamandi, Kitaifa na Kimataifa. Katika mwaka wa Fedha wa 2007/2008 fedha iliyotengwa kwa ajili ya michezo ilikuwa shs.63.0 milioni tu. Kiasi hiki ni kidogo sana kuliwezesha Jeshi kuendesha michezo kwa jeshi zima kama ilivyokuwa zamani.
- (b) Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba kutofanyika kwa mashindano hayo kumesababisha kudumaa kwa michezo katika majeshi na hivyo kutofanya vizuri kwa timu zetu katika mashindano ya Kimataifa. Taffiti zinaonyesha kuwa uwakilishi wa nchi nyingi katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa hufanywa na vilabu sambamba na waajiriwa na majeshi. Mfano ni umahiri uliowahi kuoneshwa na Col. Juma Ikangaa (Rtd), Meja Filbert Bay (Rtd) na Cpl. Samson Ramadhan. Wote wakiwa ni matunda ya michezo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa michezo Serikali inatarajia kuongeza bajeti ya michezo kadiri uwezo wa kiuchumi utakavyoongezeka. Maeneo ya majeshi yatapelele kipaumbele ili kuendeleza vipaji vya vijana wetu katika michezo na kuliletea Taifa letu sifa za ushindi katika mashindano ya Kimataifa.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika mipango ya Serikali hakuna Wizara hata moja katika bajeti inayokidhi katika matumizi na shughuli za Wizara zinaendelea kama kawaida na kwa kuwa amesema kwamba wamepatiwa shilingi 63 milioni: Je, kutokupata fedha za kutosha katika Wizara yako sawa na kusema kwamba hakuna utaratibu wa aina yoyote au

ubunifu wa aina yoyote na kupunguza matumizi ili shughuli hizi za kijeshi zikaendelea kama kawaida yake?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, ni kwamba si kwamba michezo imesimama kabisa katika majeshi yetu, bado inaendelea lakini kwa kiwango kidogo, tofauti na ambavyo tungependa iwe. Tunapokuwa tunakaribia bajeti, tunapanga bajeti kwa ajili ya michezo, lakini kwa bahati mbaya kiasi kinachopatika ni kidogo mno ukilinganisha na mahitaji halisi. Kwa maana hiyo, michezo inaendelea na hivi sasa timu teule tu ndizo ambazo zinapata fedha hizo kwa ajili ya kushiriki Kitaifa na Kimataifa. Hata mwaka uliopita, kila mwaka tuna michezo yetu ya Afrika Mashariki, Jeshi letu linaendelea na mashindano kama hayo. Lakini ninachosema ni kwamba fedha hazikidhi, siyo kwamba michezo imesimama kabisa.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri alijulishe Bunge hili Tukufu kwamba hivi sasa kule Zanzibar katika vikosi mbalimbali Wizara yake imetoa barua kwamba hakuna ruhusa kwa timu ya mpira kuendelea na mashindano isipokuwa timu moja tu ya *Hardrock* ambayo iko *Premier*. Je, hii timu ya Kipanga ambayo iko daraja la kwanza, Bavuai na *RedSea*, hivi Mheshimiwa Waziri yuko tayari zife kwa ajili ya upungufu wa fedha?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema awali, suala la michezo linahitaji fedha na inapokuwa fedha hizo hazipo maadam fedha zilizokuwepo ni milioni 63 ambazo zimepangwa kwa ajili ya timu teule tu ili ziweze kukidhi kuingia katika mashindano, zile nyingine bila shaka haitowezezana kushiriki kwa sababu fedha hakuna. Hatupendi timu hizo zife, tunachosema ni kwamba tutajitahidi kadri itakavyowezezana katika bajeti zinazofuata kuongeza kiwango hiki ili na timu nyingine ziendelee kushiriki mashindano hayo.

Na. 29

Shughuli Zinazofanywa na JWTZ na JKT

MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI aliuliza:-

Kwa kuwa, Jeshi la Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa lina vikosi vyake vinavyoshughulika na ujenzi na ufundi wa mambo mbalimbali:-

- (a) Je, Jeshi huwa linachukua tenda zozote sehemu nyingine na ni tenda za aina gani?
- (b) Je, daraja la Kyela lililojengwa na Wanajeshi ni la kudumu au la muda mfupi?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, jukumu la msingi la Jeshi la Ulinzi kwa maana ya JWTZ ni kulinda mipaka yetu na kuzisaidia mamlaka za kiraia yanapotokea maafa mbalimbali na hivyo halijihusishi na biashara. Lakini jukumu la JKT pamoja na kutoa mafunzo ya kijeshi kwa vijana wanaongia kwa mujibu wa sheria au kwa kujitolea, lina shirika la uzalishaji mali lililoanzishwa kisheria linaloitwa SUMA-JKT. Shirika hili linajihusisha na biashara mbalimbali zikiwemo za ujenzi, viwanda, ufugaji na kilimo. JKT huchukua zabuni za ujenzi wa nyumba na barabara, utengenezaji wa samani na ushonaji wa nguo za sare mbalimbali ndani na nje ya jeshi.
- (b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali, moja ya majukumu ya JWTZ ni kutoa msaada kwa mamlaka za kiraia wakati wa maafa. JWTZ liliombwa kusaidia ujenzi wa dharura wa daraja la Kyela baada ya kutokea mafuriko. Daraja hilo ni la muda litakalotumia hadi daraja la kudumu litakapojengwa.

MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningependa tu kujua, hilo shirika linajitegemea au vipi na hayo mapato yanayopatikana yanakwenda wapi au yanafanyiwa kazi gani?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zuleikha Yunus kama ifuatavyo:- Shirika la SUMA-JKT ni Shirika linalojitegemea chini ya Jeshi la Kujenga Taifa. Madhumuni ya Shirika hili ni kuzalisha mali ili fedha zinazopatikana ziweze kuliendeleza Shirika lenyewe pamoja na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa hiyo, fedha hizi zinatumika mara nyingi kulipa uwezo Shirika lenyewe liweze kujitegemea zaidi, lakini wakati huo huo linasaidia matumizi mbalimbali ya Jeshi la Kujenga Taifa.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita. Matangazo: nikianza na wageni; kwanza ni maafisa kutoka Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko wakiongozwa na Bibi Joyce Mapunjo, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo. Yupo Bwana O. Majengo, DTM. Ehe! Hawa wapo kweli hawa! Bwana E. Mapande. Nadhani nisiendeleo kuwasoma hawa, nitakuwa nachukua muda wa Bunge bure.

Pia kuna Maafisa kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Makao Makuu wanaongozwa na Mkurugenzi Mkuu Ndg. Humba. Oo, ahsante sana, nimemuona! Karibu sana Ndg. Humba, karibu pamoja na Ndg. Hamis Mdee, Ndg. Sigi Mapunda, Ndg. A. Rehani na Ndg. H. Kawawa, Mwanasheria wa Mfuko.

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine kwa leo ni wageni wa Mheshimiwa Juma Killimbari Mbunge, ambao ni Shekh Abdi Omari Shakitila, Mwenyekiti wa BAKWATA, Wilaya ya Iramba. Yule pale, karibu sana! Mzee Shaban Mdia, Mwasisi wa Chama cha Mapinduzi toka Shelui, Iramba na Shekh Shaban Said, Imam wa Msikiti,

haukutajwa Msikiti wa wapi, nadhani utakuwa humo humo katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge. Karibuni sana na muendeleo kutuombea Dua, tunamtegemea sana Mungu katika shughuli zetu, ahsante sana.

Matangazo ya kazi:- Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, ameniomba nitangaze kuwa leo saa 5.00 asubuhi kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo chumba namba 231.

Mheshimiwa Abdisalaam Khatib, Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara, ameniomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara kuwa leo saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati ya Viwanda na Biashara, ukumbi namba 219.

Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, ameniomba nitangaze kuwepo kwa kikao cha Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira saa 7.00 mchana ukumbi namba 227.

Huo ndio mwisho wa matangazo. Kwa hiyo sasa namwita Katibu atuongoze katika shughuli inayofuata.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Viwango wa Mwaka 2008 (The Standards Bill, 2008)

(Kusomwa Mara ya Pili)

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kukutakia wewe binafsi, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, heri ya mwaka mpya wa 2009. Napenda vilevile kuchukua fursa hii, kumpongeza Katibu mpya wa Bunge, Dr. Thomas Kasilillah na kukipongeza Chama cha Mapinduzi kwa kupata ushindi katika Jimbo la Mbeya Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Viwango Tanzania *(The Standards Act, 2008)* sasa usomwe kwa mara ya pili!

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Mbunge wa Jimbo la Makunduchi kwa kujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri. Hii ni kwa kuzingatia kuwa Muswada huu una umuhimu wa kipekee wakati huu wa kuelekea kwenye uchumi wa soko huru ambapo ubora wa bidhaa na huduma zinapaswa zilindwe kikamilifu. Kama hatua za makusudi hazitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kuleta Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu,

maendeleo ya viwanda, nafasi ya ajira pamoja na nafasi ya wawekezaji vitapotea, pia baa la uharibifu wa mazingira litaendelea kutokea.

Mheshimiwa Spika, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa tumezingatia kwa dhati mchango na maelekezo ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara ambayo imesaidia sana katika kuboresha Muswada huu uliopo mbele yako.

Mheshimiwa Spika, lengo na madhumuni ya Muswada: Muswada unaowasilishwa una lengo la kutunga sheria ya viwango Tanzania ya mwaka 2009 itakayoweka utaratibu wa kuandaa, kutekeleza na kusimamia kwa ukamilifu viwango vya bidhaa na huduma zinazozalishwa ndani na zinazoagizwa kutoka nje. Sheria ya Viwango Tanzania Sura 130 iliyopo haikidhi mahitaji ya kuendana na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia yanayotokea ndani na nje ya nchi ukizingatia uwepo wa mfumo wa mawasiliano na habari wa kuelekea kwenye soko huru linalosukumwa na nguvu za utandawazi.

Mheshimiwa Spika, sheria za kuanzisha mashirika ya viwango zinafanana dunia nzima, siyo ya kipekee kwa Tanzania tu. Hata sheria ya viwango ya Kenya, Uganda na Botswana zinafanana na hii ya Shirika la Viwango Tanzania. Kwa mantiki hiyo, majukumu yaliyomo kwenye sheria hizo ni yale yale. Sheria ya zamani ya TBS ya mwaka 1975 ilikuwa inakosa baadhi ya majukumu ambayo yameongezwa katika sheria hii mpya. Angalia kifungu namba 4(1)(q),(r) na (s). Pamoja na kuongeza majukumu haya, sheria mpya inaipa TBS meno, ukiangalia hasa kifungu 25 na kifungu 30 ambavyo havikuwepo katika sheria ya zamani. Vifungu hivyo vinabainisha hatua zitakazochukuliwa pindi inapobainika kuwepo kwa bidhaa hafifu. Hatua hizi ni pamoja na kuondoa bidhaa na huduma zilizopo sokoni, kutoza faini, kufuta leseni, kutangazia umma madhara ya bidhaa husika, kuweka taratibu za kufanya matengenezo, marejesho au kulipa fidia, kuweka taratibu za kuharibu bidhaa duni au kuzirudisha zilikoagizwa na kuainisha aina ya makosa ambayo yatashughulikiwa na TBS na yale ya kufikishwa mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kazi hii ya udhibiti wa ubora wa bidhaa itafanywa kwa kutambua uwepo na hivyo kushirikiana na taasisi nyingine kama vile *TFDA*, *EWURA*, *FCC*, Shirika la Vipimo na vinginevyo. Sheria mpya inasisitiza kuwepo kwa ushirikiano baina ya TBS na taasisi hizo nyingine za udhibiti na hasa inaonyeshwa katika kifungu 4(1)(j) na kifungu cha 4(2)(b).

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Muswada huu ni kutunga sheria mpya itakayowezesha utekelezaji wa yafuatayo:-

- Kulinda afya na usalama wa walaji, watumiaji wa bidhaa na huduma dhidi ya bidhaa na huduma zenye viwango duni au hafifu.

- Kuanzisha upya Shirika la Viwango Tanzania (*Tanzania Bureau of Standards*) ili liendane na kuwiana na mashirika ya viwango katika nchi jirani, Kanda na Kimataifa.
- Kuainisha majukumu ya Shirika la Viwango Tanzania ya uendelezaji, usimamizi na udhibiti wa viwango vya sekta zote kwa kushirikiana na wadau wa ndani, Kikanda na Kimataifa.
- Kufuta Sheria ya Viwango Tanzania Sura ya 130 kwa lengo la kutunga sheria mpya yenye kuweka utaratibu wa kuandaa na kusimamia kikamilifu viwango vya bidhaa na huduma mbalimbali zinazozalishwa ndani na zinazoagizwa nje kwa kutumia uwezo na uzoefu unaokubalika Kikanda na Kimataifa wa watalaam wa vifaa vya Shirika la Viwango Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mambo muhimu yaliyozingatiwa kwenye Muswada. Muswada umezingatia mambo muhimu yafuatayo:-

- Kudhibiti viwango vya ubora wa bidhaa na huduma zinazozalishwa ndani na kuagizwa kutoka nje ili kulinda afya na usalama wa walaji, watumiaji na kuwa msingi na kivitio cha uwekezaji na kufanya biashara dhidi ya madhara yanayotokana na kutumia bidhaa na huduma zenye ubora hafifu au duni.
- Kuainisha viwango vyenye rejea vya upimaji na ugezi (*physical measurements of standards and calibration*) ili kuendana na kanuni za ugezi za Kimataifa na hivyo kukubalika katika jumuiya ya kikanda na nchi wanachama wa viwango duniani.
- Kutambua uwepo wa sheria nyingine na taasisi za ndani, Kikanda na Kimataifa zinazohusika katika kupanga, kuandaa na kutekeleza masuala ya viwango. Sheria zilizoanzisha na kusimamia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zimezingatiwa kutokana na hoja ya kutumia sheria ndogo ndogo katika kupanga na kusimamia viwango na kupeleka madaraka kwa wananchi.
- Kuainisha makosa na adhabu zitakazotokana na ukiukaji wa sheria hii yakiwepo aina ya makosa yanayoweza kushughulikiwa moja kwa moja na Shirika la Viwango Tanzania na makosa ambayo yanapaswa kufikishwa mahakamani.
- Kutambua na kuweka misingi ya kiushirikiano na taasisi za Kitaifa na Kimataifa na za Kikanda zinazohusika katika kuandaa, kupanga na kutekeleza viwango.
- Hatua za kuchukua pindi inapobainika kuwepo kwa bidhaa zenye viwango hafifu ikiwa ni pamoja na kuondoa bidhaa na huduma zilizopo sokoni, kutoza faini, kufuta leseni, kutangazia umma madhara ya bidhaa na huduma husika na taratibu za kufanya matengenezo, marejeo au kulipa fidia na taratibu za kuharibu (*disposal*).

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu saba zifuatazo:-

Sehemu ya kwanza yenye kifungu cha kwanza hadi cha pili, inahusu masharti ya jumla ikiwa ni pamoja na jina la sheria, tarehe ya kuanza kutumika na tafsiri ya baadhi ya maneno muhimu yaliyotumika.

Sehemu ya pili yenye kifungu cha tatu hadi cha kumi, inahusu kuanzishwa kwa Shirika la Viwango Tanzania pamoja na majukumu yake. Aidha, inaweka masharti ya uanzishwaji na majukumu ya Bodi ya Wakurugenzi, uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania na kazi zake. Aidha, inapendekezwa kuwa Mkurugenzi Mkuu pamoja na maofisa wengine watakaoteuliwa, watakuwa watendaji wa kazi za kila siku za Shirika la Viwango Tanzania.

Sehemu ya tatu yenye kifungu cha 11 hadi 17 inaainisha vyanzo vya fedha na usimamizi wa mapato ya Shirika la Viwango Tanzania. Imebainishwa kuwa Shirika la Viwango Tanzania lina uwezo wa kukopa, kutayarisha ripoti ya fedha na kuiwasilisha kwa Waziri ndani ya muda uliopangwa kisheria. Aidha, inapendekezwa Bodi ipewe jukumu la kuandaa bajeti ya mwaka au kufanya marekebisho ya mwaka na mamlaka ya kuwekeza fedha za Shirika la Viwango Tanzania itakavyoona ina manufaa zaidi

Mheshimiwa Spika, masuala mengine yanayopendekezwa kwenye sehemu hii, ni masharti ya utunzaji wa hesabu za Shirika la Viwango Tanzania na kufanyika kwa ukaguzi wa fedha kwa kila mwisho wa mwaka wa fedha kulingana na sheria inayosimamia fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne yenye kifungu 18 hadi 21 inapendekeza kuanzishwa kwa alama za viwango, masharti kwa muuzaji wa bidhaa au mtoa huduma ya kuandaa hati ya uthibitisho wa ubora wa bidhaa au huduma anayotoa na wajibu wa Waziri kutangaza viwango kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili kuendana na dhana ya misingi imara ya utawala bora (*good governance*) na utawala wa sheria (*rule of law*) na uwajibikaji, inapendekeza kuwa mtu yeyote ambaye hataridhishwa na uamuzi uliofanywa na Waziri, ana haki ya kukata rufaa katika Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano yenye kifungu 22 hadi 30 inapendekeza masuala yanayohusu utekelezaji wa sheria ikiwa ni pamoja na uteuzi wa wakaguzi pamoja na kazi zao. Pia aina ya adhabu zitakazowakabili watakaovunja sheria hii inapendekezwa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya sita yenye kifungu cha 31 hadi cha 35 inapendekeza masharti ya masuala ya jumla kama vile mamlaka ya Waziri kutoa maelekezo kwa Bodi, kinga kwa Serikali, Shirika au Mjumbe wa Bodi dhidi ya madai yanayohusiana na alama za viwango na kutotoa taarifa za Shirika visivyo halali.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya saba yenye kifungu cha 36 hadi ya 38 inapendekeza masuala ya jumla kama vile mamlaka ya Waziri kutunga Kanuni na mamlaka ya kutunga sheria ndogo ndogo. Inategemewa kuwa sheria inayopendekzwa itakuwa na manufaa makubwa ya kukuza uzalishaji wa bidhaa na huduma hapa nchini na kuwavutia wafanyabiashara na wawekezaji wa ndani na nje kuzalisha na kuagiza bidhaa na huduma zenye ubora unaokubalika Kikanda, Kimataifa na hata Kitaifa kwa kukuza ushindani, kuongezeka kwa mapato ya Serikali, kukua kwa fedha za kigeni hivyo kuwepo kwa uwezo wa kulipia uagizaji wa bidhaa na huduma muhimu kutoka nje, kupunguza urari wa biashara na nakisi ya Serikali na hivyo kulinda afya na usalama wa walaji, watumiaji na kulinda na kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa kuwasilisha Muswada huo vizuri kama kawaida yako. Sasa kwa mujibu wa kanuni zetu ni zamu ya Mwenyekiti wa Kamati au Mwakilishi wa Kamati ya Viwanda na Biashara. Anakuja Mwenyekiti mwenyewe, Mheshimiwa Abdisalaam! Mambo haya ya kuachia achia haya...ni vizuri ukashika mwenyewe, haya! (*Kicheko*)

MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB – MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA NA BIAHARA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la Mwaka 2007 niweze kutoa maoni kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara kuhusu Muswada wa Sheria ya Viwango Tanzania wa mwaka 2008 (*The Standards Bill, 2008*).

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nichukue nafasi hii kukutakia wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti na Waheshimiwa Wabunge, heri ya mwaka mpya wa 2009! Napenda vile vile kuchukua fursa hii kumpongeza Katibu mpya wa Bunge Dr. Thomas Kashilillah na mwisho kukipongeza Chama cha Mapinduzi kwa ushindi katika Jimbo la Mbeya Vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilijadili Muswada huu katika Ukumbi wa Ofisi Ndogo ya Bunge uliopo Dar es salaam tarehe 21/22 Januari, 2009. Katika vikao vyake, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu mapendekezo yaliyokusudiwa katika Muswada huu yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu wakiwemo pia wawakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kupitia Muswada huu, Kamati iliwaalika wadau mbalimbali na hivyo kuwapa fursa ya kujadili na kutoa maoni yao kwa nia ya kuboresha. Majadiliano haya yalisaidia sana kuibua mawazo mapya, maoni na hoja muafaka. Maoni ya Kamati kuhusu Muswada huu ni matokeo ya mchakato huo wa kubadilishana mawazo na wadau mbalimbali. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wadau wote ambao

waliitikia mwaliko wa Kamati wa kuja kutoa maoni yao kwa lengo la kuboresha Muswada ulio mbele yetu hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatambua kwa majina wajumbe wa Kamati hii walioshughulikia Muswada huu kama ifuatavyo:- Kwanza, mimi mwenyewe Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbarouk K. Mwandoro, Mbunge; Mheshimiwa Mohamed Chomboh, Mbunge; Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mbunge; Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mbunge; Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mbunge; Mheshimiwa Rostam Aziz, Mbunge; Mheshimiwa Vuai Ali Khamis, Mbunge; Mheshimiwa Parmukh Hoogan, Mbunge; Gaudence Kayombo, Mbunge; Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, Mbunge; Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mbunge; Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o, Mbunge; Mheshimiwa Basil Mramba, Mbunge; Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mbunge; Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mbunge; Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mbunge; Mheshimiwa Joseph Mungai, Mbunge; Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge na Mheshimiwa Abdallah Sumry, Mbunge.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nisome maoni ya Kamati: Nianze kwa kumshukuru Waziri wa Viwanda, Biashara na Masomo, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dr. Cyril Chami na Katibu Mkuu wa Wizara Bi. Joyce Mapunjo kwa maandalizi na uwasilishaji mzuri wa Muswada kwa Kamati ikiwa ni pamoja na ushirikiano mzuri walioonyesha. Matokeo yake ni Muswada uliorutubishwa kwa mawazo ya wengi, hivyo ubora wake unajionyesha wenyewe bayana.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu una madhumuni ya kuanzisha upya Shirika la Viwango Tanzania ili kuboresha mazingira ya kiutendaji kwa kulipa meno na nguvu ili kusimamia vyema suala zima la udhibiti wa viwango vya bidhaa. Ni madhumuni pia ya Muswada huu kutunga sheria mpya ya viwango Tanzania ya mwaka 2008 itakayoweka utaratibu wa kuandaa, kutekeleza na kusimamia kwa ukamilifu viwango vya bidhaa na huduma zitakazozalishwa ndani na zinazoagizwa kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utandawazi na mabadiliko ya kiuchumi na kiteknolojia yanayotokea duniani hivi sasa, pamoja na ongezeko la bidhaa hafifu zinazoingizwa nchini na ili kulinda maslahi ya watumiaji bidhaa na Taifa kwa ujumla, Kamati yangu inaunga mkono uletwaji wa Muswada huu kwa lengo la kufanya mabadiliko yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Kamati imeridhika kuwa Muswada huu ukipitishwa utasaidia sana kumlinda mlaji dhidi ya bidhaa *fake* na hivyo kwa kiwango kikubwa utasaidia Mtanzania kwa kuwa utasimamia afya yake kwa kuhakikisha anapatiwa bidhaa na huduma kwa viwango vinavyostahili.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kamati ni kwamba, pamoja na kutambua umuhimu wa kuendelea kudhibiti bidhaa au huduma zisizo na viwango vinavyostahili, Kamati inaishauri Wizara kwamba uwekwe utaratibu mzuri wa kuwasaidia Wajasiriamali na Wafanyabiashara wadogowadogo ili kuwawezesha kufikia vile viwango vinavyohitajika. Hivyo ni vyema pia shirika hili likawa karibu sana na Shirika la

Kuhudumia Viwanda Vidogovidogo *SIDO*, kwa madhumuni ya kuboresha kazi za viwanda hivyo ili kuweza kufikia ubora unaohitajika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na malengo mazuri ya Muswada huu, mafanikio hayataonekana ikiwa wadau hawataelimishwa vizuri kuhusu masuala mazima yahasuyo viwango na namna sheria itakavyofanya kazi kwa faida yao na Taifa zima. Kamati inatoa ushauri kwa Wizara kuwaelimisha wananchi waelewe vyema umuhimu wa bidhaa na huduma za viwango bora ili kulinda afya zao. (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna Taasisi nyinginezo zinazojishughulisha na masuala ya viwango vya bidhaa kama vile Tume ya Taifa ya Ushindani, Baraza la Ushindani, Wakala wa Vipimo, Tume ya Kudhibiti Chakula na Madawa na kadhalika na kwa kuwa kuna mgongano wa baadhi ya taasisi hizi, Kamati yangu inashauri kuwa iko haja kwa Shirika la Viwango *TBS* kuainishwa kama shirika unganishi lenye kauli Kitaifa kwa masuala mazima ya viwango.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unakusudia kumlinda mlaji kwa maana ya Mtanzania. Pamoja na kuwa masuala ya viwango si ya Muungano ni muhimu masuala kama haya yakaangaliwa upya ili yapelekwe kwenye Tume ya Muungano kujadiliwa na baadaye tuweze kuwa na sheria moja kwa pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kuushukuru uongozi wa Wizara kwa kukubali baadhi ya ushauri wa Kamati moja kwa moja wakati wa mchakato wa kuchambua na kujadili Muswada huu kwenye Kamati. Hata hivyo, Kamati ilikuwa na maoni yafuatayo kwa baadhi ya vifungu:-

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa ziko Kamati kadhaa za kitaalam zinazoandaa viwango vya bidhaa na huduma mbalimbali. Kamati inashauri kuwa Kamati hizo zitambuliwe kisheria katika Muswada huu, ili majukumu yao yaweze kuainishwa ili nazo ziweze kuwajibika kisheria, katika Muswada huu kuwepo kifungu kidogo cha tatu kitakachobainisha uwepo wa Kamati hizo za kitaalam, ikiwa ni pamoja na kutajwa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imependekeza kufutwa kwa maneno yafuatayo, “*and subject to consultation with*” katika kifungu cha 12 ili kukipa kifungu hiki maana halisi iliyokusudiwa kwa maana ya Bodi kupata fedha kwa ajili ya shirika.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 21 kinachohusiana na malalamiko kwa Shirika la Viwango kwa maana ya ukataji wa rufaa, Waziri ndani ya siku 14 Kamati inapendekeza Waziri naye apewe muda usiozidi miezi mitatu kujibu rufaa husika. Aidha Kamati inapendekeza baada ya muda huo kumalizika bila Waziri kujibu ichukuliwe kwamba Waziri amekubali rufaa hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu ya Jedwali inayozungumzia Wajumbe wa Bodi, Kamati inapendekeza kwamba aongezwe mwakilishi mwenye sifa zinazostahili kutoka viwanda vidogovidogo

Mheshimiwa Spika, aidha Kamati iliona ni vyema Wajumbe wote watakaoteuliwa katika Bodi wawe na vigezo vinavyoendana na majukumu ya ushirika ili kuleta ufanisi, hii itasaidia kuzuia uteuliwaji wa Wajumbe kiholela bila kufuata msingi bora wa kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inashauri Mwenyekiti wa Bodi kufahamu au kuelimishwa majukumu yake ili kuepuka migongano na Mkurugenzi wa shirika kama ilivyokwisha tokea kwa baadhi ya Bodi na pia ni vyema Mwenyekiti akawa na mawasiliano na Katibu wake ya mara kwa mara ili kuepuka migongano hiyo.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Naomba kwa mara nyingine niwashukuru tena Waziri wa Viwanda Biashara na Masoko, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Naibu Waziri Dr. Cyril Chami, Katibu Mkuu wa Wizara Bibi Joyce Mapunjo pamoja na watendaji wote wa Wizara walioshiriki kuandaa na kuboresha Muswada huu ikiwa ni pamoja na ushirikiano walioonesha kwa Kamati wakati wote wa kuujadili.

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile nirudie kuwashukuru na kuwapongeza wadau waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao ambayo yametusaia sana. Aidha, naomba kuwapongeza Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Biashara na Viwanda kwa michango yao mizuri na makini ambayo kwa kiwango kikubwa imesaidia sana kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kumshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kasilillah kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi zake bila matatizo na Katibu wa Kamati Ndugu Abdallah Hancha na Ndugu Angelina Sanga kwa kuhudumia Kamati vizuri wakati wote.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. LUCY F. OWENYA-MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA VIWANDA, BIAHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuvusha salama mwaka 2008 na kuniwezesha kusimama tena mbele yenu ili kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Viwango wa Mwaka 2008 (*The Standards Act 2008*) kwa mujibu wa Kanuni za Bunge 86(6) Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, natoa salamu za pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Richard Nyaulawa kwa kuondokewa na mpenzi wao. Aidha, natoa pole kwa familia ya Mheshimiwa Spika kwa kufiwa na mtoto wa kaka yake na vilevile pole kwa Waheshimiwa wote ambao wamefiwa na wapendwa wao.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa pole kwa waathirika wote wa ajali za barabarani, yote haya ni mapenzi ya Mungu na Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe salamu za mwaka mpya wa 2009 kwako wewe binafsi, Naibu Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote. Aidha, napenda kuwashukuru na kuwapongeza viongozi wangu wakuu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed na Mheshimiwa Dr. Wilbroad Slaa kwa uongozi na ushauri mzuri katika shuguli za Bunge ambao umeweza kuleta mafanikio makubwa katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Dr. Mary Nagu, Naibu Waziri Dr. Cyril Chami, Katibu Mkuu wa Wizara Bi Joyce Mapunjo pamoja na timu nzima ya watendaji kwa kazi nzuri waliyoifanya na kuleta Muswada huu muhimu, ni matumaini ya Kambi ya Upinzani Muswada huu unaweza kuwa ni kichocheo cha maendeleo ya viwanda Tanzania na kutuondolea balaa la kuwa jalala la bidhaa haramu ambazo hazikidhi viwango.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani haina pingamizi na Muswada huu. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani inapendekeza mapendekezo yafuatayo ili kuongeza tija katika utekelezaji wa sheria hii:-

Kifungu cha 7(1) kinachohusu uteuzi wa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Viwango, Kambi ya Upinzani inaona kuwa ni mapungufu katika Muswada huu kwa Mtendaji Mkuu wa Shirika kuteuliwa na Rais, ni vizuri Serikali ionyeshe mfano kwa Shirika la Viwango kwa kuweka ajira ya Mtendaji Mkuu kuwa wazi na ya kushindaniwa *competition of qualified individuals*, kwa kutangaza katika vyombo vya habari ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu kuna Watanzania ambao pia wapo nje ya nchi ambao wanaweza kuomba kazi hiyo licha tu ya kupata washindani wenye uwezo mkubwa, kwa mtiririko wa mchakato huu Rais awe na uwezo wa kuidhinisha na siyo kuteua. Kambi ya Upinzani inapendekeza uteuzi ufanywe na jopo la wataalam wenye uzoefu na uelewa wa viwango ili pendekezo hili liwe na maana, Kambi ya Upinzani itawasilisha *schedule of Amendment*.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo katika mkutano wa uwajibikaji wa Mashirika ya Umma, *Public Accountability Conferences* ulioandaliwa na Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma limetolewa pendekezo kuwa watendaji wakuu wa Mashirika wateuliwe na Bodi ya Wakurugenzi kwa kutangaza nafasi hizo kwa lengo la kupata ushindani.

Mheshimiwa Spika, uteuzi wa Wakurugenzi Wakuu kutegemea Rais ni moja ya sababu zinazochangia mapungufu ya utendaji katika Mashirika ya Umma na hatimaye Mashirika hayo kufa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 9 kinachohusu uanzishwaji Wakurugenzi na Idara naomba kunukuu: “*The Board shall establish such number of directorates, departments, and section as may be necessary and proper performance of the function of the Bill*”. Kambi ya Upinzani ingependa kupata ufafanuzi ni kigezo gani kinachotumika kufanya uanzishwaji wa Idara, Kurugenzi, *Section* kuwa muhimu kiasi kwamba Bodi

itakayokuwepo ina uwezo wa kuzibadilisha, *what determines necessity and criteria for the necessity in the cause of the establish the Directorates and Sections.*

Mheshimiwa Spika, jambo hili lina hatari ya bodi husika kujiundia idadi ya kurugenzi bila kujali athari ya gharama ambayo ni mzingo kwa Taifa. Kambi ya Upinzani inapenda vigezo vya wazi viwekwe katika sheria au Kanuni ili kuwe na uhakika Bodi zinafanya maamuzi yenye tija kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 23(1) kinachohusu uteuzi wa Wakaguzi naomba kunukuu: *“The Minister may at the request of the Board by notice published in the gazette appoint any public officer or officer of the bureau as an inspector for the purpose of this Act”*. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa maneno *Public Officer* yatolewe ufafanuzi au tafsiri yake.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kambi; Kambi ya Upinzani inashauri kuwepo na sheria moja ya viwango na kuwepo na mgawanyiko wa kazi na majukumu kitaasisi yanayoeleweka ambayo yatapunguza mwingilio wa kazi ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji kwa taasisi husika, kwa mfano suala la vyakula na madawa lingekuwa chini ya Taasisi ya *Tanzania Food and Drug Authority (TFDA)*, suala la *Industrial products* ambazo haziliwi (*non consumable products*) lingekuwa chini ya taasisi ya *Tanzania Bureau of Standards (TBS)* na suala la ukiritimba (*monopoly*) na ushindani lingekuwa chini ya taasisi ya (*Fair Competition*) na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sheria kutoa mipaka ya kila chombo au mamlaka ili kuondoa mgongano unaoweza kutokea. Kambi ya Upinzani inaona kuwepo na umuhimu wa viwango vya mabasi pamoja na vipuli vyake yanayotumika Tanzania. Tunashauri viwango hivi viwekwe bayana katika sheria hii kama njia mojawapo ya kupambana na ajali za kila siku barabarani.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; Kambi ya Upinzani inapenda kutoa angalizo kwamba zipo sheria nyingi, yapo pia maagizo mengi lakini utekelezaji wake kidogo umekuwa unasuasua. Ni matumaini yetu sheria hii itakapopitishwa itatekelezwa ipasavyo na isiishie kwenye makabati. Aidha, elimu kwa umma ni muhimu kuhusiana na suala zima la kutambua bidhaa zisizokidhi viwango na madhara yake kwa mtumiaji. Tunashauri au kupendekeza kuwa Muswada huu utafsiriwe kwa lugha ya kiswahili ili walengwa waweze kujua haki zao.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa napenda kumshukuru Naibu Waziri Kivuli wangu Mheshimiwa Khadija Al-Qassmy kwa ushirikiano alionipa katika kuchambua Muswada huu, baada ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani ni matumaini yetu yatafanyiwa kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Owenya kwa kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani. Waheshimiwa Wabunge kwa Muswada huu nimepata maombi ya kuchangia

kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge sita kama ifuatavyo na mpangilio huu ndiyo nitakaoufuata wakati wa kuwaita, tutaanza na Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Pindi Chana akifuatiwa na Mheshimiwa Mohammed Sanya, Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Suzan Lyimo na Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, kwa mpangilio huo ataanza Mheshimiwa Anna Maulidah Komu atafuatiwa na Mheshimiwa Pindi Chana.

MHE. ANNA MAULIDAH KOMU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nichangie kwenye sheria hii muhimu hasa kwa wakazi na wananchi wa nchi yetu na tunapoelekea kwenye kuungana kibiashara na Umoja wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwanza ningepomba kuchangia kwenye sheria hii kuhusu ushirikiano wetu wa nchi za Afrika Mashariki, nafikiri tupo katika mazungumzo ya kuunganisha biashara na kama tunaunganisha biashara ni lazima kila nchi sasa hivi itakuwa na sheria yake ya viwango pamoja na sisi tunaunda sheria yetu ya viwango ambayo tunataka tuiptishe katika Bunge letu Tukufu hili. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri hii sheria yetu ya Tanzania ambayo tunaitunga baada ya kuungana na nchi za Afrika Mashariki itabidi tutunge sheria nyingine ambayo itafunika Afrika Mashariki au kila nchi itakuwa na sheria yake, naomba nipatiwe jibu.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu viwango, nchi yetu sasa hivi dunia nzima iko kwenye *crisis za economy* na wenzetu nchi zilizoendelea wanatuma watu kwenda kwenye nchi ambako wanapeleka *order* kutengenezewa vitu vyao kabla vile vitu havijaja katika nchi husika, sasa je, na sisi tutakuwa tayari kutuma watu waende kule kabla vitu vile havijaja hapa au vifaa vile au bidhaa ile haijaja katika nchi yetu iende ikapasishwe kulekule inapotokea ndiyo ije katika nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tumeona mambo mengi vitu vinatoka huko kwenye viwanda wakati hapa tuna kitengo kinaitwa *COTECNA* hii inaangalia bidhaa kabla hazijaja katika nchi yetu lakini cha kushangaza bidhaa zinakuja katika nchi *COTECNA* wanalipwa kwa *percent* hiyo wanayolipwa zaidi ya dola 2000 ya bidhaa, makontena yanaingia katika nchi yetu wao wameshalipwa, vitu vikishafika katika nchi havifai vinakuwa *destroyed*.

Mheshimiwa Spika, hatari kubwa zaidi vinapoangamizwa vitu hivi vinaleta hewa mbaya ya kuchafua mazingira, tumeshaona matokeo mengi sana yametokea, televisheni na vyombo vya umeme vikiangamizwa, haya yanapoangamizwa kunakuwa na hewa mbaya sana kwa afya za wananchi ambayo inasambaa katika nchi yetu hii.

Mheshimiwa Spika, mimi ningepomba Waziri anijulishe tu kwamba hawa *COTECNA* ambao wao wanapitisha bidhaa mpaka sasa tumewalipa kiasi gani wakati nchi inaendelea kwenda kwenye hasara na wananchi wanaendelea kununua vitu ghali kwa sababu ya malipo ya rejareja yanayolipwa kabla ya kitu hakijaja kwenye duka la kuuzia.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu hapa tuna wajasiriamali wakubwa na wajasiriamali wadogo, tunashuhudia watengenezaji wa unga wa ngano na bidhaa zingine za chakula, unga wa ngano unatiwa katika viroba kabla haujakuwa *packed* kwenye mifuko ya plastiki, unatengenezwa unga wa ngano unatiwa moja kwa moja kwenye viroba, unga ule unapopata maji yale maji yanaingia ndani, bahati yako mbaya ukienda ukanunua huo unga umeula!

Mheshimiwa Spika, ninachomwomba Waziri, kabla vifaa vya chakula havijaja kwenye soko tuhakikishe tunavipitia kwanza kwenye *packing* zake kabla havijaingia kwenye soko la ndani na nje, kwa sababu kitu kama unga, mchele ni chakula ambacho tunatumia, kuna mchele unatoka nchi za nje, unakuja unanunua kifuko cha mchele, unakifungua mchele umegandana, mbovu. Ukishatoa pesa mwananchi anasema situpi nitapika hivyo hivyo, nina Mungu wangu atanilinda. Sasa ninachoomba tukishaipitisha sheria hii vitu hivi vyote vipitiwe upya, viangaliwe upya kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, wajasiriamali wadogo wapelekwe kwenye elimu, wafundishwe jinsi ya kutengeneza bidhaa zilizo nzuri kwa ajili ya kuuza nje, kwa sababu sasa hivi, nimekwenda kutembelea akina mama wajasiriamali Ukonga, wanakausha mboga, wakishakausha zile mboga wanatafuta masoko lakini wanashindwa kupata masoko kwa sababu *packing* yao haitambuliki, kwa hiyo hata kama watatoka waseme wachangishane wakafanye njia waweze kuuza mali zao ili wapate hela ya kigeni na nchi ifaidike haiwezekani kwa sababu havijapitia kwenye viwango, kwa hiyo tuwapeleke hawa wajasiriamali wetu kama ni *SIDO* au wapi tuwasaidie ili waweze kutengeneza vitu ambavyo vitaendana na kiwango cha biashara za kuuza nje.

Mheshimiwa Spika, tukija kwenye matunda yetu, nchi hii tuna bidhaa nyingi sana, tuna chakula kingi sana kama tukikubali kuendana na kama tunavyosema tubadilishe nchi hii iwe kijani kwa sababu ya mazao basi hili shirika litasaidia sana katika kuuza vitu vyetu hivi. Kwa sababu kama shirika hili litakuwepo litasaidiana na mashirika mengine kwa ajili ya kuangalia wananchi wetu basi tutapata mashine za kusindika, tutapata viwango, tutapata vitu vya kubandika kwenye viwango vyetu kuonesha kwamba hiki kitu ni *grade one, two* na kadhalika na tutapata biashara nzuri na kama ninavyosema wananchi wetu watafaidika.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba Sheria hizi ambazo zinakwenda moja kwa moja kwa mwananchi ziende kwa Kiswahili, hata kama zitakuwepo kwa Kiingereza kwa sababu ndiyo mfumo wenyewe lakini kwa sababu inamgusa moja kwa moja Mkulima basi apewe kwa Kiswahili. Pia kazi nyingine ambayo naomba pia sisi Wabunge tuifanye tunapounda sheria kama hii ili kuweza kuwanufaisha wananchi wetu basi tunaporudi Majimboni tukafanye kazi ya kuwaelevesha kwa sababu sheria hii itawasaidia sana lakini sasa kama hawajui nini wafanye unakuta tu sheria zinapita wala hawajui kama kuna kitu ambacho kinaitwa sheria ambacho kinawahusu.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri yale niliyomwomba aniambie kwamba tunawalipa kiasi gani hawa *COTECNA* na kazi gani wanafanya. Je,

kweli wanakwenda huko kuangalia viwango vya biashara tunavyoletewa nchini? Naomba jibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Maulidah, sasa namwita Mheshimiwa Pindi Chana wakati huo huo Mheshimiwa Muhammad Sanya ajiandae.

MHE. PINDI H. CHANA : Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu mdogo kuhusiana na Muswada huu unaohusiana na masuala ya viwango.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kuipongeza sana Wizara kwa kuleta Muswada huu wa viwango, lengo lake ni zuri sana, azma yake ni nzuri sana na lengo ni kumlinda mtumiaji au mlaji kutokana na huduma hafifu ambazo kimsingi zinaweza zikatolewa. Kwa hiyo hilo lengo ni lengo la muhimu sana kwa ajili ya kumlinda Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuchangia Muswada huu katika eneo la tafsiri. Katika eneo hili la tafsiri kuna neno *Local Government Authority* ukurasa wa 5, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, iimetoa tafsiri kwamba inamaanisha ni mamlaka kutokana na sheria ya Sheria ya Serikali za Mitaa. Naomba kushauri kama ifuatavyo:-

Sheria hiyo iongezewe namba ya sheria na mwaka wa sheria ambao ni 1982, kwa hiyo pale mwishoni, *The Local Government (Urban Authorities) Act of 1982* na mwaka wake uoneshwe, kwa sababu mara nyingi sheria hizi zinarekebishwa, kwa hiyo ni vema wakanukuu namba hiyo ya sheria na mwaka.

Mheshimiwa Spika, suala la viwango nchini ni la maana sana lakini nikawa natafakari kwamba hizi ofisi za viwango kwa ufahamu wangu ni kwamba ziko Dar es Salaam, sasa sisi watu tunaotoka Iringa huduma hizi za kiushauri wa masuala ya viwango tutazipata wapi? Tunatokea wengine Wilaya ya Ludewa, Njombe, wengine Makete, haya masuala ya viwango tutayapata wapi, vile viazi tunavyolima tunataka tu-*export* nje ya nchi ushauri atatupa nani. Katika yale maeneo kuna maji tunataka tutafute wawekezaji, yale maji tuweke kwenye chupa na baadaye tuweze kuuza. Sasa watu wa maeneo ya pembezoni tutafanyaje wakati ofisi hii iko Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, nina ushauri ufuatao kwa Wizara. Katika Halmashauri zetu tuna ofisi za biashara na kuna Afisa Biashara, majukumu ya Maafisa Biashara wetu si mengi sana, zamani ilikuwa kila mwaka wanatoa leseni, sasa hivi hatukati leseni kila mwaka. Nashauri Wizara iwasiliane na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, wale Maafisa Biashara katika kila Halmashauri wapewe mafunzo ili waweze kutoa huduma hii ya masuala ya viwango.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huo mzima katika nchi yetu upo, Maafisa wale wapo tayari, kazi hiyo wanaweza wakaianza hata kesho. Kwa hiyo, ningependa kujua

nini msimamo wa Wizara juu ya kuwatumia Maafisa Biashara kuhusiana na masuala haya ya viwango.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana shirika hili la *TBS* pamoja na shughuli ambazo wanafanya pia wawe wanatoa mafunzo kwa watu wetu, watoe elimu, wafanye maonesho ya jinsi ya kupandisha na kutunza viwango vya bidhaa zetu za Kitanzania, kwamba isiwe tu kumlinda Mtanzania kutokana na bidhaa hafifu lakini upande mwingine wa shilingi iwe ni pamoja na kuongeza viwango vya bidhaa tunazozalisha Tanzania, maana yake huku tunasema kumlinda kwamba labda zile zinazolingia, lakini vipi kuhusu viwango vyetu kuongeza hadhi?

Mheshimiwa Spika, tunahitaji watu wetu wapewe elimu, wapewe utaratibu wa ku-*pack*, tunda moja linalotoka Afrika Kusini unaambiwa mia sita, la kwetu la Mtanzania ni shilingi hamsini, hiyo elimu ni nani jukumu lake kuwapa Watanzania, lazima iwe ni shirika la viwango, mafunzo na utaratibu wote shirika hili la viwango liwe ndilo jukumu lake. Kwa hiyo zile ofisi za biashara zifanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo imeelezwa kwamba kutakuwepo na Bodi katika Muswada huu, hiyo Bodi jukumu lake limeelezwa katika ibara ya (5) ambalo litakuwa ni kuangalia shughuli za kila siku, naomba ninukuu kwa Kiingereza kama ilivyoandikwa: “*There should be a Board of Directors*”. Ibara ya (6) imeeleza kwamba kazi ya Bodi ni *Management and Control of Bureau*.

Mheshimiwa Spika, tukienda ibara ya 20 inatuambia kwamba Bodi hiyo hiyo itakuwa na jukumu la kusikiliza *objection* kutoka kwa watu mbalimbali wanaolalamika. Nilipoangalia watu wanaounda Bodi ni maafisa kutoka Wizara mbalimbali na mashirika mbalimbali ambao kimsingi wanaingia kwa mujibu wa nafasi zao, sasa hili jukumu la kusikiliza *objection* kwa maoni yangu ni jambo ambalo yamkini inabidi lifanyike kila siku au kila baada ya siku mbili, tatu, sasa hawa wanaounda Bodi ni watu ambao wana kazi zao maalum, haiwezekani kuacha kazi zao kule kuja kusikiliza *objection* hapa kila siku, inawezekana Bodi kwa mwaka inakutana mara nne au mara tano, je, ina maana kwamba hizo *objection* kwa mwaka zitasikilizwa mara nne au mara tano?

Mheshimiwa Spika, tutambue kwamba wanaoleta hizo *objection* ni wafanyabiashara ambao ni wawekezaji wa ndani ya nchi na nje ya nchi, wamewekeza hela nyingi. Kunapokuwa na *objection* na hii Bodi inasikiliza hizo *objection* sidhani kama inafanana sana na majukumu ya Bod. Lakini pia nikawa natafakari Bodi ikianza kusikiliza *objection* maana yake inakuwa inafanya *operational activities*, yaani kazi za kila siku za shirika hili la viwango, je, hii Bodi ikitaka kuhoji mambo ya ndani na yenyewe inakuwa imeshiriki kufanya kazi ya kila siku itaweza?

Mheshimiwa Spika, kazi ya Bodi ni ku-*control and management* hasa hili jukumu la kusikiliza *objection* ushauri wangu lisipewe Bodi, Bodi iangalie kazi za kila siku, masuala ya kusikiliza *objection* kama yalivyopendekezwa pale kwenye ibara ya 20(3)(2) yabaki kwenye Shirika lenyewe la *TBS*. Endapo mtu aliyelalamika kupeleka *objection* hajaridhika anaweza akakata rufaa kwa Waziri kwa mujibu wa Muswada huu na endapo

atakuwa hajaridhika anaweza akakata rufaa tena Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara ingawa Mahakama Kuu, Kitengo cha Biashara wakati mwingine ikina viwango vyake maalum vya kupokea zile kesi, yaani kesi za thamani ndogo ndogo labda za laki mbili, milioni moja haziendi huko, lakini kwa kuwa hii itakuwa ni *appeal* kwa hiyo viwango vyovyote vile vitaruhusiwa, lakini *otherwise* katika Mahakama Kuu *Commercial Division* kuna viwango vyake maalum.

Mheshimiwa Spika, huo ndio ushauri wangu, kwamba hii Bodi isipewe majukumu ya kusikiliza *objection*. Sababu ya kwanza ni kwamba wale wajumbe hawatakuwa pale kila siku, ni wajumbe ambao wanatoka katika taasisi mbalimbali, kwa sababu atakuwepo mwakilishi wa sekta binafsi, mwakilishi kutoka Elimu ya Juu, mwakilishi wa Wizara ya Fedha, mwakilishi wa Afya, mwakilishi wa Viwanda na Biashara, mwakilishi wa Mwanasheria Mkuu hawa wote wana majukumu yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ili uweze kusikiliza *objection* unahitaji utalaam fulani wa jinsi gani ya kusikiliza. Kwa hiyo, jukumu hili liwe ndani ya taasisi na Bodi iwe inakuja kuangalia masuala ya *control* na *management*, kimsingi huo ndiyo ulikuwa ushauri wangu mkubwa na suala la kutumia Maafisa Biashara katika Wilaya zote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya ushauri wangu huu ni imani yangu kwamba Muswada huu ni mzuri ukitekelezwa utasaidia sana Watanzania hususan masuala ya viwango. Lakini pia iko haja ya Shirika hili la Viwango kuwasaidia Watanzania kuongeza viwango vya bidhaa zao, ziko bidhaa ambazo zinadumu *durable*, ziko bidhaa ambazo zinaharibika haraka kama mazao ya nyanya, vitunguu yaani *perishable*, kwa hiyo Shirika hili la Viwango liwe ndio kinara wa kuongeza kwanza viwango vya Watanzania na vilevile kuwakinga dhidi ya huduma hafifu za bidhaa.

Mheshimiwa Spika nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono Muswada huu. (*Makofi*)

MHE. IBRAHIM MUHAMMAD SANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza nikupe pole kwa kufiwa na mtoto wetu nyumbani na niwape pole wale Waheshimiwa ambao wamepata misiba mbalimbali pamoja na mwenzetu aliyefariki kule Mbeya Vijijini. Vilevile niwatakie heri ya mwaka mpya kwa miaka yote miwili mwaka wa Kiislamu na mwaka huu wa 2009.

Mheshimiwa Spika, nataka kuchangia kidogo kuhusu *TBS* na huu Muswada ambao umeletwa. Ni vizuri na umekuwa wakati muafaka kwa vile Tanzania ni wadau wa biashara na hatuwezi kujitenga na ulimwengu wa leo kwamba kila kitu tunaweza kutengeneza wenyewe bila kuagiza au tukanyimwa uhuru vilevile wa kusafirisha bidhaa zetu. Lakini madhara ninayoyaangalia hapa ni madhara ya namna mbili katika viwango hivi. Kuna madhara ya kiafya ambayo ndio mara nyingi sisi kama Waheshimiwa Wabunge au Watanzania wa kawaida huwa tunaelewa labda madhara ya kiafya hutokana na chakula na madhara ya pili ni madhara ya kiuchumi. Nataka niangalie pande zote mbili kwa ufupi kabisa kwamba madhara ya kiafya yanatokana na chakula ambacho

tunakitumia aidha, tunakitengeneza wenyewe kwa maana tunakizalisha mashambani mwetu au tunaagizia kutoka nchi za nje.

Lakini kuna madhara ya muda mrefu ya kiuchumi, Watanzania ni maskini, mara nyingi huwa tunachangachanga hela zetu kwa ajili ya kuwa na maisha bora, mtu anapotaka kujenga nyumba, anapotaka kununua gari au chombo kingine cha kumsaidia hata vifaa vya nyumbani, anategemea anapokwenda dukani anapata kifaa ambacho kitadumu kwa muda mrefu, lakini matokeo yake anauziwa kitu ambacho hakimpi manufaa yeye na badala yake kinampa madhara ya kiuchumi kwa sababu muda alitegemea kutumia chombo kile au kifaa kile haufikii.

Mheshimiwa Spika, tuchukulie mfano, unanunua *television*, inaweza ikakupa madhara mawili kwa wakati mmoja, unaweza kununua televisheni ambayo haina kiwango itakupa madhara makubwa na itaharibika mara moja ikawa umetumia fedha nyingi ulizochanga lakini zikapotea kwa kipindi kifupi, *television* yako haifanyi kazi. Lakini madhara ya kiafya vilevile *television* inatumia vifaa fulani vya kurushia picha katika *screen* yake. Kama ukiangalia na zikawa *television* ambazo hazina viwango zinaweza kuharibu hata macho yako na familia yako.

Kwa hiyo, nasema Watanzania tuna tabia ya kuruhusu watu kuja kuwekeza lakini tunachokitegemea sisi, wanapokuja watu kuwekeza wanakuja na (*capital*) mtaji na wanakuja na *technology* ambayo itatusaidia. Kwa hiyo, akija na *capital* nzuri na *technology* ya kisasa atatoa *employment*, akitoa *employment* anatengeneza njia mpya ya vijana wetu kupata kazi katika nchi yao. Vile vile atapata soko la ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, leo inastaajabisha kuwaruhusu watu kujaa nchini mwetu halafu wao wakawa wafanyabiashara wanashindana na biashara za watu wa ndani wakapewa leseni za kuagizia bidhaa. Utampaje mgeni kuagizia bidhaa kutoka nchi za nje na tunao mfano hai kabisa, nafikiri mwaka jana tu kulikuwa na mfanyabiashara wa Kichina ameleta bidhaa, bidhaa zile zikaonekana hazina kiwango matokeo yake akawa anatafutwa hakuonekana yuko wapi, hajulikani hapa Tanzania alipo wala nje hana *invest* aliyoacha na kalitelekeza kontena lake kuja Dar es salaam. *As a result* bidhaa zile zikapigwa moto na ndio alivyoelezea Mheshimiwa Mama Komu kwamba pale vinapopigwa moto vifaa sio tumezuia tu kuingiza bidhaa mbovu nchini lakini tumepata madhara kwa sababu unapopiga bidhaa moto inatoa gesi fulani ambayo inaharibu mazingira.

Kwa hivyo wewe umesema kwamba umetoa agizo biashara ipigwe moto lakini unapopiga moto humuumizi yeye peke yake, lakini mfanyabiashara yule angekuwa Mtanzania, ungejua unamfuatilia wapi, leseni yake ni nambari gani, amepewa kibali na nani kuagiza mali ile sio tu mtu anatoka nchi za nje anakuja hapa, keshona kwamba hapa pana biashara, anaagizia makontena ya biashara, halafu makontena yanalundikana, uchunguzi unapofanyika unaonekana bidhaa feki inapigwa moto, ni hasara kwetu sisi hasa kiafya.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotaka kuzungumzia ni kuwa, soko la ndani likimilikiwa na watu wetu na tukawapa mwamko wa kufungua viwanda vidogo vidogo. Tusikubali kila kitu kifanywe na watu kutoka nchi za nje, matokeo yake tunaona mikataba mingi tu ya biashara, tulizungumza ndani ya Bunge hili hili inakwenda kombo, tunakula hasara, wawekezaji wanakuwa ni waongo, wanakwenda kinyume na taratibu ambazo tumekubaliana. Tutazame mambo ambayo yametufika hivi karibuni kutokana na reli ya kati na tulichangia hapa, tukazungumza madhara yake na haraka za kuwapa hawa watu, mambo ndio huwa kama yalivyo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nizungumzie ni kwamba, kama alivyozungumza Mheshimiwa Pindi Chana kwamba haya mambo yasifanyike tu kwa ajili ya Mji Mkuu wa Dar es Salaam, kuna Mikoa iliyokuwa nje ya Dar es Salaam na hizi bidhaa zinakuwa na sehemu tatu za kuingizwa katika nchi mbali zinazotengenezwa ndani. Kuna zile zinazokwenda kupitia bandari kuu kama ya Tanga, Dar es Salaam na Mtwara vile vile zinazopita viwanja vyetu vya ndege na nyingine zinapita mipakani kwenye *entry point* zetu. Kwa hiyo, katika maeneo hayo yote kunahitajika kuwe na watalaam wa kuweza kudhibiti biashara zile ili kinachoingia kijulikane kwamba kina kiwango kinachotakiwa na Serikali yetu kwa ajili ya matumizi ya watu wetu. Kwa hiyo, kuwe na maabara za kisasa. Huwezi tu ukaanzisha *TBS* ukawa huna maabara za kisasa.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka mwaka jana au mwaka juzi nchi ya New Zealand ilifanya uchunguzi mpaka kwa vitambaa vinavyoagizwa Uchina kwamba rangi inayotumika katika vitambaa vile ilikuwa na madhara kwa binadamu. Kuna kipindi fulani tungekuwa tunafuatilia vipindi vya biashara za nchi za nje kuna nchi kama Uingereza na Marekani zilizuia kuagiza *toys* kutoka China kutokana na matatizo ya madhara ya kiafya ambayo yangepatikana baada ya *toys* kutumika katika nchi zao. Kwa sababu kila kitu kina kiwango chake, aina gani ya *toys*, *materials* aliyotumia kutengenezea *toys* hata rangi vile vile ili kulinda afya za watoto wetu na afya za walaji pamoja.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu chakula na madawa. Madawa yapo ya kila aina hata hapa Dodoma ukipita barabarani kwenye mabaraza kuna madawa ya Kichina ambayo hayakuandikwa hata kwa lugha nyingine, yameandikwa kwa lugha ya Kichina peke yake. Sasa hujui matumizi yake yanatumikaje, unayatumia wakati gani, kutwa mara ngapi. Sasa unaponunua sabuni kama zile, unaponunua dawa za meno kama zile unaponunua madawa mengine ya ngozi, baada ya muda tunapata madhara na hasara kwa sababu matibabu yake yanakuwa ni ghali na Serikali ndiyo inayobeba mzigo ule. Kwa hiyo, tuwe *careful* na madawa.

Mheshimiwa Spika, vile vile tuwe waangalifu na chakula ambacho kinauzwa katika *supermarkets*. Nafikiri Watanzania tusiwe na tabia tu ya kuwa na *tendency* ya kwenda *supermarkets* kwa sababu una fedha unakwenda *supermarket*. Unaweza ukapata hata matunda au *juice* zilizokuwa *fresh* sokoni kuliko hata *supermarket*. *Supermarket* ni vitu ambavyo vimetengezwa na kuwekwa madawa ambayo baadaye yanaleta taathira katika mwili wako na katika maisha yako.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni *furniture*, tunapendelea sana hata Serikali yenyewe inafanya makosa makubwa sana kwamba Wizara zote zimejaa *furniture* kutoka Malaysia, China, Indonesia, *why?* Nimepata mfano mzuri tu hapa Bungeni kwetu ndani ya Bunge hili meza yetu hii hapa imetengenezwa na SUMA-JKT, *look the difference*, hii ni *original*, hii ni *genuine*, ni mbao hii wanaweza kuja Maspika mbele wakaikuta hii meza iko hivi hivi. Lakini *what I am telling you*, hatuwezi tukamaliza hata vipindi vitatu au vinne hizi meza na viti vitabadilishwa tu kwa sababu hizi ni *fibres* tu, wana *pressing machine* zao, wana *paint* wanatuletea, lakini hii meza ni ya mbao na mbao ni zetu kwa nini tusafirishe mbao tusiagizie wataalam wa kutengeneza *furniture* wakawa-*educate* watu wetu katika vyombo kama vya SUMA-JKT tukatengeneza mbao na *furniture* kwa ajili ya Wizara zetu, kwa ajili ya Ofisi zetu na vingine tukasafirisha nchi za nje, tukawa ni wasafirishaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, muda ni mfupi lakini kuna mengi tu, kuna vitu vya *electronics*, tunaagiza makompyuta *used*, kompyuta *used* ni hatari sana, kompyuta *used* kukupa 100 na kukupa moja mpya ni bora hiyo moja kutokana na athari zake na wale ni wajanja wenzetu ni wjanja wakishakuzitumia wakaona kwamba hizi zimekwisha muda wake wanatufanya dampo kwa kutugawia kwa sababu wanajua kwamba hizi zina madhara kama hazija-*expire* zitabaki kwao. Kwa hiyo matokeo yake sisi tunaona kama tumepata msaada *NGO's* imetuletea zawadi, zipigwe marufuku kabisa kabisa *electronics* za kompyuta kuingia katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, vifaa vya ujenzi hasa umeme vinaweza vikaleta taathira kubwa sana *you can build a house of billions of shillings* kumbe umetia *wire* za umeme feki, baadaye zinakuja kuleta hasara zinalipua nyumba yako zinamaliza kila kitu. Kwa hiyo utakuta kwamba kile ulichokiweka kwa muda mrefu kikusaidie kinaleta taathira na athari kwa nchi yetu na Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, lingine ni *spare parts*, *spare parts* sio tu za mabasi hata watu wa kawaida wanatembelea kwenye gari zao ndogo, *motor bicycle* hizi ziwe *spare parts* ambazo ni *original* na unapokwenda dukani siku hizi wanakuuliza sasa unataka *genuine* au unataka namba *two* ukimwambia namba *two* inakuwa ni ile ya rahisi ambayo labda inatoka nchi ambazo hazina viwango lakini unaitumia muda mfupi na inaweza ikaleta ajali katika barabara, ikapoteza maisha ya Watanzania. Kwa hiyo tuwe tayari na sisi kuwapa leseni watu ambao wanaagiza vitu japo ni ghali kidogo lakini vitu vinavyoweza kusaidia na kudumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho tujaribu na sisi sasa kuyapa uwezo mabengi yetu kuamsha ari ya Watanzania kujiunga kwa pamoja ili vikundi hivyo viweze kutengeneza viwanda vidogo vidogo na hivi viwanda vina kodi kubwa sana *it is quite impossible* kwamba wewe huwezi ukafungua kiwanda, unaweza ukafungua kiwanda, lakini hebu angalia tuchukulie mfano khanga, unapo *import* khanga kutoka *Bombay*, inafika mpaka Tanzania khanga inauzwa elfu tatu, lakini khanga inakuwa *produced* Tanzania inauzwa elfu nne mpaka elfu nne na mia tano, na ukiuliza kitu gani kinachorejesha nyuma kwanini khanga ambayo *imported* imelipiwa usafiri, imelipiwa ushuru wa hapa na bado inakuwa rahisi kuliko ambayo inatengenezwa Tanzania. Tatizo lenyewe ni kwamba kodi

zimekuwa kubwa, bei ya umeme ni kubwa, wapunguziwe kodi na umeme uwe rahisi, pamba tunayo, tusafishe pamba yetu tungeneze vitenge, tutengeneze khanga na hatimaye tuweze kusafirisha badala ya sisi kuagiza nguo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tunayo pamba ni jambo la aibu kabisa kabisa kuona kwamba sisi tuna pamba lakini nguo tunaagiza. Utaona leo vitu *used* kama viatu, viatu vinaagizwa kutoka nchi kama Mashariki ya Mbali lakini havina viwango vinaleta madhara, ngozi zake ni uwongo sio ngozi *plastic* yenyewe ni mbovu, soli zenyewe haziendi sio *scientifically made* kwamba hiki anaweza akavaa binadamu na hawezi akakiagizia kutoka Uingereza cha *hush puppies* au *grasshoppers* au *clerk's* kwa sababu ni *too expensive so is better* leo mtu ananunua kiatu cha mtumba kinakuwa ni bora kuliko kipya kilichotoka Mashariki ya Mbali, kwanini? Kwa sababu wale wenzetu kule Ulaya na Marekani tayari wana viwango, wafanyabiashara *fake* ambao wanatengeneza zile bidhaa hawana viwango, matokeo yake sisi ndiyo tunavamia soko lile tunaleta bidhaa inakuwa ni rahisi kwa mlaji, lakini matumizi yake ya muda mfupi na yanaleta madhara kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ningepomba tu hiki chombo ambacho kimeleta huu Muswada leo kiweze kupewa meno ya kufanya kazi zake kisheria na kisifanye kimabavu kwa kuonyesha chuki dhidi ya wafanyabiashara, wafanyabiashara ni sehemu ya Watanzania, ni sehemu ya watu ambao wanawasaidia Watanzania kiuchumi kwa kupata *revenue* kutoka kwao. Lazima tuweke hekima, tuwasomeshe, tuwaelimishe, tuwatafutie nchi za kuagizia bidhaa, tuwatafutie makampuni bora ya kuleta bidhaa ili Tanzania iweze kung'ara kwa wafanyabiashara na walaji.

Mheshimiwa Spika, nategemea kwamba Tanzania ni nchi makini, ina viongozi makini na sisi Wapinzani tupo tutasaidia tutakapotakiwa kutoa ushauri na ushauri wetu mara nyingi unakuwa ni mzuri kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu. Sisi hatupo hapa kwa ajili ya kusaidia chama tuko hapa kwa ajili ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri njoo na timu yako sisi tuko tayari kukupa maelekezo na kukusaidia ili Tanzania iondokane na bidhaa *fake* na ili Watanzania wapate bidhaa ambazo ni bora kwa afya zao na kwa uchumi wao. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. SUZAN A. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia Muswada huu wa viwango hasa ukizingatia kwamba wewe ni Spika wa Viwango.

Mheshimiwa Spika, nia ya Muswada huu ni kuipa meno zaidi kiutendaji na kusimamia vizuri udhibiti wa viwango vya bidhaa ndani na nje ya nchi yetu. Nakubaliana kabisa na Muswada huu kwamba umefika kwa wakati muafaka kwa sababu kwa kweli kwa sasa hivi utakubaliana nami kwamba, kuna bidhaa nyingi sana zinazolingia nchini. Vile vile bidhaa nyingi zinazolingia nchini sasa hivi kutokana na utandawazi na soko huria, zimekuwa siyo za viwango ambavyo vinastahili katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, suala la viwango kwa kweli ni suala muhimu sana hasa tukizingatia bidhaa zile ambazo ni za vyakula.

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia kimsingi unakuta kwamba *TBS* kuna muingiliano mkubwa sana na *TFDA*. *TFDA* ambayo ni mamlaka ya madawa na vipodozi hapa nchini. Hata nikiangalia katika *schedule of amendment* utaona kwamba katika ukurasa ule wa 24 mfano, hata wale *members* wa hii Bodi unakuta kwamba hakuna mjumbe yeyote kutoka *TFDA*. Kwa hiyo, naona kwa kweli kuna haja kabisa ya *TFDA* kuwa mjumbe kwa sababu bidhaa nyingi zinazolingia nchini hasa vyakula zinahusu afya za wananchi. Kwa hiyo, naona kuna haja kabisa ya *TFDA* na *TBS* kukaa kuona ni jinsi gani wanaweza kutoa ufafanuzi ni namna gani na ni nani atashiriki katika suala zima la bidhaa hasa zile zinazohusu afya za binadamu.

Mheshimiwa Spika, pia kuna suala zima la *trademarks*. Tumeona kwamba kuna baadhi ya wafanyabiashara wanakuwa na *trademark* lakini unakuta anaihodhi lakini haitumii. Kwa hiyo, mtu mwingine akitaka kufanya ile biashara inashindikana. Kwa hiyo, nilidhani kuna kila sababu ya Wizara kuhakikisha kwamba kama mtu ana ile *trademark* basi ahakikishe anaifanyia biashara na asimzuie mwenzie kufanya kwa sababu kwa kweli inakuwa ni tatizo kubwa, mtu anahitaji biashara ile ambayo haipo lakini kwa kuwa kuna mtu tayari ana ile *trademark* inakuwa ni vigumu sana kwa mtu mwingine kuifanya hiyo biashara au kuipata hiyo *trademark*.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la taratibu za kazi, ukiangalia ibara ya 23 unakuta kwamba ukurasa wa 17 Waziri anaweza kuteua: “*The Minister may at the request of the Board by the notice publishing in the gazette appoint any public officer or officer of the bureau as an inspect for the purpose of this Act*”.

Mheshimiwa Spika, ninavyojua ni kwamba Serikali ina taratibu za kazi za ajira. Sasa kama Waziri anakuwa na mamlaka ya kuajiri mtu naona hapa kuna tatizo kwa sababu yeye pia ni binadamu, anaweza akaajiri mtu ambaye hana sifa au pamoja na kwamba ana sifa labda ikaleta matatizo baadaye. Kwa hiyo, naomba suala la ajira lifuate taratibu za kawaida.

Mheshimiwa Spika, lakini suala la udhibiti wa viwango kwa kweli naomba nilizungumzie kwa kina. Nina hakika kabisa kwamba *Tanzania Bureau of Standards* wanafanya kazi zao lakini tunajua kwamba Tanzania ni nchi kubwa sana yenye mipaka mirefu na kwa hiyo mara nyingi sana bidhaa nyingi pamoja na kwamba zingine zinapitia bandarini, lakini nyingine zinapita katika njia tunazoita njia za panya. Kwa hiyo, nafikiri kuna haja kabisa ya wao kuwa na *staff* wa kutosha lakini vile vile washirikiane na taasisi nyingine ambazo zinafanya kazi kama za kwao kwa mfano *TFDA* na wengine ili waweze kukagua vizuri bidhaa zinazolingia nchini.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine ambalo tulilizungumza na hata jana nilijaribu kuligusia, suala zima la *TRA* huwa wanaruhusu baadhi ya bidhaa kupitishwa bila kukaguliwa. Hili limezungumzwa na tumekuwa tunazungumza sana. Nina wasiwasi kwamba baadhi ya bidhaa zinaweza zikawa ni bidhaa ambazo ni vyakula au madawa

ambayo yanaweza yakaingia nchini moja kwa moja bila kukaguliwa na hivyo kusababisha wananchi wakapata madhara na hasa tukijua kwamba sasa hivi soko limekuwa huria na bidhaa nyingi zinaingia na watu wanaweza wakatumia mwanya huo kuingiza bidhaa ambazo kwa kweli zitakuwa zinawaathiri sana wananchi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kuzungumzia kuhusu viwango. Kama ambavyo nimesema kutokana na soko huria wananchi wengi sana wajasiriamali na wengine wameamua kuingia kwenye biashara ndogo ndogo na kubwa na ukienda hasa kwenye masoko makubwa kama Kariakoo utaona bidhaa nyingi achilia nguo lakini bidhaa kwa mfano za umeme ambazo zimeshazungumzwa kidogo, kwa kweli hizi zimeleta madhara makubwa sana na naamini hata mara nyingi nyumba zinapoungua wanasema zinatokana na umeme, nadhani tatizo kubwa linakuwa ni zile nyaya za umeme ambazo nyingi zinakuwa ziko chini ya kiwango. Kwa hiyo, kumekuwa na tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, siyo tu nyumba kuungua, unakuta mara nyingi vifaa vya umeme kwa mfano redio zinazonunuliwa sasa hivi, TV na vingine vingi unanunua unakaa siku mbili, tatu, tayari imeshaungua. Kwa hiyo, naomba udhibiti ule wa muhimu, lakini udhibiti huu hautakuwa wa muhimu kama hawana vifaa. Sijajua Wizara imejiandaa kiasi gani kuwa na vifaa bora vya kisasa ambavyo vinaweza kabisa kugundua kwamba bidhaa hii ni *fake* kwa sababu kila siku tunapata taarifa kwamba bidhaa mbalimbali zimegunduliwa kwamba ni mbovu. Lakini linachukua muda mrefu sana na unakuta tayari watumiaji wameshazitumia.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ni mwaka jana tu tumesikia tatizo hili la maziwa kule China ambayo yalikuwa na *chemically* inaitwa *Melanin* sijui Tanzania kwa kiasi gani wamejiandaa, nakumbuka *TFDA* walisema kuna baadhi ya maziwa yamepatikana kutoka Afrika Kusini nayo yalikuwa yana chembechembe hizo. Kwa hiyo, sijajua *TBS* hapo imeingia kiasi gani. Kwa hiyo, naomba pia tuone ni jinsi gani tuna vifaa vizuri sana vya kisasa. Lakini pamoja na hilo tuwe na watalaam, watalaam ni muhimu sana ambao wataweza kututhibitisha kwamba bidhaa zinazoingia nchini ni nzuri ili Tanzania isije ikabakia kuwa dampo la bidhaa kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, hayo yalikuwa ya jumla lakini nikija kwenye Muswada wenyewe tukiangalia katika ibara ya 20 ukurasa wa 14 inasema: “*The Minister may on the recommendation of the bureau and subject to the provision of this section, by notice published in the gazette declare a standard for any commodity or for the manufacturing, production, processing or treatment of any commodity to be a compulsory standard....*”

Mheshimiwa Spika, suala la kuwa *compulsory standard* yaani viwango vya lazima, nimesoma Muswada wote lakini sijaona mahali popote ambapo huu Muswada unaeleza sababu na misingi ya kisheria ambayo inaweza kusababisha nchi kutangaza viwango vya lazima, inaeleza tu sababu lakini ule msingi wa kisheria sijauona mahali popote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kutokana na hilo itakuwa vigumu sana kwa wadau kujua wanadai nini kama hakuna ule msingi hasa kwamba hiki ni kiwango cha lazima. Uko wapi msingi wa kisheria unaonyesha hiyo kwamba kutakuwa na sababu hiyo? Kwa hiyo, naona kuna haja pia Muswada ubainishe hizo sababu za msingi kisheria zinazofanya viwango vya lazima. Kwa sababu hata ukiangalia katika viwango vya *East Africa* wao katika Jumuiya ya Afrika Mashariki wanavyo, wanazo sababu za msingi za kisheria, zipo tano na wamezieleza kifasaha. Kwa hiyo, nadhani ni muhimu na Muswada huu pia ueleze sababu zipi za Kisheria ambazo zinafanya nchi kutangaza viwango vya lazima.

Mheshimiwa Spika, pia katika kifungu cha 23 mpaka 24 hapa inaelezea kabisa jinsi gani ukaguzi utafanyika. Lakini kama ambavyo nimesema awali kuna muingiliano mkubwa sana kati ya *TBS* na *TFDA*. Ukiangalia yule mkaguzi anaenda kwenye maeneo yote mpaka yale masuala ya madawa na vipodozi, lakini sasa huyu ni mtu wa *TBS*, na sisi tunavyojua *TFDA* ndiyo wana wataalam wazuri wa afya, tunao na tunawaona. Sasa nilikuwa naomba kujua huyu mtaalam wa *TBS* anahusikaje na yule *TFDA* kwa sababu hapa imeonyesha anakwenda sehemu zote na sehemu hizi vilevile zinakaguliwa na mtu wa *TFDA*? Kwa hiyo, naomba kupata ufafanuzi wakati Waziri anakuja kuhitimisha atwambie huu muingiliano kwa sababu ninavyoona huu Muswada kwa kweli umefanya sasa ule muingiliano umekuwa mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhimitisha atueleze vizuri mipaka ya *TBS* ni ipi, na mipaka ya *TFDA* ni ipi? Kwa sababu watakapokuwa wanagongana *inspectors* itakuwa ni tabu kwa sababu hii ni Serikali moja. Kwa hiyo, tunafikiri ni vyema kabisa kuwe na mipaka ya kazi. Vinginevyo kama wanampa *TFDA* ijulikane ni *TFDA* au kama wote wanafanya kwa pamoja, lakini naona kufanya kazi kwa pamoja Taasisi mbili tofauti ni tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, nadhani hapo kuna tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, labda la mwisho, nizungumzie suala zima la jinsi gani, tunahitaji kuwe na elimu sana kwa umma kuhusu viwango vya bidhaa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo wengine wamesema sasa hivi kwa mfano, mtu unaenda dukani, wale wafanyabiashara hawaoni aibu wanasema unataka *genuine* au *second class.*, ina maana hao wafanyabiashara wanajua hivyo. Lakini mtu anadhani kabisa kitu kile cha bei ndogo labda ndicho kizuri. Kwa hiyo, naona kuna haja kabisa ya Wizara kutoa elimu kwa umma ni jinsi gani wanaweza kupata bidhaa au wafanyaje ili waweze kupata bidhaa ambazo zina ubora na wajue kweli kama *value for money* inafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo niliyosema nakushukuru, lakini namwomba Waziri ajaribu sana kufafanua huu muingiliano wa kazi kati ya *TFDA* na *TBS*. Nashukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Susan Lyimo, namwita sasa Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir ambaye ndiye mchangiaji wa mwisho kwa Muswada huu. Mheshimiwa Hafidh karibu.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na pia namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Muswada huu, lakini nami kabla sijaendelea nichukue nafasi hii kuwapa pole wale wote ambao wamefikwa na misiba mbalimbali wakati tulipokuwa hatujakutana. Lakini pia niwatakie wananchi pamoja na Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kheri ya mwaka mpya pamoja na wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii mia juu ya mia na niitakie kheri tu *TBS* baada ya kuleta Muswada huu iweze kufanya kazi zake vizuri kwa niaba ya Tanzania na kwa niaba ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, la kwanza kabisa pamoja na Muswada huu kuletwa, lakini ningeomba tena *TBS* isimame imara zaidi baada ya kupitishwa Muswada huu katika kuhakikisha mambo yote ambayo tunayapitisha yanasimamiwa vizuri na yanachukuliwa hatua kwa mujibu wa taratibu na sheria tulizoziweka hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nikisema hivyo, ukiisikiliza *TBS* katika maelezo yake utaona wanaelekea sana moja kwa moja pale ambapo bidhaa inaingizwa ama kutoka nje, ama kutoka katika viwanda vyetu mbalimbali. Lakini *TBS* bado ina nafasi nyingine baada ya bidhaa hiyo kufika na kufanyiwa kazi, lakini iangalie pia basi utumiaji wa bidhaa yenyewe hiyo inamsaidia Mtanzania au haitomletea madhara Mtanzania pale ambapo bidhaa hiyo itatumika. Sasa sijui watafanya njia gani ili kuona kwamba bidhaa iliyoingizwa inatumika vizuri na inamsaidia Mtanzania na haitompa maradhi.

Mheshimiwa Spika, nitakupa mfano mdogo ambapo kuna bidhaa nyingine hapa huwa zinaingizwa kwa mfano, mafuta ya kupikia. Tunapoingiza mafuta ya kupikia hapa nchini hasa yale yanayotumika kwa *chips* na mambo mengine. Siku hizi umeanza mtindo mwingine, sasa hili sijui *TBS* watakuja kumwambia nini Mheshimiwa Waziri. Watanzania tunaweza kuingia katika madhara makubwa baada ya kuja mtindo wa kununua mafuta, mkaanga *chips* na yeye anaongeza na mafuta ya *transformer*, anaongeza mafuta ya *transformer* kwa sababu ya kutafuta njia muafaka au asipate hasara kwa kumalizika upesi mafuta yake.

Mheshimiwa Spika, sasa ukiangalia mafuta ya *transformer* madhara yake hatujayajua, sasa *TBS* watashirikiana vipi na Taasisi nyingine katika hili baada ya kuhakikisha mafuta yale yapo na ya mwanzo yamekubalika? Lakini kuna nyongeza hii inafanywa, sasa hii imenitia wasiwasi, naiomba *TBS* labda ije kutuambia watashirikiana vipi au watafanya mpango gani ili kuona kwamba wananchi wa Tanzania hawaathiriki na mambo haya.

Mheshimiwa Spika, lingine katika hili hili, tunapokea mafuta ya aina mbalimbali hapa ya nywele na ya mambo mengine. Yanaweza yakawa yako katika kiwango lakini siku hizi akinamama wameshavumbua mtindo mwingine hapa, mafuta haya ya *transformer* yanatiwa kwenye nywele. Sasa sijui hapa ndugu zetu hawa watatusaidia vipi. Pia kuna mambo mengine nitayasema mbele huko yananita wasiwasi katika afya kwa kutumia vitu kama hivi. *TBS* hapa naongea wajikaze zaidi na nikasema wasimame imara zaidi katika kuhakikisha vitu vinavyoingia na vile ambavyo vilikuwa hapa vinatumiwa vizuri na havileti athari kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba *TBS* inaushirikiano na wenye viwanda nchini, limezungumzwa sana hili. Kwa kweli ningewaomba sana *TBS* baada ya kupitishwa Muswada huu ikawa wanaangalia sana viwanda vyetu na kuwa vile viwango vikawa viko pale katika hatua inayotakiwa. Isiwe wanaviacha viwanda wanatengeneza bidhaa kwa ajili ya kusafirisha nje na *TBS* wakahakikisha kwamba bidhaa zile ziko katika kiwango kwa ajili ya kupeleka nje. Lakini kuna bidhaa nyingine zikawa zinatengenezwa katika viwanda vilevile ikawa ni bidhaa za kuwaletea Watanzania. Sasa unapofika mahali katika kutazama viwango utaona labda kiwango hiki kwa sababu kinakwenda nje anakwambia ni hivi hivi ndio tunaleta Tanzania. Lakini ndani ya viwanda huenda kukawa na utaratibu mwingine wa kutengeneza vitu vikawa vinaleta matatizo kwa wananchi wetu hasa katika matumizi.

Mheshimiwa Spika, mfano hai, utakumbuka katika ujana wako na wengi wa hapa tulikuwa tunanunua viberiti, viberiti hivi vya kawaida vya kuwashia moto. Lakini kumbuka kibiriti ambacho ulikuwa unakitumia wewe Mheshimiwa, sasa hivi unaweza ukawasha kibiriti nusu hakijawaka. Sasa haya ni matatizo, nani anaangalia viwango hivi? Ulipokuwa unatumia kiwembe, hiki hiki kiwembe cha kawaida cha chapa mamba kwa mfano, unaweza ukakitumia kiwembe kile labda siku mbili, siku tatu, wiki wakati mwingine, lakini kanunue kiwembe sasa hivi. Sasa viwango hivi vinatazamwa vipi? Siku nyingine katika viwanda vyetu huwa wanatengeneza viwembe labda kwa sababu ya nje lakini sisi Watanzania wakatuona hatuna maana, wakatuletea viwembe vibovu. Sasa na hili ningependa *TBS* waliangalie, viwango vya aina hii kwanini? Kibiriti kweli utawasha njiti saba, kumi hakijawaka! Haiwezekani. Sasa kuna bidhaa nyingi za aina hii zinatoka katika viwanda vyetu, bado *TBS* hawajaweza kuangalia ubora na viwango vinavyotoka katika viwanda hivi.

Mheshimiwa Spika, kingine nilikuwa nataka niwanasihani sana *TBS*. *TBS* ni taasisi yetu ambayo tumewapa kazi kubwa sana ya kulinda maisha ya Watanzania, kulinda afya za Watanzania, lakini kulinda mambo mengi ambayo yanatugusa moja kwa moja sisi Watanzania. Kutokana na hilo nimeingia hofu kidogo na ninawanasihani *TBS*, sisemi kwamba lipo lakini nawanasihani sana, waangalie sana suala la rushwa. *TBS* wasikaribishe rushwa katika taasisi hii. Pindi watakapokaribisha rushwa katika taasisi hii maisha ya Mtanzania, mwenendo wa Mtanzania utakwenda pabaya. Kwa sababu rushwa ikikaribishwa maana yake itaharibu utaratibu wote wa *TBS*. Itaweza kuruhusu mambo yote ambayo yalikuwa hayatufai yakaingia katika Tanzania. Itaruhusu bidhaa hizi ambazo zimezungumzwa hapa kutoka nje, mafeki na nini yote yaingie katika Tanzania.

Sasa ningewaomba sana katika suala hili waliangalie kwa sababu kila binadam ana mambo yake.

Mheshimiwa Spika, nazungumza hivi kwa sababu kuna *element* ambazo nimeziona za harufu harufu ya rushwa katika *TBS*. Sasa nalizungumza hili ili kuweka hadhari kabisa ili wenzetu hawa waweze kujikinga na wasiweze kuingia katika hali hiyo, watusaidie sisi Watanzania tuwe katika hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, lingine ni *TBS* na mafunzo ya wananchi, hili limezungumzwa sana na nalitilia mkazo. Nalitilia mkazo kwa sababu ni jambo muhimu na ni jambo ambalo linaweza likasaidia sana. Mafunzo yatasaidia sana ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, *TBS* ni chombo kinachofanya kazi ya Kitaifa sasa hivi. Kule Zanzibar, kuna wananchi ambao huwa wanasafirisha embe bolibo na huwa wanasafirisha shokishoki kwenda nje. Sasa hawa wenzetu wanapokea kule huwa hawatazami wakasema hii inatoka Zanzibar wanasema hii inatoka Tanzania. Sasa kama *TBS* haikushirikiana na taasisi inayoshughulika na mambo kama hayo ya usafirishaji wa mazao kama haya, Zanzibar, basi tunaweza tukapata sifa mbaya na mazao yetu yakaweza kuingia katika hali mbaya. Lakini elimu kwa wananchi itasaidia sana katika mikoa yetu yote, itasaidia ili kuweza kutengeneza vitu vizuri ambavyo vitasaidia kuleta sifa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini *TBS* na bidhaa za nje ni jambo muhimu sana na hapa ninataka nizungumze mambo ambayo yako wazi sana. *TBS* wanatafuta viwango lakini bado kuna hofu ya kupokea bidhaa ambazo zina matatizo ndani ya maisha ya Mtanzania. Nichukue mfano hai, wakati tulipokuwa tuna matatizo ya umeme, umeme ukawa wa mgao. Tumepokea majenereta ya ajabu ajabu hapa nchini na wenzetu wafanyabiashara walichukua nafasi ile kwa kuona kwamba sasa hivi nikipeleka jenereta la aina yoyote ile linapokelewa. Kutokana na sababu hii *TBS* nao wakalegeza kamba, wakaona kwamba aah, kwa sababu kuna matatizo ya umeme basi acha tu. lakini unalinunua jenereta leo, ukienda kuliwasha nusu saa limekwisha halifanyi kazi lakini umeshatumia laki tatu na nusu. Umesham-*cost* Mtanzania laki tatu na nusu mpaka nne kutumia kununua jenereta ambalo anakwenda kujihifadhi kwa sababu ya umeme lakini jenereta halifanyi kazi, anarudi palepale, sasa haisaidii.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo pia naomba *TBS* waangalie sana ni bidhaa hizi kutoka nje, bado zina matatizo, hata katika mambo haya ya anasa. Kwa mfano wale akinamama wanaopenda kutumia *perfume* na sisi akina baba tunaotumia mambo hayo, nataka tujiulize hivi *brute* ambayo ulikuwa unaitumia mwaka mmoja uliopita ndio *brute* ambayo utaipata sasa hivi? Si kweli, sasa vitu hivi vinakaribishwa na *TBS* ipo na wanaona. Utaalam, harufu na kila kitu kina namna yake.

Mheshimiwa Spika, lakini pia lingine ambalo linaonekana sasa hivi lipo ni dawa kwa wananchi wetu, hizi dawa za hospitali. Dawa kwa ajili ya matibabu zina matatizo. Hivi sasa kuna makampuni ambayo yanaleta madhara kwa wananchi kwa kutumia dawa, hivi sasa kuna dawa kama utazifungua ndani ukategemea labda utakuta ule unga ambao unategemea kwamba ndio huo, huukuti, utakuta kuna chokaa. Huu ni ukweli na

imeshaonekana na naomba *TBS* ilifuatilie. Katika hospitali zetu mtu unakwenda na homa basi unapewa dawa huponi mwezi mmoja na nusu na umepewa hizi halafu dawa za mchanganyiko sijui dawa za nini, hapa ndiyo utajiuliza. Pia tunapokea dawa na kuziruhusu zitumike dawa ambazo zinawekwa lebo kuonesha kwamba mna dawa, lakini hamna dawa mle mna chokaa, sitaki kutaja ni kampuni gani. Lakini huo ndio ukweli na sisi tunapokea hatufanyi uchunguzi, sasa wananchi wetu wanapata madhara ambayo hatujayategemea.

Mheshimiwa Spika, nina wasiwasi hata haya mambo ambayo yanatokeatoka sasa hivi hapa nchini kwetu yanantia wasiwasi sana kuhusu hizi dawa. Unajua, samahani wale akinamama, unajua kuna wanawake wengi wana ndevu siku hizi? Sijui kama mmelipeleleza hilo, sasa kuna nini? Hivi wenzetu hawa hawatusababishii mambo haya? Sisi wanaume wengine tuna vipara vingi, vinatoka vipara bila kutegemea. Sasa naomba *TBS* tuangalie sana hasa dawa hizi ambazo tunazipokea kutoka nje. Lakini kwa kweli ni jambo lenye athari kwa Watanzania katika maisha yao.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nina mambo mawili ambayo nilikuwa nataka niombe *TBS*. *TBS* tunazungumzia taasisi mbalimbali ambazo mnazo na hizi zimezungumzwa katika taarifa mbalimbali hapa ambazo tumezipokea. Kuna Tume ya Ushindani (*FCC*), tume hii inashirikisha taasisi mbalimbali lakini kuna taasisi hapa zimezungumzwa kwa mfano hiyo Tume ya Taifa ya Ushindani, halafu Baraza la Ushindani, Wakala wa Vipimo, Tume ya Kudhibiti Chakula na Madawa na Kadhalika. Lakini hizi taasisi ambazo ninazizungumza sasa hivi suala la viwango ni la Tanzania na ninapozungumza Tanzania nazungumza sehemu zote mbili za Jamhuri ya Muungano. Mheshimiwa Waziri ukija utufahamisha, hivi *TBS* na taasisi hizi mnashirikiana vipi na Zanzibar kuhakikisha kwamba mambo haya yanakwenda sambamba ili kuwalinda wananchi wetu katika matumizi na upokeaji na katika kuwaweka wananchi katika hali nzuri?

Hizi taasisi za viwango bado hazijaunganishwa vizuri katika kuweka maslahi mazuri kwa wananchi wetu. Sasa Mheshimiwa Waziri, utakapokuja basi unisaidie ili na mie niweze kufahamu mnashirikiana vipi na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho kabisa ningepomba tu *TBS* mkashirikiane sana na Taasisi nyingine inayoshughulika na mambo ya viwango kule Zanzibar. Hii itasaidia kwa sababu Zanzibar ni kisiwa na visiwa siku zote shughuli zao ni biashara. Sasa tuwasaidie basi katika kuendesha biashara na tusitoe fursa kwa mtu mwingine kuona kwamba labda biashara ya Zanzibar inazuiliwa kuingia bara, itakuwa sio jambo sahihi. Hapa ndio ninagusa pale kwenye rushwa. Nina mfano hai, kule Zanzibar tuna Kiwanda cha Sukari, kipindi fulani kilisimama lakini sasa hivi kinafanya kazi. Viongozi wa *TBS* wataalam wake walikaribishwa katika Kiwanda cha Sukari na wakaenda wakaangalia, wakaona sukari inayotengenezwa wakaridhika, lakini cha kushangaza sukari ya Zanzibar safari moja ikasafirishwa kuja bara...

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Rished Abdallah, alikuwa nje, sasa amekuja, aliomba nafasi na muda tunao kwa hiyo nampa fursa sasa ya kuchangia Muswada huu.

MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na niombe tena radhi kwa kutoka nje kwa sababu ya dharura isiyoweza kuzuilika.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Muswada huu. Nafikiri umefika wakati kwamba nchi yetu sasa hivi isigeuke kuwa ni jalala la kutupa taka za vifaa ambavyo havikubaliki kwa matumizi ya binadamu. Huu Muswada nina hakika utaweza kurekebisha mambo mengi ambayo bado yana kasoro na nitaje maeneo machache ambayo bado nayaona yana umuhimu sana katika kuendeleza uchumi wa nchi hii na kwa kuagiza vifaa ambavyo haviko katika viwango yanaitia hasara nchi hii kwa pesa nyingi sana za kigeni.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa *spare* za magari. *Spare* za magari tunavyofahamu ambao tuna uzoefu wa shughuli hizi za magari, wale wanaotengeneza yale magari, tukichukua mfano Toyota, Kiwanda cha Toyota hakitengenezi *spare*, Kiwanda cha Toyota kinatengeneza gari wakati zile *spare* zote zinazofungwa mle ndani ya gari, wana *sub-contract* kampuni mbalimbali ambazo ndio wanaotengeneza *spare* zile ambazo ndio zinazojulikana kwamba ndio sahihi, *genuine*, kwa mujibu wa *standard* ya gari zao. Sasa ukibadilisha *spare* ambayo hailingani na matakwa ya kampuni ya Toyota na ile kampuni ya Toyota ikija ikipata malalamiko kwamba gari yako ni mbovu na ikija ikichunguza inakuta kuna *spare* iliyofungwa ambayo siyo *standard* ya kampuni ile ya Toyota ambayo inatakiwa, moja ni kwamba Serikali yetu inaingia gharama kubwa sana ya fedha za kigeni kwa kupitia kwa wafanyabiashara na kusafirisha fedha za kigeni nje ya nchi na hatimaye kuleta *spare* ambazo siyo *genuine* kama zinavyotakiwa. Sasa hatuwezi tukasema kwamba *spare* zinazouzwa madukani ni *genuine*. Kwa usemi huo ni kwamba *spare* zote haziwi *genuine* isipokuwa ziwe zimeagizwa kutokana na lile shirika au kampuni ambayo inaitengenezea Toyota *spare* zile na hizo ndio zitajulikana kwamba ni *genuine*. Lakini kuna kampuni nyingine zinazotengeneza *spare* zinazofanana na ile kampuni inayotengenezea Toyota, sasa hizo hatuwezi tukaziita ni *genuine spares*.

Mheshimiwa Spika, hivi Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha na kufahamu kwamba ni kampuni gani zinazwatengeneza *spare* za magari ya kampuni ya Toyota, kampuni ya Nissan au gari za Kiingereza au gari za Kifaransa na za Kijerumani na nchi ikawa inajua kwa uhakika kwamba kampuni fulani kwa gari fulani ndio zitakazojulikana kwamba ni *genuine spares* au *spare* halisi? Hilo naliomba Serikali ilifanye utafiti na kuhakikisha kwamba *spare* zinazokuja nchini zinakuwa ni *genuine*. Kwanza tuta-save pesa za kigeni za nchi hii. Pili, tutakuwa tunanusuru maisha ya binadamu kwa kupata ajali ambazo zinatokana na kufunga vipuri ambavyo sio sahihi au siyo *genuine*.

Mheshimiwa Spika, hilo moja, lakini vilevile kuna kampuni hizi zinazotengenezwa magari huwa wana *sub-contract* nchi nyingine kutengeneza magari yao lakini juu ya *supervision* ya kwao wenyewe. Inawezekana gari ya Toyota ikawa ni

made in Japan, lakini ikawa *manufactured* kama Kenya, lakini tunafahamu kwamba kile kiwanda kinachotengeneza au kinacho *assemble* magari ya Toyota pale Kenya, *spare* zote au vifaa vyote kwa ajili ya ku-*assemble* magari yale pale Kenya zinatoka Japan. Sasa hiyo pia tufuatilie kwa karibu ili tusipoteze maisha ya wananchi wetu na kuweza kudhibiti fedha za kigeni ambazo zinatoka hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la madawa. Suala la madawa kwa kweli hili ni tatizo kubwa sana pamoja na juhudi za Serikali za kuhakikisha kwamba wanafanya ukaguzi katika maduka ya madawa katika maeneo mbalimbali ambayo wana-*supply* madawa kwa wingi, kuhakikisha kwamba hizi dawa kweli ni *genuine*. Sitaki kutaja majina ya nchi, lakini niseme tu kuna madawa yanayotoka nchi fulani ambayo ndiyo wenyewe wanayotengeneza madawa hayo halisi lakini dawa hizo hizo zinatengenezwa na nchi nyingine. Utakuta zile dawa zinafanana, hazina matatizo yoyote kwa rangi kwa ukubwa kwa kila kitu, hata *assembling* ile namna ya kufunga katika vifurushi vyake vinafanana, lakini wakati wa matumizi ya dawa zile ndio utaona kuna tofauti. Ukichukua dawa zinazotengenezwa na ile kampuni halisi, labda dozi moja utakuwa umepona ugonjwa ule, lakini ukikinunua dawa zile zile zinazotengenezwa kutoka nchi nyingine zinaweza kukuchukua mwezi bado hujapona. Sasa hapo ndio tunapoingia mashaka. Sasa Serikali sijui inachukua utaratibu gani wa kudhibiti hii hali kwa sababu siku hizi huu utaratibu wa biashara huria unatupa tabu sana.

Mheshimiwa Spika, hivi kweli Serikali haiwezi ikaweka utaratibu kwamba madawa yote yanajulikana kwamba aidha yatapita kwa njia ya usafirishaji wa ndege au kwa njia ya usafirishaji wa Bandari au kwa njia ya barabara, inategemea dawa hizi zinatoka wapi. Sasa hapo ni kuweka wataalam wa kutosha kabisa kuhakikisha kwamba hizi dawa zinazopita hata kama itakuwa ni usumbufu wa kukagua mizigo ile lakini tuwe na uhakika kwamba madawa yanayoingia nchini ni halisi, hatuingiziwi madawa ambayo siyo halisi kwa sababu yanaleta madhara kwa wananchi wetu na vile vile kwa upotevu wa pesa za kigeni.

Mheshimiwa Spika, nataka nifahamu, hapa naona sasa panakuwa na muingiliano kati ya *TBS* na *TFDA*, hivi ni nani ambaye anatakiwa akague nini? Ninavyofahamu *TFDA* wanakagua madawa kujua kwamba haya madawa yanayokuja nchini ni sawa sawa, lakini utakuta na *TBS* na wao wanafanya kazi hiyo hiyo. Utakuta *TBS* wanazunguka madukani wanatazama vipodozi, wanatazama sijui madawa mengine mbalimbali. Sasa nina wasiwasi muingiliano huu wa hizi taasisi mbili katika kukagua kitu kimoja inaweza kuwa pengine wao wenyewe wataelewana lakini watatupa tabu sisi wananchi na hasa wale wafanyabiashara ambao wanakaguliwa na taasisi mbili kwa kitu moja. Hii kwa kweli itatupa tabu.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba Kamati ya Huduma za Jamii iliagiza uongozi wa Viwanda na Biashara wakae kwa pamoja walitatie hili tatizo, sasa sijui kama walifanya hivyo? Hapa bado napata tabu ya muingiliano wa *TFDA* na *TBS* katika masuala ya madawa, sasa basi sheria iwe wazi ambayo inaonesha kwamba *TFDA* watakagua nini na *TBS* watakagua nini. Naona *TBS* wakague zaidi vifaa vinavyotoka viwandani, pamoja kwamba na madawa yanatoka viwandani lakini inajulikana kwamba

vifaa ambavyo sio vya madawa na madawa basi wapewe kazi hiyo *TFDA* ili wafanye kazi yao, ama sivyo hakuna sababu basi ya kuwa na vyombo hivi viwili vinavyofanya kazi moja ya ukaguzi na hatimaye bila kuwekeana mipaka ya kuchanganua kwamba ninyi mtakagua hiki na ninyi mtakagua hiki. Hili ninaliona ni la msingi na lisije likawapa tabu wafanyabiashara na wale wengine ambao inabidi wapite katika utaratibu wa ukaguzi na hatimaye wakasumbuliwa kwamba wakifika *TBS* wataambiwa hiki na wakifika *TFDA* wataambiwa lile lile, watasema kwamba *TBS* tumeshaambiwa hili tumetekeleza na wao watasema aah na sisi utekeleze kwa mujibu wa sheria zetu. Hili Mheshimiwa Waziri, naomba sana utuondoe wasiwasi ili tuweze kuweka hili jambo wazi ili liweze kujulikana.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kwamba sasa hivi kuna utaratibu wa kuleta matrekta nchini kutoka nje na bei zinatofautiana. Lakini trekta ni chombo ambacho kinafanya uzalishaji mkubwa kwa ajili ya kuinua uchumi wa nchi hii. Tunapoleta trekta likakaa shamba miaka mitatu likaanza kuharibika na tunafahamu kuna matrekta ukinunua linakaa miaka 10 bado linadunda, linafanya kazi ile ile, hili lingne kwa kweli litakuwa linaleta athari kwa uchumi wa nchi. Kwa hiyo, ni vema basi Serikali ikaweka viwango vya aina ya trekta kwa nchi zote ambazo zinaleta nchini, sisi tumezoea hapa matrekta ya *Ford* kutoka Uingereza, *Massey Ferguson* pamoja na matrekta ambayo yanajulikana kabisa yako mengi, tuna matrekta ya *Fiat* hapa yanajulikana tumeyazoea, lakini siku hizi kuna matrekta mengi yanakuja kutoka China. Sikatai yasitoke China kuja huku.

Mheshimiwa Spika, ukienda China leo, yeye Mchina anakuuliza unataka trekta ya *standard* gani? Atakwambia kabisa kuna *fake*, kuna *semi-fake* na kuna *genuine*, unataka lipi? Sasa wafanyabiashara ni bora tuwaambie kwamba Tanzania inahitaji matrekta ya aina hii, kama ni kutoka China basi ni aina fulani ya matrekta na Serikali iwasiliane kabisa na Serikali ya Uchina kupitia utaratibu wake kwamba sisi Tanzania tunahitaji yaagizwe matrekta ya kampuni mbalimbali lakini yawe katika *standard* fulani. Hivi tutakwenda vizuri kuliko kuwaachia wafanyabiashara walete matrekta ya aina mbalimbali kwa sababu tu ni rahisi na wananchi wetu hawaelewi mambo kama haya, matokeo yake wanakuja kuingia katika hasara moja kubwa wakitegemea kwamba trekta litachukua miaka mitano kumbe linachukua miaka miwili au mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, hili ni vema tukaliangalia na Wizara ya Kilimo vilevile isaidie kutoa mawazo na kushirikiana vizuri na Wizara ya Viwanda na Biashara hatimaye tuweze kupata matrekta mazuri ambayo yatadumu kwa muda mrefu na hatimaye wakulima wetu waweze kunufaika katika kuendeleza nchi yetu na kuinua uchumi wa Tifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja na ninasema ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia hautuwezeshi kupata kutoka kwa mtoa hoja majumuisho na majibu kuhusu hoja mbalimbali na wakati huo huo tena tukaingie kwenye Kamati ya Bunge Zima ili kuipitia Muswada kifungu kwa kifungu. Katika mazingira haya kanuni zetu, kanuni ya 28 ibara ndogo ya 2 inasema: “Bunge litakutana hadi saa 07.00 mchana ambapo Spika ataahirisha shughuli yoyote itakayokuwa

inafanyika hadi saa 11.00 jioni, isipokuwa kama Spika akiona inafaa Bunge linaweza kuendelea kukutana kwa muda usiozidi...” lakini hiyo sio, ni ile, “...au kusitishwa wakati wowote kabla ya saa 07.00 mchana baada ya kuwahoji Wabunge.” Sasa kinachofuata pale kinasema, “Hoja ya kubadilisha nyakati za vikao itatolewa na Waziri.” Kwa kuzingatia kanuni hii katika sehemu zake hizo mbili, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi sasa atoe hoja ya kusitisha shughuli za Bunge kabla ya muda wake.

HOJA YA KUSITISHA SHUGHULI ZA BUNGE KABLA YA MUDA WAKE

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, ili kumpa nafasi Mheshimiwa Waziri kuandaa majibu kwa ajili ya hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lisitisha shughuli zake kwa mujibu wa Kanuni ya 28(3) hadi saa 11.00 jioni.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Kusitisha Shughuli za Bunge kabla
ya muda wake iliridhiwa na Bunge)*

(Saa 06.22 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, naupongeze Muswada huu mzuri na muhimu sana.

Sehemu ya kwanza kwenye tafsiri ya *Local Government Authority*, iongezwe mwaka wa Act na Namba ya Act; No. 6 and 7 of 1982.

Mheshimiwa Spika, ili lengo la kuwalinda walaji na watumiaji wa bidhaa nchini litimie, ipo haja sana ya kuwa na *inspectors* (wakaguzi) wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, katika kila Halmashauri ya Wilaya nchini, tunao Maafisa Biashara wa Wilaya, ambao wangetumika kucheki viwango vya bidhaa na *standard*.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Dar es Salaam zoezi linaenda vyema lakini, mikoani inabidi tuongeze juhudi. Vifaa vya umeme vingi ni kama *disposable* sio vya kudumu.

Ofisi za TBS nchini zipo Dar es Salaam tu, ningeshauri wawe na Ofisi Mikoani au washirikiane na Wizara ya Viwanda na Biashara. Maafisa wapewe elimu waweze kutumika.

Mheshimiwa Spika, katika *section 5 page 9*, Muswada umeeleza kuwa kutakuwa na Bodi. Majukumu ya Bodi yapo *section 6 page 9*, yaani *Management and Control of the Bureau*.

Mheshimiwa Spika, *section 20(3), page 15*, inaongeza majukumu ya Bodi, yaani kusikiliza *objection*. Jukumu hili linapingana na jukumu la *section 6 page 9*, yaani *Management and Control*, kwani hapa Bodi inakuwa imeingia katika *Operations* za *Bureau* na kwa mfano ikikosea jambo lolote (*Bureau*), Bodi itashindwa ku-control, kwani Bodi itakuwa imeshiriki katika kazi za kila siku.

Mheshimiwa Spika, aidha, kutokana na Wajumbe wa Bodi, rejea *section 2*, kwenye *schedule, Composition of the Board*, sioni uwezekano wa Wajumbe tajwa kuwepo kila siku kusikiliza *objection* na kuzifanyia kazi haraka na mapema, kwani Wajumbe wengi wanaingia kwa mujibu wa nafasi zao na ni Wajumbe wa Bodi, ambao wana kazi zao maalum.

Nashauri jukumu hili lisiwepo kwenye Bodi, liwepo ndani ya TBS yenyewe na endapo mtu aliyepeleka pingamizi hajaridhika na *objection*, anaweza aka-*appeal* kwa Waziri au akalalamika akakata rufaa katika Mahakama Kuu, Kitengo cha Biashara (*Commercial Division of High Court*); ingawa kuwa angalizo la viwango au *pecuniary jurisdiction* kwenye *High Court Commercial Division*.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kuwa ushauri wangu utazingatiwa.

Naomba kuunga mkono Muswada huu.

MHE. JANETH M. MASSABURI: Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa juhudi kubwa wanayofanya na pia kwa kuandaa Muswada huu muhimu sana, unaolenga kuboresha huduma kwa jamii na tija kwa Taifa.

Kwa kuzingatia yote yaliyomo katika Mswada, nina maoni yafuatayo:-

1. Kuzingatia viwango vya vifungashio (*International Standard*)

Wizara ihakikishe kunakuwa na viwanda vya kutengenezea vifungashio vyenye hadhi ya Kimataifa (*International Standard*).

Kwa kufanya hivyo kutasaidia kuinua kilimo, ufugaji na viwanda vidogo vidogo na vya kati, kwa lengo la kuwasaidia wananchi wazalishe mazao kwa tija.

Kuhakikisha soko la ndani limelindwa kwa bidhaa kama maziwa, juisi, kahawa, chai, nyama, mboga mboga na kadhalika.

Wizara itafute wawekezaji wa nje kuja kuanzisha viwanda vya aina hiyo ya vifungashio (*packaging*) au waingie ubia na viwanda vya humu nchini.

2. Bidhaa *fake*

Wafanyabiashara wa Tanzania kwa asilimia kubwa ndio wanaoingiza bidhaa *fake* hapa nchini, wao ndio wanaotoa *order* na *specifications* za bidhaa wanazohitaji huko nje. Kwa sababu hiyo, taasisi husika kwa kushirikiana na *TRA* na *TBS* zitafute suluhu la tatizo la bidhaa *fake* kuingizwa hapa nchini.

Watendaji wasikae maofisini waende mitaani kukagua bidhaa, hiyo itasaidia watu wasio waaminifu kuogopa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawapongeza tena na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA: Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara, kwa kuleta Muswada huu wa Sheria ya Viwango wakati huu muafaka, ukizingatia sera ya soko huria na utandawazi. Kutokana na hali hii, bidhaa nyingi na hasa za kutoka nchi za Mashariki ya mbali kama vile China, Indonesia, Malaysia na kadhalika, zimekuwa zinaingizwa hapa nchini zikiwa katika viwango vya chini. Hata hivyo, naipongeza Wizara kwa hatua mbalimbali ambayo imekuwa ikichukua ili kuthibiti hali hii.

Taasisi mbalimbali zinafanya kazi ya kuthibiti ubora wa bidhaa zinazolingizwa au kuzalishwa nchini, lakini mafanikio ya juhudi hizi hayajawa mazuri sana. Ushauri wangu ni kwamba, taasisi ziwe chini ya uratibu wa taasisi moja ili kuimarisha uthibiti wa ubora wa bidhaa ili kuwalinda walaji.

Aidha, Wizara zinazohusika na viwango vya bidhaa mbalimbali, zitazame uwezekano wa kuhuisha sheria husika. Vilevile utazamwe uwezekano wa kuwa na Ofisi za Kanda za *TBS*.

MHE. FUYA G. KIMBITA: Nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote, waliohusika kwa njia moja au nyingine katika kuuandaa huu Muswada, ambao kwa maoni yangu ni mzuri sana na mkombozi wa nchi yetu, licha ya kuchelewa. Hongereni sana na Mungu awabariki sana. Kipekee, umuhimu wa huu Muswada kwangi ni kule kuiepusha nchi yetu kuwa jalala la bidhaa mbovu, ikiwa ni pamoja na madhara yake kwa ujumla.

Ninashauri mpaka katika taasisi zetu za kudhibiti viwango mbalimbali, ieleweke vizuri ili kuepusha migongano na mianya kwa wachache kutumia migongano hiyo kwa faida zao binafsi.

Ninaunga mkono pendekezo la *TBS* kuwa *umbrella* ya taasisi zote za kudhibiti viwango, ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa sheria na viwango vya *TBS* kutumika katika pande zote za Muungano ili kuepusha manung'uniko kutoka upande wa pili wa Muungano.

Nilichokuwa ninakishauri na kukililia siku nyingi, ninashukuru sasa kimo katika Muswada huu; nacho ni kuipa *TBS* meno kwani kazi yao imekuwa nzuri, lakini walikuwa wanakosa uwezo wa kisheria wa kuwachukulia hatua wakosaji. Ninapongeza kwa hili na kuomba sheria hii ikafanye kazi vizuri kama tunavyokusudia.

TBS kuna vifaa vya thamani sana, pamoja na kazi nyeti zinazofanyika pale, ninashauri umuhimu wa ulinzi nikianza na *fence* (uzio wa ukuta ambao unahitaji kuimarishwa).

MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi husika, Wataalamu na Wafanyakazi wa Wizara, kwa kuleta Muswada huu ambao utamlinda mlaji dhidi ya bidhaa *fake*.

Katika dunia ya ushindi na utandawazi, Tanzania kama sehemu ya dunia, hatuna budi sisi Wananchi wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali yetu, tuhakikishe kuwa bidhaa hafifu zinazolingia nchini ni salama. Kwa mantiki hiyo, naunga mkono Muswada na nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake, kwa kuandaa Muswada huu kwa wakati wake.

Napenda kuichangia kwa kutoa ushauri/mapendekezo kwa lengo la kusisitiza yafuatayo:

Sehemu II ya Muswada: Napendekeza/nashauri katika kufanya ukaguzi wa ubora wa bidhaa zinazolingia nchini na zinazotengenezwa hapa nchini; ni vyema maabara ya kisasa ijengwe katika kila mkoa na ikiwezekana wataalamu wa *TBS* waajiriwe kwa kila mkoa, hususan mikoa ya pembezoni kama Mara.

Viwanda vidogo vilivyopo mikoani vinatoa michango mikubwa kwa kuzalisha bidhaa kwa bei nafuu. Nashauri Wizara/*TBS* zitoe kipaumbele kusaidia wenye viwanda hivi kuhusu mafunzo, wataalam, mashine na uhifadhi wa mazingira ili wananchi wengi waweze kupata ajira na kulinda afya za wananchi.

Narudia tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake.

MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS: Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Viwango huu ni mzuri na utasaidia Watanzania. Ninawapongeza Mawaziri wa Wizara hii, kuanzia Mheshimiwa Waziri Dkt. Mary Nagu (Mb) na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami (Mb), kwa kazi nzuri na kwa kusharikiana na Watendaji wa Wizara yao.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ukipita, itolewe elimu kupitia ngazi mbalimbali kuanzia Wizara yenyewe, sekta za biashara zote ndani na nje hadi wananchi wenyewe na wafanyabiashara na wadau wengine.

Mheshimiwa Spika, Wizara ipewe uwezo mzuri kwa hali zote ili iweze kukidhi haja ya kuisimamia nchi yetu na tuwe na *standard* tuondokane na uhafifu wa viwango wa bidhaa za nchini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali chini ya Wizara iwe na usimamizi mzuri na tahadhari kuepuka madhara na mambo yasio mazuri kwa faida ya Taifa letu yanayosababishwa na bidhaa zinazoingizwa ndani ya nchi yetu za aina zote, hasa zinazoliwa au zinazotumika, ulaji wa dawa na kadhalika.

Kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Magogoni, naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara.

Sheria hii ni muhimu sana, hasa kwa viwango vya matumizi ya vitu mbalimbali.

Sehemu ya nne ya Muswada kuhusu utendaji wa Shirika la Viwango, hasa pale Watendaji wanapofanya *testing* (jaribio), juu ya bidhaa katika kuthibitisha ubora wake kwa watumiaji, Sheria ingebainisha wazi iwe wakati wowote pale inapoendelea kutengenezwa viwandani au hata inapokuwa sokoni tayari kwa matumizi ya mlaji.

Kadhalika, sampuli iliyothibitishwa katika hatua za awali, isiwe ya hatua ya mwisho katika kutoa cheti kwa bidhaa husika, kwani upo uwezekano mkubwa kwa wakorofi kutumia *certificate* hiyo na baadaye kuendelea na utengenezaji wa bidhaa hafifu na hivyo kumfanya mlaji aamini viwango vilivyotumika ni sahihi.

Muswada pia haujaeleza namna ya mtiririko wa utendaji wa *TBS*; ni vyema basi ngazi kama mkoa na wilaya kuwa na wawakilishi, kwani maeneo hayo ndiyo yenye walaji wengi na uwezekano wa kupenyeza bidhaa feki na udhibiti wake ni mdogo.

Muswada pia uangalie juu ya suala la matumizi ya mizani, udhibiti wake na namna ya matumizi yake, kwani viwango vingi vya mizani vina tofauti kubwa sana; unaweza kuwa na kilo moja basi ukifanya majaribio katika mizani zaidi ya mbili, utagundua tofauti kubwa.

TBS na VAT vifanya kazi kwa ukaribu ili kuepuka uingizaji wa bidhaa fake, kwani wingi wa bidhaa ziingiazo nchini ni zile ambazo sio genuine (sio halisi). Kitendo cha uingizaji bidhaa za aina hii kumeathiri sana nchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DR. ALI TARAB ALI: Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu kumekuwa na mkanganyiko kati ya majukumu ya *Tanzania Bureau of Standard (TBS)* na *Tanzania Food and Drug Authority (TFDA)*. Jambo hili pia linaleta usumbufu mkubwa kwa wafanyabiashara wanaoleta mali zao nchini na pia wale wanaozalisha ndani ya nchi.

Muswada huu utakuwa na maana tu ya kuondoa mkanganyiko huu, ikiwa TBS itabaki na jukumu la kuweka viwango tu, lakini udhibiti wa chakula, dawa na vipodozi, ubakie mikononi mwa *TFDA*.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 20 cha Muswada, kinatoa mamlaka kutangaza viwango vya lazima ingawa kifugu hiki hakisemi ni sababu gani ya kisheria, itaweza kusababisha nchi kutangaza viwango vya lazima. Sababu hizi zikijulikana mapema ni mambo gani ya msingi kisheria yanayopelekea nchi kutangaza viwango hivyo vya lazima, wadau wote wataelewa mapema.

Mheshimiwa Spika, vifungu 23 na 24, vinatoa mamlaka ya kuwepo wakaguzi ambao watakuwa na jukumu la kukagua viwango vya lazima vya bidhaa yoyote. Hapa ni lazima iainishwe bayana, majukumu na mipaka ya *TBS* na *TFDA*. Hii ni vyema ikafanyika, kuondoa ule mkanganyiko au mwingiliano wa kazi baina ya *TBS* na *TFDA* katika ukaguzi wa chakula, dawa na vipodozi.

Mheshimiwa Spika, ingekuwa ni vyema malengo au misingi ya kutangazwa viwango vya lazima iwe sawa na ile ya Sheria ya Viwango ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2007, kifungu cha 19.

MHE. MSOLWA C. MSOLWA: Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni msingi kwa uchumi wa Taifa letu, ukitekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa na taasisi za udhibiti viwango vya ubora wa bidhaa hapa nchini, inaonekana kuna upungufu wa utaalumu kwa wataalamu wetu wa kubaini kwa baadhi ya bidhaa (ubora wake), hasa zinazolingia hapa nchini, kutokana na kukua kwa teknolojia na kutokana na viwanda husika hapa nchini, ambavyo wataalamu wetu ingekuwa ni rahisi kwao kujifunza kwa vitendo na kuainisha ubora wa bidhaa.

Mheshimiwa Spika, bidhaa feki zinachangia kwa kiwango kikubwa, umaskini kwa Watanzania na nchi yetu kwa ujumla. Bidhaa kama pikipiki zinazolingizwa hapa Tanzania kutoka nchi za Asia (hasa China), hazina viwango vya ubora. Kwa kuwa huuzwa kwa bei ya chini, Watanzania wengi wamekuwa wakizinunua kwa wingi, lakini baada ya miezi michache tu pikipiki hizo hupoteza ubora wake na kuwa scraper. Sasa kama kweli wataalamu wetu wanaodhibiti uingizaji wa bidhaa hiyo feki, wanao utaalumu

wa kubaini kipi ni bora na kipi ni feki, mbona bidhaa hiyo ya pikipiki inazidi kuzagaa nchini?

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe elimu kwa wananchi kuhusu suala la bidhaa yenye viwango hafifu na madhara yake na iendelee kuviangamiza viingiapo nchini lakini pia zoezi la kuvikamata kwenye maduka kwa ambavyo vimepenya kupitia njia za panya, nazo ziangamizwe. Kama hakuna kipengele cha sheria cha kukamata bidhaa feki vinavyouzwa madukani ni vyema kikawepo.

Mheshimiwa Spika, wataalamu wetu ni lazima waendane na teknolojia ya sasa, kwani kuna ujanja mwingi unaofanywa na watengenezaji wa bidhaa mbalimbali kwa udanganyifu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, orodha ya wachangiaji kwa Muswada huu imekwishakamilika na kwa hiyo lililobaki sasa ni kumwita mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, kwa mpangilio kwamba, ataanza Mheshimiwa Naibu Waziri kama walivyojipangia isizidi nusu saa, halafu Mheshimiwa Waziri kwa muda usiozidi dakika 45.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, naomba kuungana na walionitangulia kusema, kwa kutoa pole nyingi kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge wengine wote, ambao kwa njia moja au nyingine, wamepata misiba ya kuondokewa na wapendwa wao.

Napenda pia kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Moshi Vijijini, kwanza, kutoa pole kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Marehemu Nyaulawa. Pili, natoa pongezi kwa Wananchi wa Mbeya Vijijini, kwa kumpata Mbunge mpya, anayetokana na chama kile kile alichokuwa Marehemu Nyaulawa, yaani CCM. (*Makofi*)

Napenda pia kuungana na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara, kwa kufanya kazi kwa karibu sana na Wizara yetu katika mambo mengi, ikiwa ni pamoja na kuufanya Muswada huu ufikie hatua hii. Hakika Wajumbe wa Kamati hii wamechambua, wameshauri na wamekosoa pale ambapo wameona kasoro. Katika haya yote, jambo la msingi waliloliweka mbele ni kuhakikisha kuwa, maslahi ya Taifa yanazingatiwa katika Muswada huu, ninawashukuru sana.

Napenda pia kumpongeza Msemaji wa Kambi ya Upinzani na Wajumbe wa Kamati kutoka Kambi hiyo, kwa jinsi walivyotoa ushirikiano katika kuujadili Muswada huu hadi hapa ulipofikia. Baada ya maneno hayo ya awali, naomba nami kuchangia Muswada huu kwa kujibu hoja moja moja za Waheshimiwa Wabunge, nikimwacha Mheshimiwa Waziri wangu ajibu hoja za jumla.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ilikuwa kwamba, Ofisi za TBS zipo Dar es Salaam tu na kwamba, kuna umuhimu ofisi hizi ziwe katika mikoa mbalimbali ya nchi yetu. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Mbunge wa Kilolo kwa tiketi ya CCM. Jibu hapa ni kwamba, lengo hilo lipo na tunapenda kuwahakikishia kwamba, udhibiti wa viwango utapelekwa hadi kwa wananchi vijijini na hata kwa wajasiriamali wadogo wadogo; ndiyo maana tumeona katika Muswada huu tuwahusishe wenye viwanda vidogo vidogo ili wawakilishe katika bodi hii, kuhakikisha maslahi yao yanazingatiwa. Vile vile niseme tu kwamba, pale TBS kwa kuona kwamba sio rahisi kuwa na ofisi kila mkoa, uharaka tunaopenda wamekuwa na gari ambalo ni maabara inayotembea, ambayo inaweza ikafika katika mkoa wowote ule kuhakiki ubora wa bidhaa pale.

Tunapojitahidi kujenga ofisi, tuna hakika gari hili litasaidia kupunguza matatizo katika mikoa ile ambayo imekaa mbali sana na Dar es Salaam.

Hoja ya pili nayo imetolewa na Mheshimiwa Pindi Chana, amesema kwamba, kuipa bodi kazi ya kusikiliza *objection* ni kuipa mzungu mkubwa kwa sababu bodi hii ina watu ambao wanafanya kazi nyingine na akashauri kwamba ni afadhali kazi hii ya *objection* isikilizwe na *bureau* yenyewe badala ya kuipa bodi.

Mheshimiwa Spika, jibu hapa ni kwamba, kwa kuwa anayelalamikiwa hapa atakuwa ndiyo *bureau* yenyewe, itakuwa sio Utawala Bora kuiambia tena *bureau* yenyewe isikilize *objections*. Niseme tu kwamba si mambo mengi ambayo yanapita pale kwenye *bureau* halafu mdau anaacha kutosheka mpaka anataka iende mbele yale, machache ambayo *bureau* anaona kwamba hawakuelewana na yule mdau ndiyo yanapelekwa kwenye bodi ili bodi iweze kukaaa.

Mheshimiwa Spika, tumeweka tena utaratibu kwamba, endapo mdau hata kubaliana na bodi, uwepo utaratibu wa kukata rufaa kwa Mheshimiwa Waziri na baada ya miezi mitatu au ndani ya kipindi cha miezi mitatu, baada ya Mheshimiwa Waziri kujibu ile rufaa, kama yule hajaridhika, bado anaweza kukata rufaa tena kwenye Mahakama Kuu, Kitengo cha Biashara. Yote hii ni kumpa mdau nafasi pana ya kuweza kuona kwamba, anatendewa haki.

Hoja nyingine ni hoja ya TBS, pamoja na Viwanda vya Biashara na Masoko, kutoa elimu kwa wadau, ikiwa ni pamoja na kuwafunza Maafisa Biashara ili Maafisa hao waweze kusaidia katika kueneza elimu ya TBS, yaani ya viwango katika mikoa.

Mheshimiwa Spika, waliochangia hapa ni Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mheshimiwa Vuai Abdallah Hamis na Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa.

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru Wabunge wote hawa na tunasema, tumepokea ushauri huu, unafanyiwa kazi na utaendelea kufanyiwa kazi zaidi kadiri siku zinavyosonga. Hoja nyingine ilikuwa ni tafsiri hii ambayo Mheshimiwa Pindi Chana

ameisema ya *Local Government Authority*, pale tulikuwa tumesahau namba ya sheria na mwaka; akashauri kwamba ni vyema tuvitamke. Tunatambua Mheshimiwa Chana ni Mwanasheria aliyebobea na tunakiri kulisahau hilo, ushauri wake tunaupokea na tutaufanyia kazi.

Hoja nyingine ni utaratibu wa uteuzi wa Mtendaji Mkuu wa TBS kuteuliwa na Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Owenya alikuwa amependekeza kwamba ni vyema huyu mtu akateuliwa na Bodi, badala ya kuteuliwa na Rais. Uteuzi wa Mtendaji Mkuu wa TBS ni wa wazi, kama Mheshimiwa Owenya alivyopendekeza na wa ushindani kama ulivyofanyika kumpata Mtendaji Mkuu aliyepo hivi sasa. Utaratibu unaotumika, unaruhusu ushindani kwa kutangaza nafasi katika vyombo vya habari na baada ya mchujo, ikiwa ni pamoja na *interview* anayosema, majina matatu hupatikana. Majina hayo yakishapatikana, Mheshimiwa Waziri anayehusika na suala hili, huyawasilisha kwa Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Rais huwa anafanya uteuzi.

Hoja nyingine ni vigezo vya uanzishaji wa Idara ya Kurugenzi ya TBS. Mheshimiwa Owenya vile vile alisema kwamba, vigezo gani vinatumika mtu anaposema tuunde Idara fulani, tuunde Kurugenzi fulani ndani ya TBS ili kuondoa mwanya wa watu kujipangia tu idadi ya Idara au Kurugenzi bila kuzingatia hali halisi.

Mheshimiwa Spika, vigezo vya kuanzisha Idara na Kurugenzi, kwanza ni muundo wa majukumu ya shirika, shirika lilivyokaa ndiyo linatufanya hapa tulipe Kurugenzi kadhaa, Idara ziwe kadhaa na kadhalika.

Pili, tathmini zinazofanyika mara kwa mara ndani ya nchi na kwa kuzingatia hata muundo wa mashirika mengine, kwa ajili ya kuleta ufanisi. Tathmini hizi zinafanyika sio na mtu mmoja au na taasisi moja, bali zinafanywa na wadau walio wengi kuhakikisha kwamba, maoni ya wengi yanazingatiwa.

Tatu ni ushauri na maoni ya wadau mbalimbali waliopo ndani na waliopo nje ya nchi. Narudia tena kusema kwamba, lengo hapa ni kuhakikisha taasisi yetu inakuwa na ufanisi na tija, pale Wizarani hatutakubali Kurugenzi iundwe ambayo haina kazi kwa ajili tu ya kutumia fedha za Taifa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo imechangiwa sana na Waheshimiwa Wabunge ni kuondoa mwingiliano wa majukumu kati ya TBS na Taasisi nyingine za udhibiti kama vile TFDA, WMA na EWURA. Mheshimiwa Waziri wangu, atalisemea sana lakini itoshe tu hapa kusema kwamba, waliochangia ni Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Mheshimiwa Dkt. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Omar Kwang' na Mheshimiwa Fuya Kimbita Mbunge wa Hai.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ambayo atayasema Waziri wangu ni kwamba, TBS ni Msimamizi na Mpangaji Mkuu wa Viwango vya sekta zote za uchumi. Hata hivyo, inatambua uwepo wa mashirika na taasisi nyingine za udhibiti. Jibu la tatizo la mwingiliano wa majukumu ni kutambua uwepo wa taasisi hizi nyingine na kuhakikisha kuwepo kwa ushirikiano wakati wa utekelezaji na utendaji kazi wa taasisi hizi. Ni kwa

mantiki hii, ndiyo maana Muswada huu wa Viwango, umesisitiza ushirikiano huo kupitia kifungu cha 4(2)(j) na kifungu kidogo cha 2(b). Kwa vile hili ni suala la kiutendaji, tatizo hili litatatuwa wakati wa kuandaa kanuni.

Hoja nyingine ambayo ameitoa Mheshimiwa Lucy Owenya na Mheshimiwa Susan Lyimo, inahusu kifungu na 23(1), ambacho kinahusu uteuzi wa Wakaguzi kwamba, maneno *public officer* yatolewe ufafanuzi au tafsiri. Kipengele hiki kimewekwa kwa lengo la kuwezesha ukaguzi kufanyika, kwa kuwatumia watumishi wa serikali, lakini wale wenye sifa husika. Ipo hoja nyingine ambayo imetolewa na Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, ambaye ameuliza; je, tutakapoingia katika mashirikiano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, sheria hii itaendelea kutumika au itatungwa nyingine? Jibu ni kwamba, makubaliano yaliyopo kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kuwa, kila nchi itakuwa na sheria yake ya viwango, isipokuwa kutakuwa na *harmonization*, yaani namna fulani ya kuainisha viwango hivyo ili kuhakikisha kwamba, hakuna tofauti kubwa kati ya nchi na nchi.

Hoja nyingine ni je, tutakuwa tayari kutuma wakaguzi wa bidhaa kabla ya bidhaa kuingizwa nchini? Je, COTECNA tumewalipa kiasi gani na wamefanya kazi gani? Litafutwe suluhisho la bidhaa feki, yote haya yamesemwa na Waheshimiwa Wabunge watano; Mheshimiwa Vuai Abdallah Hamisi, Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi na Mheshimiwa Dkt. Mzeru Nibuka.

Mheshimiwa Spika, TBS inakamilisha utaratibu wa ukaguzi wa ubora wa bidhaa katika nchi zinakotoka kabla ya kuingizwa nchini. Hii inaitwa *pre-shipment verification of conformity to standards*. Kuhusu COTECNA, COTECNA hulipwa 0.8% ya *FoB value* ya bidhaa ambazo tunaingiza kutoka nje. Kwa hivi sasa COTECNA wanajihusisha na kuthibitisha thamani na bei ya bidhaa zinazolingizwa nchini, hawahusiki na masuala ya ubora. Waheshimiwa Wabunge, ni vyema tukafahamu mgawanyo huo wa kazi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni vigezo vya viwango vya lazima vitolewe, suala la vigezo vya viwango vya lazima vitolewe katika muswada hili limesemwa na Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Omary Kwaangw'. Jibu hapa, suala hili ni la kiutendaji zaidi na hivyo litaingizwa kwenye kanuni.

Lipo suala la kuangalia uwezekano wa sheria kutumika pande zote za Muungano, ambalo limesemwa na Mheshimiwa Fuya Kimbita, limesemwa vile vile na Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir.

Mheshimiwa Spika, suala hili litapelekwa kwenye Tume inayoshughulikia masuala ya Muungano; Tume ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi, chini ya Mwenyekiti wake Makamu wa Rais.

Hoja nyingine ilikuwa ni maabara za kisasa zijengwe kila Mkoa, hilo ni mwendelezo tu wa ile kwamba, maabara ziwe kila Mkoa. Hapa wanasisitiza maabara iwe ya kisasa na Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi ndiyo ametoa hilo wazo; ni

kwamba, Serikali itaendelea kuimarisha maabara zilizopo na kujenga maabara za kisasa, kulingana na upatikanaji wa rasilimali.

Hoja nyingine inasema, TBS wafuatilie ubora wa bidhaa zote zilizothibitishwa na haya ni maoni ya Mheshimiwa Juma Hassan Kilimba. Jibu hapa ni kwamba, Sheria imezingatia ufualitaji wa ubora. Kipengele kingine ambacho kimesemwa ni Muswada uangalie namna ya kuthibiti usahihi wa vipimo vya mizani. Mheshimiwa Juma Hassan Killimba, ameshauri tena hivyo na ni kwamba, Sheria imezingatia suala la usahihi wa vipimo vya mizani.

Mwisho kabisa, Mheshimiwa Janeth Massaburi ameshauri kwamba, Sheria ihakikishe kwamba kunakuwa na viwango vya kutengeneza vifungashio vyenye hadhi ya kimataifa. Tumepokea maoni na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, naomba niendeleo kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge letu, kwa kuliongoza Bunge letu kwa amani wakati wote. Naomba nikushukuru sana leo kwa kutuongoza wakati nawasilisha hoja hii na wakati wa majadiliano ya Muswada huu wa Viwango Tanzania wa Mwaka 2009.

Aidha, napenda vile vile kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuendelea kutoa maelezo ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, pamoja na za Kamati ya Kudumu ya Viwanda na Biashara na zile za Kambi ya Upinzani, kuhusu Muswada wetu wa Sheria ya Viwango Tanzania ya 2008.

Vile vile kwa ruhusa yako, naomba niishukuru Kamati ya Kudumu ya Viwanda na Biashara, kwa ushirikiano wao wa karibu sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, ameelezea vizuri jinsi wanavyoshirikiana na Wizara yetu katika kuhakikisha, tunayatekeleza vizuri majukumu tuliyopewa.

Naishukuru Kambi ya Upinzani, kwa sababu ninyi wenyewe ni mashahidi, leo wameunga mkono Muswada huu kwa kujua kwamba ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. Inanionyesha jinsi siasa inavyokomaa sasa Tanzania, kwa pande zote mbili kukubali kwamba, suala la vyama vingi ni suala la kuimarisha Utawala Bora ndani ya nchi yetu; pale ambapo jambo halifai wanapinga lakini wanapinga kwa namna ambayo inakubalika na pale ambapo mambo yanaenda vizuri, wanaunga mkono. Nawapongeza sana kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maelezo, napenda kuchukua nafasi hii kuungana na wenzangu, kutoa pole kwa familia ya Marehemu Richard Saidi Nyaulawa, kwa kuondokewa na mpendwa wao. Natoa pole pia kwako wewe Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Mama Margaret Sitta, kwa kufiwa na mtoto wa kaka yako.

Naomba kwa ruhusa yako, niwashukuru sana Wananchi wa Jimbo la Hanang, kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi na katika kutekeleza yale yote ambayo yanaleta maisha bora kwa Wananchi wa Jimbo la Hanang na kwa kukubali kushirikiana na Serikali kwa kufanya kazi kwa bidii ili kujiletea maisha bora.

Mheshimiwa Spika, napenda nitambue na kushukuru hoja zote zilizotolewa leo asubuhi na Kamati ya Kudumu ya Viwanda na Biashara, Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge ambao walichangia Muswada wa Viwango Tanzania wa Mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, Wabunge waliochangia Muswada huu kwa kauli na kwa maandishi ni kama ifuatavyo: -

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kauli ni pamoja na Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami, Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mbunge wa Viti Maalum na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Anna M. Komu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah, Mbunge wa Pangani na Mheshimiwa Omari Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini. *(Makofi)*

Wabunge waliochangia kwa maandishi ni pamoja na Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Mbunge wa Kilolo, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mbunge wa Rorya, Mheshimiwa Juma Killimba, Mbunge wa Iramba Magharibi, Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mbunge wa Hai, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge Dimani, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mbunge wa Konde, Mheshimiwa Vuai Khamis, Mbunge wa Magogoni, Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mbunge wa Bububu, Mheshimiwa Dkt. Mzeru Nibuka, Mbunge wa Morogoro Mjini, Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki, Mbunge wa Bukoba Mjini na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, tayari Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami, Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, ameshatoa majibu ya kina kwa hoja nyingi. Jukumu langu kubwa sasa lililobaki ni kuweka msisitizo na kufafanua masuala machache ya kiujumla. Ningependa sana kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami, kwa kutoa maelezo ya kina na kwa umahiri mkubwa. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiunganisha hoja zote, suala kubwa lililojitokeza na ambalo ni changamoto katika Muswada huu ni mwingiliano au mgongano wa majukumu kati ya TBS na Taasisi nyingine za uthibiti, hasa TFDA, EWURA, FCC na Mamlaka au Wakala wa Vipimo na wengine ambao sijawataja. Hoja hii ilichangiwa kama alivyoeleza Mheshimiwa Dkt. Chami na Mheshimiwa Abdisalaam Khatibu, Mheshimiwa Lucy

Owenya, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Mohamed Sanya na Mheshimiwa Dkt. Ali Tarab Ali.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umetambua uwepo wa Taasisi hizi nyingine na kuhakikisha kuwepo kwa ushirikiano wakati wa utekelezaji na utendaji kazi wa taasisi hizi. Napenda kusema kwamba, namshukuru Mtendaji Mkuu wa TFDA, ambaye yuko hapa Dodoma. Baada ya Wabunge wengi kuleta hoja hii, tulikubaliana naye kuona namna gani TBS na TFDA watatekeleza majukumu yao kwa kushirikiana zaidi, badala ya kushindana. Zote mbili ni taasisi za Serikali na lengo letu ni moja la kuhakikisha kwamba, walaji au watumiaji wa bidhaa, wanazipata kwa ubora unaotakiwa na usalama wa afya zao. (*Makofi*)

Kwa *mantic* hii ndio maana Muswada huu wa Viwango umesisitiza ushirikiano kupitia kifungu cha 4(1)(j) na kifungu cha 4(2)(b) cha Muswada. Kwa vile hili ni suala la kiutendaji, linaweza likatatuliwa wakati wa kuandaa kanuni ambapo mipaka ya kiutendaji itabainishwa. Napenda kuahidi kwamba, wakati wa kuandaa kanuni hizi, tutasaidiana na TFDA na taasisi nyingine ambazo ni za uthibiti ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hoja ya mwingiliano, hoja ya kuwepo vigezo vya kutangaza viwango kuwa ya lazima, ilitolewa na Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini na Mwenyekiti wa Huduma za Jamii na Mheshimiwa Dkt. Ali Tarab Ali, Mbunge wa Konde. Hoja hii nayo ni ya kiutendaji na itafanuliwa wakati wa kuandaa kanuni. Napenda kurudia kwamba, tumekaa na TFDA na kukubaliana kwamba, tutakaa pamoja wakati wa kutengeneza kanuni za utekelezaji wa sheria hii. Hata hivyo, vigezo vinavyotumika kwa sasa ni vinne na hutumika kwa bidhaa zinazohusu usalama, afya, mazingira na zile za kuuzwa nchi za nje au *export products*.

Mheshimiwa Spika ni vyema ikaeleweka kwamba, katika biashara ya kikanda na ya kimataifa, uthibiti wa ubora wa bidhaa unaofanywa na mashirika kama TBS, ndio hutumika popote duniani. Hata kama taasisi nyingine za uthibiti zikifanya kazi zake, bado TBS itafanya kazi yake, kwani hutambulika kama taasisi unganishi, yenye kauli ya kitaifa kuhusu masuala ya viwango na uthibiti wa ubora wa bidhaa. Hii inatokana vile vile na kwamba, TBS imepewa umahiri kimataifa, kwa hiyo, kauli yake inakubalika kuliko taasisi nyingine ambazo ni za kitaifa.

Hata hivyo, hili ningependa kuliunganisha na Maabara za TBS; ukienda TBS utakuta maabara ambayo yapo ni ya kisasa na ndio maana inatambulika kimataifa, lakini hii haina maana kwamba, hatuna majukumu ya kuboresha zaidi. Kwa sababu kila muda unapopita na matakwa ya viwango yanabadilika, kwa hiyo, tutaendelea kuboresha Maabara za TBS. Kutambulika huku kwa mfano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, ndiko kumepelekea kuwepo makubaliano ndani ya Afrika Mashariki kwamba, bidhaa zote ambazo zinathibitishwa ubora wake na TBS, zinaruhusiwa kuuzwa katika Afrika Mashariki bila kupimwa tena ubora wake. La msingi katika makubaliano hayo ni kwa kila nchi mwanachama wa Afrika Mashariki, kuwa na mkakati madhubuti wa kuimarisha uwezo wa shirika lake la viwango; ukizingatia miundombinu au *physical infrastructure*

na utaalamu. Kwa hiyo, kazi kubwa ni kuhakikisha kwamba, viwango vya TBS vyenyewe vinaendana na viwango vya nchi hizi za Afrika Mashiriki na nchi nyingine katika dunia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimwa Vuai Khamis, Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimwa Ibrahim Sanya, wametoa hoja kuhusu tatizo la uthibiti wa ubora wa bidhaa za aina zote toka nje ya nchi. Muswada huu umetambua tatizo hili na pengine ndio sababu ya kuuleta Muswada mpya. Kupitia kifungu cha 4(1)(s), TBS imepewa mamlaka ya kisheria, kukagua ubora wa bidhaa kutoka huko zinakotoka, yaani *pre-shipment verification conformity to standards*. Hapo kuna uwezekano kabisa TBS ikafikiriwa kwamba, itakuwa na mgongano na COTECNA.

Mheshimiwa Spika, ningependa kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, jukumu la COTECNA ni kuisaidia Serikali kupitia *TRA*, kutopoteza mapato yanayokana na bidhaa ziingizwazo nchini. Kwa maana nyingine, COTECNA inabidi iangalie bei za vitu vinavyoagizwa nchini kama zinakwenda na bei ambazo zinatambulika kimataifa ili Serikali isikose mapato yake. COTECNA haina jukumu la kuangalia viwango au haitakuwa na jukumu la kuangalia usalama wa afya za wananchi, kupitia bidhaa zinazoagizwa. Kazi kubwa ya COTECNA ni kuona nchi inapata thamani ya fedha kupitia ushuru kama inavyotegemewa.

Mheshimiwa Spika, Wizara itazingatia ushauri wote uliotolewa na Kamati ya Kudumu ya Viwanda na Biashara, Kambi ya Upinzani na Wabunge wote katika maeneo yafuatayo: Kwanza, kabla ya kuangalia maeneo hayo, napenda kusema kwamba, TBS imeshaanza maandalizi ya kutafuta makampuni yenye uwezo wa kufanya kazi hii ya kufanya *pre-shipment verification* na *conformity* ili kuona kwamba, kabla ya vitu kuingia Tanzania, vina ubora unaotakiwa badala ya kungojea kufika na kuleta hasara hata kwa waagizaji wa ndani ya nchi, kwa sababu haitakuwa wale tu walioagiza watapata hasara bali na nchi vilevile itapata hasara kwa namna moja au nyingine, hasa pale ambapo bidhaa inayoagizwa ikikosa usalama kwa afya ya binadamu, gharama itakuwa kubwa zaidi. Kwa hiyo, tunapenda kuchukua ushauri huo na tutazingatia kwa siku za baadaye. Sasa kama nilivyosema, Wizara itazingatia ushauri wote uliotolewa na Kamati ya Kudumu ya Viwanda na Biashara na vilevile Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Kwanza, masuala ya kuangalia upya ili yapelekwe kwenye Tume ya Muungano kujadiliwa na kuangalia uwezekano wa sheria kutumika pande zote za Muungano; suala hili ni la msingi hata sasa kwani bidhaa nyingi zinazolingia nchini kupitia Zanzibar huuzwa Tanzania Bara na zinaangaliwa ubora wake. Kwa hiyo, inakuwa ni vizuri zaidi na inakuwa bora zaidi kama tutakuwa na ushirikiano wa karibu ili bidhaa itakapotoka Zanzibar isiwe chanzo cha kuvuruga Muungano wetu.

Pili, kuzingatia Wajumbe wote watakaoteuliwa katika Bodi kuwa na vigezo vinavyoendana na majukumu ya TBS na hili nalo ni la msingi sana, kwa sababu umahiri wa TBS utatokana na Wajumbe wa Bodi ambao wapo mahiri. Kwa hiyo, tutazingatia

sana wale ambao wanakuwa na *qualification* au uwezo unaotakiwa, ndiyo watakaolingia katika Bodi ya TBS.

Tatu, elimu kuhusu viwango na jinsi ambavyo Sheria hii itawasaidia wananchi wote. Hili ni la lazima na wananchi wengi tayari wameshataka kupata elimu hiyo; wale wanaoagiza na wale wanaotumia. Tukifanya hivyo, tutapata ushiriki wa wananchi badala ya kuwa tunachoma bidhaa, watu wenyewe watatusaidia kufanya uthibiti huo.

Nne, kuweka utaratibu mzuri wa kusaidia wajasiriamali na wafanyabiashara wadogowadogo ili waweze kufikia viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, wajasiriamali wadogowadogo ndiyo ambao wanaendesha uchumi wa Tanzania kwa sehemu kubwa. *Informal Sector* ni 66% ya uchumi wa Tanzania. Kwa hiyo, kama tutaishirikisha *sector* hii, utaona kwamba, tutapata ushirikiano mkubwa na mambo mengi yatakwenda vizuri zaidi kuliko ilivyo hivi sasa. Tutashirikiana na SIDO na nilishaelekeza Shirika la TBS katika kila wanalofanya, SIDO wawepo, ili pale ambapo viwango vimefikiwa, waweze kuweka nembo wajasiriamali waweze kuuza bidhaa zao bila usumbufu wowote. Nembo ya TBS inajaribu kuonyesha kwamba, TBS inaamiwa na watu wengi, basi uzaji wa bidhaa hiyo unakuwa mkubwa zaidi na wa urahisi zaidi.

Tano na mwisho, nafasi ya Mtendaji Mkuu wa TBS kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa umahiri mkubwa, kushindanishwa kabla majina matatu kupelekwa kwa Rais kwa uteuzi utakaotakiwa. Hili ni muhimu kwa sababu tunataka atakayekuwa anaendesha shirika hili, awe ni yule ambaye hata dunia na ndani ya nchi anaaminika na anakubalika. Ushindani ndiyo ambao utatupatia mtu wa aina hiyo, hasa pale utakapofanywa kwa namna ambayo inatakiwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoelezea leo asubuhi, sheria inayopendekezwa ni ya umuhimu na wa manufaa makubwa kwa taifa letu katika kukuza na kuimarisha uwekezaji, viwanda na biashara. Kutekelezwa kwa Sheria hii, kutasaidia sana wafanyabiashara wakubwa na wajasiriamali wengi na kukuza viwanda vidogovidogo, ambavyo vitasaidia kuwa na viwango. Katika kufanya hivyo, tutakuwa tunaimarisha uchumi wa taifa letu hasa katika soko hili huru ambalo utawandazi ndiyo unaliendesha.

Mheshimiwa Spika, jukumu kubwa ambalo ni changamoto kwa Wizara yangu ni kuzingatia ushauri wote uliotolewa na kutayarisha Kanuni mapema kwa kuhusisha vyombo vyote husika, ambavyo ni pamoja na TFDA, FCC, WMA na wengine. Nina hakika kuwa, kwa kushirikiana na kufanya kazi kwa pamoja katika kutekeleza sheria hii, tutawasaidia wananchi na hivyo kuleta maendeleo kwa nchi yetu, ambalo ndilo lengo la Muswada huu.

Ninapenda kuwashukuru sana, kwa ushauri mlioutoa kwa hoja zote na kama kuna Mbunge ambaye hoja yake haijajibiwa vizuri, basi tunaweza tukampa kwa maandishi

ilimradi siku ya leo mmetusaidia sana kuiboresha sheria hii na yale yote tuliyoyaahidi tutayatekeleza. Ninawashukuru sana kwa usikivu wenu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)

SPIKA: Ahsante sana Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, kwa ufafanuzi wa hoja zote za Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, hoja ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, iliyopo mbele yetu imetolewa na kuungwa mkono. Sasa tutaingia katika utaratibu unaofuata wa kutunga Sheria na ninamwomba Katibu atufahamishe utaratibu huo.

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Viwango wa Mwaka 2008 (The Standards Bill, 2008)

Ibara ya 1

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 2

Ibara ya 3

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 4

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nipate tu maelezo ya ziada, part ya pili, ibara ya nne, ambapo nilichangia nilipopata nafasi na nikatoa mifano kwa sababu suala hili si la Muungano. Nilikuwa namtaka Mheshimiwa Waziri, ashirikiane sana na kitengo kile cha kumlinda mlaji kule Zanzibar ili kuona kuwa Watanzania kwa ujumla, hatuwezi kupata madhara kutokana na mambo hayo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niligusia pia suala zima la rushwa ambalo lilynagusa pande zote ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa sasa si mjadala ungelenga kwenye kifugu chenyewe.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nipo hapo, sasa nilikuwa sijapata maelezo ya ule ushirikiano niliokuwa nautaka baina ya Kitengo hiki cha Bara na kile cha Zanzibar. Suala langu kubwa ni ushirikiano wa pamoja katika kutekeleza suala hili.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, kwa kutaka ufafanuzi zaidi, pamoja na kwamba, nilitoa ufafanuzi na kukubali kwamba ni muhimu sana TBS na kile Kitengo cha Zanzibar, kushirikiana kwa karibu sana ili tusitoe usumbufu kwa wananchi wa pande zote mbili na hata nikaendelea kusema kwamba, ili tupunguze mgogoro ndani ya Muungano.

Sasa zaidi ya hapo, sijui nitafanyaje lakini kama anataka kujua ni namna gani, nafikiri ni vyema tukaachia hilo kwenye TBS yenyewe na Kitengo ambacho kipo Zanzibar.

MWENYEKITI: Ahsante sana, naona Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir ameridhika.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 5

Ibara ya 6

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 7

MWENYEKITI: Ibara ya saba ina marekebisho ambayo Msemaji wa Kambi ya Upinzani aliyatoa, Katibu aliyapokea na yamesambazwa. Mheshimiwa Lucy Owenya, anataka kutoa maelezo.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilipeleka *schedule of amendment* lakini kutokana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwamba, Rais hatakuwa anateua tu ila wanatangaza kazi ile halafu ndiyo wanapeleka majina matatu kwa Rais, nita-*withdraw amendment* yangu. Natoa angalizo kwamba, hayo majina matatu basi yatakayoteuliwa, yawe ndiyo hayo hayo Rais atateua mmoja kati ya hayo majina matatu.

MWENYEKITI: Ni kweli ndiyo utaratibu ulivyo kwa Taasisi zote hizi, kwa sababu kuna Sheria Mama inayotawala hayo mengine, ndiyo maana halionekani hapa. Ule utaratibu wa hatimaye Rais kupata majina matatu, umeelezwa katika taratibu za kiutumishi.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 12

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 13
Ibara ya 14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Ali Tarab Ali na Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo.

Mheshimiwa Dkt. Ali Tarab Ali, wewe ulikuwa unahama tu? Ooh! Basi ni vizuri kuangalia mambo yapi yanaendelea la sivyo mnamchanganya Mwenyekiti wa Kamati.

Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ibara ya 15(2) nayo labda ni English tu anasema: “*Within six months of the close of each financial year the Board shall cause ...*,” nilikuwa nafikiri *shall cause* sijui kama hilo neno ni *correct*?

MWENYEKITI: Naona hiyo iliyopo ni sahihi, yaani watapeleka; *you will cause to do something*, ndio *standard drafting in English*.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 16
Ibara ya 17

Ibara ya 18
Ibara ya 19

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 20
Ibara ya 21

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

MWENYEKITI: Mbona kimya? Hata Mheshimiwa Hawa Ghasia amekaa kimya sijui kwa nini? *(Kicheko)*

Ibara ya 22

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 23

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 24

MHE. DKT. ALI TARAB ALI: Ahsante sana, mimi nilitaka ufafanuzi tu kwa sababu kifungu cha 24 kinazungumzia kuteuliwa kwa huyu *Inspector*, ambapo hapa ndio kuna tatizo na uchunguzi wenyewe unahusika na chakula, madawa na vipodozi. Hapo nilitaka ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, itakuwaje na jukumu hili linaangukia kwenye TFDA? Ahsante.

MWENYEKITI: Sijui kama Mheshimiwa Waziri amemuelewa, amesema haraka sana.

Hebu rejea kidogo na Kiswahili chako unajua sisi wengine wa Bara inakuwa tabu kidogo. *(Kicheko)*

MHE. DK. ALI TARAB ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kifungu hiki kinaelezea kuteuliwa *Inspector*, yaani Mkaguzi na hapa ndiyo penye matatizo makubwa kwa sababu Mamlaka ya Chakula na Dawa inashughulikia mambo ya chakula, dawa na vipodozi; sijui hapa itakuwaje uhusiano baina ya Mamlaka yenu na TFDA?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa hoja ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliahidi ushiriki wa TFDA, pale ambapo masuala ya chakula yanahusika na kwa sababu hii ipo kwenye ngazi ya Waziri, basi nitashirikiana na Waziri wa Afya au pale ambapo Wizara ile ambayo TFDA nayo itahusika. Kwa hiyo, napenda kuisisitiza zaidi umuhimu wa kushirikisha taasisi zile ambazo zinahusika.

MWENYEKITI: Ahsante sana, labda niongezee tu kwa hali ya ujanja ujanja na ulanguzi uliopo hata vyombo viwili vikienda kukagua kuna tatizo gani au sikuelewa vizuri? Takwimu zilizopo asilimia 40 ya bidhaa zinazoingia ndani ya nchi yetu ni feki, acha watu wapate tabu kidogo; unakaguliwa asubuhi na TFDA jioni anakuja huyu basi aaa! Basi nisiisemee Serikali. Ahsante sana.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32

(Ibara ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 33

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36
Ibara ya 37
Ibara ya 38

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Jedwali

(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati)

ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

(Bunge lilirudia)

Muswada wa Sheria ya Viwango wa Mwaka 2008
(The Standards Bill, 2008)

(Kusomwa Mara ya Tatu)

SPIKA: Je, Mheshimiwa Waziri, unaweza sasa kutupa taarifa ya yale yaliyotokea katika Kamati?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima, imepitia Muswada wa Sheria uitwao *The Standards Bill, 2008* ibara kwa ibara na kuukubali, pamoja na marekebisho yote yaliyofanyika. Hivyo basi, ninaomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa *The Standards Bill, 2008* sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyopo mbele yetu na ambayo imeanza kujadiliwa tangu leo asubuhi ni ya kupitisha Muswada wa Viwango wa Mwaka 2008 *(The Standards Bill, 2008)*. Hoja hiyo ilitolewa na kuungwa mkono na baada ya hatua zake zote, sasa nawahoji muamue.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa
Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

SPIKA: Walioafiki wameshinda. Nadhani wasioafiki wanaleta bidhaa feki hawa. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, Muswada wa Sheria ya Viwango umesomwa kwa mara ya tatu na kwa hiyo, kwa taratibu zetu sasa umeiva na utafikishwa tu kuhitimishwa kwa hatua zile nyingine za kuweza kupata saina ya Rais.

Wizara na Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kazi yote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho Kwenye Sheria Mbalimbali wa
Mwaka 2008
(*The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Bill, 2008*)**

(Kusomwa Mara ya Pili)

SPIKA: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mtoa hoja hii ya Marekebisho ya Sheria kwenye Sheria Mbalimbali, yaani *Miscellaneous Amendment Bill, 2008*.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria uitwao *The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Bill, 2008*, sasa usomwe mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa yote, kwa kutuwezesha kuvuka mwaka uliopita na kuuona mwaka huu tukiwa bukheri wa afya. Napenda nitumie wasaa huu, kumtakia kila mmoja wetu, kheri ya mwaka 2009. Namwomba Mwenyezi Mungu, aufanye mwaka huu kuwa wa mafanikio na manufaa kwetu sote, Taifa letu na Watanzania wote kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya salamu hizo za mwaka mpya, kwa ruhusa yako, naomba nilete mbele yenu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2008, unaokusudia kufanya marekebisho katika Sheria mbalimbali zilizotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kwa kuupitia na kuuchambua Muswada huu na kwa ushauri mzuri walioutoa.

Ushauri huu umetusaidia sana kuboresha na hivyo kuwezesha uwasilishaji mbele ya Bunge lako Tukufu. Tunawashukuru kwa dhiti, Wajumbe wote wa Kamati hiyo, kwa kazi nzuri waliyoifanya na kwa ushirikiano waliotupatia.

Mheshimiwa Spika, Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Kazi na Majukumu ya Kabidhi Wasii Mkuu, Sura ya 27; Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo, Sura ya 108; Sheria ya Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo Tanzania; Sheria Namba Tano ya Mwaka 2007; Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298; Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa, Sura ya 395; Sheria ya Huduma ya Uendeshaji wa Mashtaka ya Kitaifa Namba 27 ya Mwaka 2008; Sheria ya Uchawi, Sura ya 18; Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16; Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200; Sheria ya Leseni za Usafirishaji, Sura ya 317; na Sheria ya Ardhi, Sura ya 113.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali zilizotungwa na Bunge, ulitangazwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 17 Oktoba, 2008 na umechapishwa tena katika Gazeti la Serikali, baada ya kufanya marekebisho kadhaa,

ikiwa ni pamoja na kuondoa marekebisho yaliyokuwa yamependekezwa katika Sheria ya Mahakama Suluhishi ya Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Muswada huu ni kufanya marekebisho katika Sheria mbalimbali zilizoainishwa ili kuboresha utekelezaji wake na pia kuondoa upungufu ambao umedhihirika wakati wa utekelezaji wa masharti ya Sheria hizo. Aidha, malengo ya marekebisho haya ni kuweka masharti ambayo yatawezesha kukuza na kulinda dhana ya Utawala Bora wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu 12. Sehemu ya kwanza, inahusu masuala ya utangulizi kama vile jina la Sheria inayopendekezwa na uwiano wa masharti ya vifungu vipya na masharti ya Sheria zinazofanyiwa marekebisho.

Sehemu ya pili ya Muswada huu, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kazi na majukumu ya Kabidhi Wasii Mkuu, Sura ya 27 ili kufuta baadhi ya vifungu katika Sheria hiyo kwa kuwa vimepitwa na wakati. Aidha, inapendekezwa pia kuongeza kiwango cha chini cha thamani ya mali ya Marehemu, ambacho Kabidhi Wasii Mkuu anaweza kusimamia mirathi, tofauti na kiwango cha sasa.

Sehemu ya tatu ya Muswada, inapendekeza kurekebisha na kufuta baadhi ya vifungu katika Sheria ya Msajili wa Vizazi na Vifo, Sura ya 108 ili kuweka masharti ya matakwa ya kusajili vizazi na vifo vyote, tofauti na hali ilivyo hivi sasa.

Sehemu ya nne ya Muswada, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Taasisi ya Mafunzo kwa Vitendo ili kumwondoa Jaji Kiongozi kwenye Ujumbe wa Bodi ya Taasisi hiyo na badala yake kumuweka Msajili wa Mahakama ya Rufani. Marekebisho haya, yameanza kuzingatiwa katika itifaki kwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi hiyo ni Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Inapendekezwa pia kuongeza nafasi moja ya Mjumbe wa Bodi ambaye ni Mwakilishi wa Wanafunzi wa Taasisi hiyo.

Sehemu ya tano, inapendekeza Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 ili kuondoa dhana ya sasa kwamba, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiyo pia Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria. Marekebisho haya yanalenga kuendana na muundo mpya wa kiutendaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Sehemu ya sita, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Bima ya Afya ya Taifa, Sura ya 395, kwa lengo la kuweka mazingira yatakayoruhusu watumishi wa umma wastaafu kuendelea kupata mafao yanayotolewa na Mfuko wa Bima ya Afya baada ya kustaafu.

Aidha, inakusudia kuruhusu Waheshimiwa Madiwani wasio Wabunge, kunufaika na mafao ya Mfuko huo katika kipindi cha Uongozi wao.

Sehemu ya saba ya Muswada huu inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Huduma ya Uendeshaji wa Mashtaka ili kuweka utaratibu wa Kurugenzi ya Mashtaka, kukasimu mashtaka yake chini ya Sheria hiyo.

Sehemu ya nane ya Muswada huu inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Uchawi, Sura ya 18 ili kuondoa masharti yanayotaka kabla ya kufungua shtaka chini ya Sheria hiyo, kupata idhini ya Mwanasheria Mkuu au Wakili wa Serikali Mfawidhi.

Sehemu ya tisa, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kanuni za Adhabu. Sura ya 16 inapendekeza kufuta kifungo cha 162 cha Sheria, kinachotaka kabla ya kumfungulia mtu mashtaka ya kuingiliana kimapenzi na maharimu apate idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Sehemu ya kumi, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200. Katika mabadiliko haya, inapendekezwa kufuta aya ya (1) na ya (2) katika jedwali la kwanza. Aya hizo zinafutwa kwa sababu masharti yake yamehuishwa na kuingizwa katika Sheria ya Kupambana na Kuzuia Rushwa ya Mwaka 2007. Sheria hiyo ambayo ni mpya, imeweka masharti bora zaidi.

Sehemu ya kumi na moja, inapendekeza kurekebisha Sheria ya Leseni za Usafirishaji, Sura ya 317 ili kuruhusu pikipiki zikiwemo za magurudumu matatu, maarufu kwa jina la Bhajaj, kuweza kupata leseni za usafirishaji wa abiria kwa malipo na kukata bima ya kinga kwa abiria.

Sehemu ya kumi na mbili, ina mapendekezo na marekebisho katika Sheria ya Ardhi, Sura ya 113, ili kuongeza muda wa leseni za makazi, zinazotolewa chini ya Sheria hiyo. Aidha, inapendekezwa kuendelea kuzitambua kisheria, hati za gawiwo la awali, yaani *offer document* za umiliki wa ardhi, zilizotolewa mapema kabla ya marekebisho ya Sheria ya Ardhi, kwa kufuta masharti yanayohusu utoaji wa hati za gawio la awali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, kwa kupitia kwako, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, waujadili Muswada huu na hatimaye upitiwe na kuwa Sheria ambayo italeta marekebisho ya Sheria zilizokusudiwa.

Aidha, napenda kukushukuru tena kwa kunipatia nafasi hii na kupitia kwako, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana na naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kama kawaida, sasa nitaomba tupokee maoni ya Kamati husika, ambayo ni Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Mheshimiwa George Lubeleje. (*Makofi*)

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni Na. 86, kifungu cha 5, Toleo la Mwaka 2007, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2008 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2008*).

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilikutana tarehe 14 Januari, 2009 katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam na kupokea mapendekezo ya Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2008, yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Johnson Mwanyikwa (Mbunge).

Aidha, Kamati ilipokea maoni ya wadau kutoka Taasisi ya Msaada wa Sheria, yaani *National Organization for Legal Assistance* (nola) na kutoka Chama cha Wanasheria Wanawake nchini Tanzania (*Tanzania Women Law Association - TAWLA*).

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya uchambuzi wa kina, kwa ujumla Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kuhusu Muswada huu, yaliyowasilishwa na mtoa hoja. Kamati inatumaini kuwa, endapo Bunge litaridhia kufanya marekebisho katika Sheria zinazohusika, sheria hizo zitasaidia sana kuimarisha utendaji katika maeneo yanayohusika. Pamoja na hayo, Kamati inapenda kutoa maoni na mapendekezo kwenye baadhi ya sheria kama ifuatavyo:-

Kwanza, Marekebisho ya Sheria ya Kabidhi Wasii Mkuu, Sura ya 27 (*Amendment of Administrator-General (Powers and Functions) Act, Cap. 27*).

Mheshimiwa Spika, kimsingi, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kuvifuta vifungu vinavyohusika kama alivyoeleza mtoa hoja, kwani vikibaki kama vilivyo katika Sheria hiyo, havitakuwa na kazi yoyote hasa ikizingatiwa kuwa hivi sasa hakuna tena nyumba ambazo zinatumiwa na askari au wafanyakazi wa kikoloni.

Sheria ya pili ni marekebisho ya Sheria ya Vizazi na Vifo, Sura ya 108 (*Amendment of the Births and Deaths Registration Act, Cap.108*).

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya kuleta mapendekezo ya kuirekebisha sheria hii, Kamati inashauri kwamba, Serikali iweke utaratibu sasa wa kuhakikisha kuwa, vyeti vya usajili wa vizazi na vifo vinapatikana kwa urahisi, hasa huko vijijini kwa kuzingatia hali halisi ya jiografia ya vijiji vyetu.

Aidha, Taasisi zinazohusika na zoezi hilo, zimeshirikiana moja kwa moja na Taasisi zilizopo vijijini, vikiwemo Vituo vya Afya na Zahanati. Kwa kufanya hivyo, Kamati inaamini kuwa, wananchi wataondokana na urasimu usiokuwa wa lazima katika kupata vyeti hivyo.

Tatu, Marekebisho ya Sheria ya Taasisi ya Sheria Tanzania ya Mwaka 2007 (*Amendment of the Law School of Tanzania Act, 2007*).

Mheshimiwa Spika, Kamati inaafikiana na mapendekezo yaliyokusudiwa katika Sheria hii, kwa vile yanalenga kurekebisha kasoro zilizojitokeza katika utendaji unaogusa itifaki za Uanasheria na Mhimili wa Mahakama. Marekebisho haya yakikubalika, Bodi ya Taasisi hiyo ambayo ndiyo chombo kikuu cha uendeshaji, kitafanya kazi kwa ufanisi bila migongano iliyopo.

Sheria ya Nne ni Marekebisho ya Sheria Utumishi wa Umma, Sura ya 298 (*Amendment of the Public Service Act, Cap. 298*).

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya kurekebisha Sheria hii, kwa kuwa yanalenga kuimarisha utendaji katika utumishi kwenye Taasisi za Sheria kwa kuondoa utatanishi uliopo wa nyadhifa au vyeo vya Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria. Pamoja na hayo, baada ya marekebisho hayo kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu, Kamati inashauri kuwa, elimu ya kutosha itolewe na chombo kinachohusika kwa Taasisi za Umma na Wananchi kwa ujumla, kuhusiana na marekebisho hayo.

Sheria ya tano ni Marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya, Sura ya 395 (*Amendment of the National Health Insurance Fund Act, Cap. 395*).

Mheshimiwa Spika, kwanza, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwaingiza Madiwani wasiokuwa Wabunge katika Sheria hiyo. Hata hivyo, Kamati inashauri kwamba, Serikali iwe makini katika utekelezaji wa Sheria hiyo kwa kuwa watumishi wengi wa umma na wadau wengine wa Mfuko huo, hawaelewi mambo mengi yanayohusu uendeshaji wa Mfuko huo. Pamoja na kwamba, Mfuko huo umefanya kazi kubwa na nzuri katika kipindi kifupi, Kamati inaishauri Serikali kutoa elimu zaidi na kuongeza vifaa vinavyohitajika kwa matibabu katika hospitali za hapa nchini, hasa zilizopo Mikoani na Wilayani.

Sheria ya Sita ni Marekebisho ya Sheria ya Huduma ya Mashtaka ya Taifa ya Mwaka 2008 (*Amendment of the National Prosecution Service Act, 2008*).

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukubaliana na mapendekezo ya sheria hii, yanayolenga kuboresha utendaji katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini, Kamati inaishauri Serikali kutatua baadhi ya matatizo yanayozikabili Taasisi zinazoshughulikia utoaji haki ili kukabiliana na tatizo kubwa la msongamano wa mahabusu waliopo magerezani.

Sheria ya saba ni Marekebisho ya Sheria ya Uchawi Sura ya 18 (*Amendment of the Witchcraft Act, Cap. 18*).

Mheshimiwa Spika, kimsingi, Kamati inaafikiana na mapendekezo yaliyokusudiwa ambayo yanalenga kukabiliana na mabadiliko makubwa ya mazingira kwa wakati yalipowekwa masharti hayo na hali halisi ya maisha ya sasa. Pamoja na hayo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuchukua hatua kali na za haraka, kuhusu suala la mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi (*albino*), wanaouawa kwa imani za kishirikina.

Kupitia Bunge lako Tukufu, Kamati inatumia fursa hii pia kuwataka Watanzania wote, kupiga vita uovu wa kila aina, zikiwemo imani potofu na kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anapata hifadhi ya maisha yake na nchi yake inaendelea kuwa kisiwa cha utulivu na amani. (*Makofi*)

Sheria ya nane ni Marekebisho ya Sheria Makosa ya Jinai, Sura ya 16 (*Amendment of the Penal Code Cap. 16*).

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yaliyokusudiwa katika Sheria hii, yanalenga kuimarisha utendaji wa Mahakama zetu za chini (*subordinate courts*). Kamati inaafikiana na mapendekezo hayo. Hata hivyo, inaishauri Serikali ivitumie vyombo vya habari, watu binafsi na asasi zisizo za Kiserikali, kusaidia kuielimisha jamii kutokomeza vitendo vya baadhi ya watu kuwa na uhusiano wa kimapenzi na maalimu wao au watu wenye uhusiano wa kindugu.

Sheria ya Tisa ni Marekebisho ya Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200 (*Amendment of the Economic and Organised Crimes Control Act, Cap. 200*).

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria hii yanakusudia kuondoa migongano iliyopo ya kisheria na kuimarisha utendaji kazi wa Taasisi zinazohusika na kupambana na kuzuia rushwa. Pamoja na nia nzuri ya marekebisho hayo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea na jitihada za kupambana na tatizo la rushwa kwa nguvu zake zote.

Sheria ya kumi ni Marekebisho ya Sheria za Leseni na Usafirishaji, Sura ya 319 (*Amendment of the Transport Licensing Act, Cap. 317*).

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa Sheria hii katika kuongeza kipato cha wananchi, Kamati inaishauri Serikali kufikiria uwezekano wa baiskeli kutumika kama chombo cha usafirishaji wa kibiashara, kwa kuwa wananchi walio wengi hivi sasa huko vijijini, hukitumia chombo hicho kwa shughuli kama hizo kwa ajili ya kujipatia kipato cha kuendesha maisha yao. (*Makofi*)

Vilevile Kamati inashauri kwamba, Serikali iziagize mamlaka zinazosimamia utoaji wa leseni, kuhakikisha kuwa elimu ya kutosha inatolewa kwa wale wote wanaoendesha biashara hiyo ili kulinda usalama wa wateja na wale wote wanaopewa huduma hiyo.

Marekebisho ya Ardhi, Sura ya 113 (*Amendment of Land Act, Cap. 113*).

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya sheria yanakusudia kuondoa kasoro nyingi, zilizoleta usumbufu mkubwa katika utekelezaji wa sheria hiyo. Kwa kuzingatia kuwa zipo sheria nyingine zinazolingiliana na sheria hii katika utekelezaji wa masuala ya ardhi, Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya mambo mbalimbali kama vile dhana nzima ya Utawala Bora na Utawala wa Sheria inavyotekelezwa katika vyombo vinavyoshughulikia utoaji haki, yakiwemo Mabaraza ya Ardhi Vijijini, ambayo yanaweza kuwa kikwazo cha utekelezaji wa sheria hiyo. Hii ni pamoja na kuzifanyia uchambuzi wa kina, sheria zote zinazohusiana na ardhi kwa ajili ya kuondoa migogoro na urasimu usio wa lazima katika masuala ya ardhi vijijini ili kuondoa kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nachukua fursa hii, kukushukuru kwa kunipatia fursa hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati. Vilevile namshukuru Mheshimiwa Johnson Mwanyika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wataalam wake, kwa kushirikiana vyema na Kamati yangu wakati wa kushughulikia Muswada huu. Aidha, nachukua fursa hii, kuwashukuru Wajumbe wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kuujadili na kuuchambua Muswada huu. Kwa heshima na taadhima, niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mwenyekiti, Mheshimiwa Ramadhan Maneno, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Yusuf Makamba, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Rajab H. Juma, Mheshimiwa Abubakar K. Bakary, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Salim Y. Mohamed, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Abbas Mtemvu na Mheshimiwa Benedict N. Ole-Nangoro.

Aidha, napenda kumshukuru Dkt. Thomas Kashililah, Katibu wa Bunge na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kufanikisha shughuli za Kamati kama zilivyopangwa. Bila kuwasahau Makatibu wa Kamati hii; Ndugu Charles Mloka, Ndugu Ramadhan Abdallah na Ndugu Elihaika Mtui, kwa kuratibu shughuli zote za kamati na kuhakikisha kuwa, maoni ya Kamati yanakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naiunga mkono hoja hii na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa George Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika eneo hili la Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Fatma Maghimbi. Siwaoni Waheshimiwa Wabunge wa CHADEMA wakishangilia; sasa sijui lakini endelea Mheshimiwa. *(Kicheko)*

MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBA: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uzima na nguvu na kuweza kusimama mbele yenu ili kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Muswada wa sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani, naomba kwanza, nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa George Lubeleje, kwa kuiongoza Kamati hii vizuri na umahiri wake alionao katika uongozi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa George Lubeleje, awe Mwenyekiti wa Kudumu wa Kamati hii. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa utangulizi huo, sasa kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kutoa baadhi ya upungufu uliojitokeza katika baadhi ya vifungu vya sheria, ambazo zinafanyiwa marekebisho katika Muswada huu.

Nitaanza na sehemu ya pili: Kabidhi Wasii Mkuu, kifungu cha tisa cha Muswada kinachofanyia marekebisho kifungu cha 52(1) cha Sheria ya Kabidhi Wasii Mkuu, Sura ya 27. Kwa ujumla, Kambi ya Upinzani haina pingamizi na marekebisho hayo ila inataka pia kifungu cha 52 kifanyiwe marekebisho kwa kufuta maneno “*ten thousand*” na kuweka “*ten million*” ili kiende sambamba na mabadiliko ya kifungu cha 52(1).

Sehemu ya Tatu: Usajili wa Vizazi na Vifo. Huduma hii hivi sasa inapatikana kwa Mkuu wa Wilaya tu. Kama huduma hii inatakiwa ipate ufanisi mzuri kabisa, basi Kambi ya Upinzani inapendekeza iwekwe vijijini. Vijiji vingine vipo mbali sana na Makao Makuu ya Wilaya, kwa mfano, Ngorongoro, Makao Makuu ya Wilaya ni Kilomita 394 na upande wa pili wa Wilaya hiyo una kilomita 384; huwezi kumtegemea mtu wakati amefiwa kwenda kilomita zote hizo kusajili kifo cha ndugu yake na hata kuandikisha vizazi siyo rahisi. Kwa hiyo, watoto wanaweza kukosa vyeti vya kuzaliwa na baadae watakosha kuingia shuleni.

Sehemu ya Sita: Bima ya Afya; kifungu cha 25 cha Muswada kinachofanyia marekebisho kifungu cha (2) cha Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya, Sura ya 395. Kifungu kidogo cha (b) katika Muswada kama kinavyosomwa, nanukuu: “*Inserting after the words “public servant” which appears in subsection (2) the phrase “erson or group of persons.”*”

Kifungu cha 2(2) cha sheria kinachotakiwa kufanyiwa marekebisho kinasomwa kama ifuatavyo, naomba kunukuu: “*The Board may from time to time by Notice published in the Gazette determine any other category of members to the Fund*”

Mheshimiwa Spika, ukisoma kifungu tajwa katika Sheria Mama, hakuna maneno yanayotajwa katika Muswada huu. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaiomba Serikali kuwa makini kadiri iwezekanavyo, wakati wa kurekebisha sheria ndogo ndogo kama hizi. Kosa kama hili, linaweza kutoa mwanya kwa watu wajanja kufanya yasiyotakiwa kufanywa na lawama zitaelekezwa kwa wale wanaotunga sheria.

Kifungu 27(e), Madiwani wamekubaliwa kuingia ndani ya Mfuko huu, lakini akitoka tu huduma hii inafutika.

Mheshimiwa Spika, mtu anapostaafu ndio wakati anapohitaji huduma za afya. Kambi ya Upinzani inapendekeza kwamba, huduma hii iendele mpaka mtu anapostaafu na sio tu Madiwani bali kwa Wafanyakazi wote. (*Makofi*)

Sehemu wa Kumi na Moja katika Muswada imezungumzia usajili wa pikipiki tu. Kambi ya Upinzani inaomba kufahamu, baiskeli zitasajiliwa pahali gani kwa sababu pikipiki sio usafiri pekee vijijini hasa Wasukuma na Wanyamwezi. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Ungetakiwa utaje mikoa tu siyo kabila. (*Kicheko*)

MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI - MSEMAMI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBA: Sehemu ya Kumi na Tatu: Sheria ya Ardhi; kifungu cha 46 cha Muswada kinafanyia marekebisho kifungu cha 23 cha Sheria ya Ardhi, Sura ya 113. Kifungu cha 23(5) cha Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 hakina vifungu vidogo bali vifungu vidogo vidogo vya a, b na c vipo chini ya kifungu cha 23(3).

Mheshimiwa Spika, katika uandishi wa Sheria, (,) inaweza kubadili maana yote ya sheria. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara hasa Idara ya *Drafting*, iwe makini sana wakati wa *ku-draft*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache ambayo Kambi ya Upinzani imeona ni muhimu, nawashukuruni sana kwa kunisikiliza. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Fatma Maghimbi, kwa maelezo yako mafupi lakini yameeleweka.

Waheshimiwa Wabunge, hatua ya sasa ni kusikia kutoka kwa wachangiaji wa hoja hii ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu. Hadi sasa, nina majina matano na bado kuna nafasi ya kuweza kuongeza mengine. Majina niliyonayo ni Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa John Momose Cheyo na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah.

Kwa hiyo, kama nilivyosema, Muswada huu unagusa sheria mbalimbali, bado ipo fursa ya kuweza kuleta maombi ya kuchangia hapa kwa Katibu. Tunakusudia *winding up* ya Muswada iwe ni kesho asubuhi. Kwa hiyo, sasa nitamwita Mheshimiwa Vita Kawawa, wakati huo Mheshimiwa Felister Bura ajiandae kuchangia.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, naomba nami nitumie fursa hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali (*Miscellaneous Amendment Bill, 2008*).

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mwanasheria Mkuu, kwa kuwasilisha vyema hoja hii na pia Mwenyekiti wa Kamati kwa kuwasilisha mawazo ya Kamati na Mwakiilshi wa Kambi ya Upinzani kwa kuwasilisha mawazo yao.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na sehemu ya tatu ya Muswada huu, inayo-*amend the Births and Deaths Registration Act, Cap. 108*. Nakubaliana na *amendment* zote zilizofanyika katika eneo hili, lakini nina ushauri kwamba, tusiishie katika ku-*amend* tu sheria bali pia tuimarisha vyema kitengo hiki cha RITA. Malengo ya kufanya *amendment* hii ni kuweka masharti ya matakwa ya kusajili vizazi na vifo vyote, sivyo ilivyokuwa awali; kulikuwa na baadhi tu ya vifo na vizazi vilikuwa vinalazimika kusajiliwa.

Mheshimiwa Spika, sasa hii maana yake inaonyesha kwamba, RITA itaongeza kazi zake. Sasa tunaomba tusaide ili iweze kufanya kazi yake vyema, kwa sababu ni eneo nyeti sana kwa taifa letu. Kwa hiyo, tuipe uwezo wa kifedha na kiutendaji ili kuwa na mazingira bora ya kisasa na wafanye kazi kwa kuweka kumbukumbu kulingana na hali iliyopo ya sasa ya teknolojia ya wakati huu. Pia iweze kufanya vizuri kazi yake ya kuweka kumbukumbu ya waliozaliwa zamani. Utaratibu mahususi wa kupata vyeti vya kuzaliwa kwa wale waliozaliwa zamani.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie sehemu ya (6) inayo-*amend National Health Insurance Fund Act, Cap. 395*. Mimi naamini eneo hili malengo yake makuu ni kuendelea kuwahudumia watumishi wa umma watakaostaafu, kupata huduma hii ya bima ya afya. Pia nimefurahishwa naamini na Waheshimiwa Wabunge wamefurahishwa kwa Madiwani kuingia katika huduma hii ya Bima ya Afya.

Kubwa zaidi ninalotaka kulizungumzia ni kwa wale wazee wastaafu. Muswada huu unaonyesha kwamba, watakaopata huduma hii ni watastaafu, wale waliokuwa wanachama wa Mfuko huu toka mwaka 2001 ulipoanza *operations* zake. Wapo wastaafu wengine walioanzia mwaka 2000 kushuka nyuma; je, hawa nao wanafanywa nini kwa sababu nafahamu kabisa ukishafika *retirement age*, uwezo wa kujihudumia kiafya nao unapungua? Katika Muswada huu, sioni hawa waliostaafu nyuma watasaidiwa vipi.

Sasa naiomba Serikali isaidie, kwa sababu Sera ya Wazee inaelekeza kutoa msamaha wa huduma ya afya kwa wazee waliozidi miaka 60 na wasiokuwa na uwezo. Katika Muswada huu kama nilivyosema awali, wazee watakaopata huduma hii ni wale ambao walikuwa wanachama kuanzia mwaka 2001.

Sasa je, Serikali inaweza kufanya mkakati wa kuwajumuisha wazee wote katika huduma hii kupitia Mpango wa Afya Jamii au huu wa Bima ya Afya? Kwa kweli ni ukweli usiopingika kuwa, wazee wamelitumikia Taifa hili kwa uaminifu na uadilifu mkubwa na wengi wapo vijijini na hawana uwezo. Tuna sera ya kuwahudumia kama nilivyoeleza awali, kupata huduma ya afya bure, lakini wakifika hospitali, wanamwona daktari bure lakini wakati mwingine wanaambiwa wakanunue dawa katika maduka ya dawa. Hapo ndiyo nguvu yao inapoishia. Sasa kama tukiwawekea utaratibu mzuri hasa wa mifuko hii miwili; Mfuko wa Bima ya Afya na Mfuko wa Afya ya Jamii, tunaweza kuainisha shughuli zake hii mifuko yote miwili, ili iweze kuimarisha kasi yake hasa kwa huu wa Bima ya Afya kuusaidia ule wa Afya ya Jamii ili kuweza kufanyakazi zake kwa ubora zaidi kwa maana ya kuwasaidia wale wazee waliokuwepo vijijini.

Vilevile ili tuweze kusaidia Mifuko hii katika utoaji huduma za dawa ni vyema ukaandaliwa utaratibu wa uanzishaji wa *Regulatory Authority* ili kupunguza pia kupanda kiholela kwa bei za dawa. Sisi tunaamini kabisa, *Regulatory Authority*, kwa mfano wa haraka haraka EWURA, imetusaidia sana hapa katikati. Tusingekuwa na *Regulatory Authority* kama EWURA, tungebabaika sana kichumi, hasa katika biashara ya mafuta.

Najua kabisa suala la dawa ni *very essential*, nalo tungelitengenezea utaratibu wa kuanzishia *Regulatory Authority* ili iweze kusaidia ku-*regulate prices* mbalimbali

zinazopanda kiholela mara kwa mara. Vilevile tunaweza tukaipa nguvu TFDA ikafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo ulikuwa ushauri wangu. Naomba nikushukuru na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Vita Kawawa, kwa ushauri ambao hukutumia muda mrefu kuutoa.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuwezesha sisi sote kuuona mwaka huu wa 2009, kwa sababu ni kazi kubwa kuimaliza mwaka. Pia nikushukuru wewe mwenyewe, kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya marekebisho ya sheria mbalimbali, ambayo imewasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kabla sijaanza kuchangia, nikipongeze chama changu cha Mapinduzi, kwa ushindi mkubwa walioupata katika uchaguzi wa Jimbo la Mbeya Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache na mimi napenda kuchangia baadhi ya maeneo katika marekebisho ya Muswada huu. Nichukue nafasi hii, kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kufanya marekebisho katika maeneo mbalimbali ya sheria ambazo zimeonekana kwamba, zimepitwa na wakati. Nianze kwa kuchangia sehemu ya sita ya Muswada ambao unahusu Marekebisho ya Sheria ya Bima ya Afya na ambayo inaruhusu waliokuwa wafanyakazi wastaafu waliotoka katika ofisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni uamuzi mzuri kuamua kwamba, wastaafu sasa watibiwe. Kwa sababu mtu anapotoka ofisini, wengine wanatoka bila kujiandaa, hawana namna ya kuishi. Inapofikia kwamba, lazima atoe fedha yake mfukoni ndiyo apate matibabu, wengi wanakufa haraka mno. Wengine wanakufa hata kabla ya mwaka kuishi. Naomba ufafanuzi kuhusu suala moja tu; anayestaafu kama ni baba kama au mama anastaafu huyu aliyekuwa mfanyakazi, lakini je, sheria hii itaruhusu mwenza wa yule mstaafu kutibiwa; yaani kama ni baba ndiyo amestaafu mama ataruhusiwa kuendelea na matibabu; na kama ni mama ndio amestaafu; je, sheria hii itaruhusu baba aendelee kupata huduma ya matibabu?

Ninaomba sheria iainishe kwamba, aliyestaafu ndiyo ataruhusiwa kuendelea kutibiwa au matibabu yatajumuisha wote wawili; mstaafu na mwenzi wake? Sheria ikiruhusu mstaafu na mwenzi wake, itawasaidia sana wastaafu kwa sababu hata maombi ya udanganyifu hayatakuwepo. Hii ni kwa sababu, kama mimi ndio nimestaafu, naweza nikafanya mpango mume wangu akatibiwa kwa kadi yangu na kama mume wangu ndio amestaafu na hatuna namna ya kujitibia, tunaweza tukafanya mpango na nikatibiwa kwa kadi yake.

Kwa hiyo, ili kuondoa udanganyifu wa namna hiyo, ninaomba sheria iruhusu mtu atibiwe na mwenzi wake kama huyo mwenzi atakuwepo. Kitu kingine ambacho

nimekiona ni kwamba, wastaafu hawa watahangaika sana kwa sababu dawa zile muhimu kuna wakati hazipatikani katika hospitali zetu. Naomba litengwe dirisha na Bima ya Afya kwa ajili ya hawa wastaafu, badala ya kwenda mitaani kutafuta dawa wakati hata pesa ya matumizi hawana katika mifuko yao, ihakikishwe kwamba, dirisha lao linakuwa na dawa muda wote.

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia nichangie sehemu ya tatu ambayo inahusu Marekebisho ya Sheria ya Vizazi na Vifo. Sidhani kama kuna mtu anayependa kutokuwa na cheti cha kuzaliwa mtoto, lakini inatokea kwa sababu kusajili uzazi ni mpaka uende Wilayani au uende Mkoani. Zahanati zetu zikiwa na vyeti vya vizazi na vifo, sidhani kama kuna Mtanzania ambaye atahangaika kutomsajili mtoto wake. Vilevile sidhani kama kuna Mtanzania ambaye kifo kitatokea, hata kama ni kijijini, asipate cheti cha kifo. Naiomba Wizara inayohusika, iangalie uwezekano wa kwamba, vyeti hivi vipatikane maeneo karibu na vijijini. Sasa hivi maeneo ya mjini hata vijijini, kumwandikisha mtoto mpaka uwe na cheti cha kuzaliwa.

Wananchi wetu wanashindwa kupata vyeti hivyo kutokana na umbali, wengine wapo kilomita 100 ndio wafike Wilayani na wengine zaidi ya kilomita 100. Sasa kwenda kwa ajili ya kutafuta cheti tu na cheti chenyewe hakipati kwa siku moja ni nenda rudi; wananchi wengi wanakata tamaa na wengi hawajajua umuhimu. Watakapojua umuhimu na vyeti vikipatikana katika maeneo yaliyo karibu kama ni zahanati au vituo vya afya, naamini kabisa kwamba, wananchi wengi watakuwa na vyeti vya kuzaliwa na itasaidia sana katika kuandikisha watoto shule na itasaidia sana katika utoaji wa vitambulisho vya uraia.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie kuhusu leseni ya pikipiki ya miguu mitatu. Niipongeze Serikali kwa kuleta marekebisho haya ya kuruhusu pikipiki ya miguu mitatu, kufanya biashara ya abiria. Ninaona wanavyokimbizana na Askari wa Usalama Barabarani katika mitaa yetu; si bhajaj si pikipiki za kawaida, wanakimbizana kwa sababu hawana leseni hawajaruhusiwa. Kwa kuwa sasa hivi wataruhusiwa, hata wananchi wasio na uwezo wa kununua magari, wanaweza wakanunua pikipiki na wakazifanyia biashara wakapata mapato. Vilevile wananchi ambao hawana uwezo wa kupanda teksi na teksi kufika vijijini au kwenye njia za ajabu ajabu za vijijini sio rahisi, lakini pikipiki zinapenya katika njia zisizo rahisi kupitika kwa gari. Kwa hiyo, wananchi watapata urahisi sana wa usafiri.

Ninachoomba sasa kitazamwe ni leseni za hawa watakaokuwa wanafanya biashara za pikipiki za miguu mitatu na pikipiki za kawaida. Waelimishwe kufuata sheria, kwa sababu wanapita tu bila kufuata sheria na sheria za uvaaji wa helmet kwa wale wanaoendesha pikipiki za kawaida. Kwa hawa wanaoendesha pikipiki za miguu mitatu, wajue sheria za usalama barabarani. Tukiwaruhusu tuwe na utaratibu wa kuwafundisha, tusipokuwa na utaratibu wa kuwafundisha, haitawasaidia wananchi kwa sababu vifo vitakuwa vingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda nichangie kuhusu Sheria ya Uchawi. Nimeitafuta hii sheria sikuipata, lakini kwa kuwa inagusa wenzetu hawa walemavu wa ngozi, naomba niizungumzie kidogo. Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kuna haja sana ya kuwasaidia na kuweka sheria inayowalinda hawa maalbino, kwa sababu wamekuwa wanaonekana na wenzetu wachawi au wafanyabiashara wa madini kwamba ni mtaji, kitu ambacho si kweli. Kwa hiyo, kama sheria hii itawabana wale ambao watapatikana na makosa kama hayo na kuadhibiwa hadharani au adhabu ikaonekana kwamba ni kubwa, sidhani kama mauaji ya albino yataendelea. Kwa hiyo, sheria hii itamke wazi adhabu ambayo atapewa yule ambaye atapatikana na hatia ya kudanganya kwamba albino ni mtaji. Atakayepatikana na kiungo cha albino, adhabu itolewe na wale wachawi wanaohusika basi wasiachiwe kwa kuwa hakuna ushahidi au Serikali haiamini mambo ya uchawi. Uchawi upo na wapo hawa, ndio maana albino wanakufa kila siku.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya machache, naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kusema hayo machache. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Felister Bura. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Ponsiano Nyami, wakati huo huo Mheshimiwa John Cheyo ajiandae.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi, nami niweze kuchangia katika Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali. Nikianza na ile sehemu ya pili, naomba kwanza niwashukuru Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla, kwa kuleta marekebisho haya.

Pili, naomba nitoe pongezi kwa Chama cha Mapinduzi, kwa ushindi mzuri wa ubunge kule Mbeya. Mwisho, naomba niwatakieni nyote mliomo humu na Watanzania wengine, kheri ya mwaka mpya wa 2009. *(Makofi)*

Katika sehemu ya pili, nilikuwa nashauri hasa lile eneo linaloelezea mali kwamba, aidha, inapendekezwa pia kuongeza kiwango cha thamani cha mali za marehemu, ambapo Kabidhi Wasii Mkuu anaweza kusimamia mirathi yake, yaani huyo marehemu. Nilikuwa naomba kuishauri Serikali, iweke utaratibu kuhakikisha kwamba, watu wanaandika mirathi kwa sababu kuna tatizo kubwa hasa mwanamume anapokufa; mwanamke anapobakia, wanawake wengi huwa wananyanyaswa sana, kwa kudhulumiwa mali. Kama kungekuwa na maandishi ambayo iwe mwanaume au mwanamke ameandika jinsi gani urithi wake utakavyokwenda, matatizo kama hayo ya kudhulumiwa yasingeweza kuwepo. Kwa hiyo, Serikali iweke utaratibu wa kuhakikisha hiyo inakuwepo. Mimi nasisitiza vilevile na kuunga mkono kwamba, kweli Kabidhi Wasii Mkuu aweze kusimamia mirathi hiyo ili wenye haki kama watoto waweze kupata haki hiyo.

Katika sehemu ya tatu ya Muswada huu, nilikuwa nashauri kwamba, kwenye suala la kusajili vizazi na vifo ni kweli sheria imekuwa ikibagua katika historia yake; kwanza, ilibagua kwa baadhi ya watu kuandikishwa lakini baadaye ilibagua pia maeneo, ilitaja waziwazi maeneo fulani waandikishwe na baadaye ndipo kwa ujumla wakasema

wote waandikishwe. Inavyoonekana, bado wanaoonekana kuwa na haki ya kuandikishwa ni wale wenye familia zenye nasaba, zenye utajiri au pengine za wafanyakazi au baadhi ya wasomi na kundi kubwa la wakulima, ambao pengine hawaelewi faida ya kitu hiki. Hawapewi haki hiyo na matokeo yake, wanasumbuliwa sana pale wanapotaka labda kuandikisha watoto wao sekondari kwa mfano au kupata kazi au pengine kusafiri wanakuwa na tatizo kubwa. Kwa hiyo ni muhimu kwa kila Mtanzania aandikishwe.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napendekeza kwamba, kwa vile utaratibu wenyewe wa kuandikisha una ugumu wake mpaka Wilayani, utaratibu ule unaotumiwa wa kuwepo na daftari la hesabu katika kila kijiji ambapo huandika nani amezaliwa lini, amefariki lini na kwa vile kijiji chenyewe ndicho kinachowafahamu watu wake na madaftari hayo yapo, basi nilikuwa nashauri daftari lile litumike. Daftari ninalolisema ni tofauti na lile la wapiga kura. Katika vijiji, lipo daftari maalum ambapo Wenyeviti wa Vijiji, pamoja na Serikali ya Kijiji, huwa wanaorodhesha wakazi wake wote waliopo wanaozaliwa na wanaokufa. Lile daftari ndilo linaweza likatumika pengine kwa kutoa karatasi maalum zenye namba ili baadaye ndipo vyeti maalum vitolewe. Kwa hiyo, hilo lilikuwa ndio pendekezo langu kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya sita, hii ipo katika Bima ya Afya; ni muhimu sana nimeona watu wengi wanapata matatizo makubwa kutokana na pato dogo wanalopata Watanzania. Mfuko huu zaidi unawaneemesha wafanyakazi wa umma. Nadhani Serikali inapaswa kuweka utaratibu kwamba, watumishi wote bila kujali ni wa umma au si wa umma na hata wakulima au wafanyabiashara, uwepo utaratibu ambapo kutakuwa na aina ya kuchangia ili wote hao wafaidike kuliko ile ya kwenda analipa, anakwenda analipa.

Pato la Mtanzania wa kawaida linafahamika, hata kama angekuwa anaugua anakwenda hospitali, bado mahesabu yanaweza yakafanyika ikajulikana. Kwa nini kusiwepo na utaratibu wa kulipia kwa mwaka halafu vitambulisho hivyo maalum, vikatolewa kwa kipindi maalum hata kama ni cha mwaka ili wote waweze kufaidika na Mfuko huu kulikoni ambavyo leo hii umekuwa wa ubaguzi; ni kwa ajili ya watumishi wa umma tu. Kwa kuwa tu wale wanaopata mshahara ndio wanafaidika na utaratibu huo, kwa nini msiweke utaratibu mwingine kwa watu wote hawa wengine wasiendelee kupata matatizo? Kwa hiyo, nilikuwa na haya.

Nashukuru pia Waheshimiwa Madiwani mmewaweka kwenye Mfuko huu. Mnasema wasio Wabunge na Wabunge mmewaweka wapi, kwa nini wote wasingeingia hapa au kuna utaratibu mwingine utakaowekwa kwa Wabunge maana wote wanahitaji Mfuko huo na wao wana familia pia wanahitaji Mfuko huo? Kwa hiyo, nilikuwa napenda labda nifahamu ni kwa nini Wabunge wamebaguliwa?

Jambo lingine, nashukuru kwamba, wastaafu wameingizwa, lakini tulipopitisha Sheria hapa ya ile Mifuko ya PPF na NSSF, Sheria inamtambua huyu mtumishi ambaye alikuwa anachangia Mifuko hiyo; awe amestaafishwa kabla ya miaka 55 hata kama ana miaka 40 au 45 au ameacha kwa njia yoyote ile. Hatalipwa mafao yake na hata pensheni mpaka atakapokuwa amefikisha miaka 55. Maana yake ni kwamba, naye unamwondoa

katika haki hii ya Bima ya Afya, kwa sababu hajafikisha miaka 55 ya kustaafu na hana pesa kwa kipindi hicho, kwa hiyo na yeye ana tatizo. Kwa hiyo, nadhani kuna umuhimu wa kuleta sheria ikarekebishwa ili waweze kupata haki yao.

Katika eneo la nane kuhusu Sheria ya Uchawi, nimefurahi kuondolewa masharti magumu, kwa Kiswahili kingine tunaweza tukasema *minkofyonkofyo*, yaani ...

SPIKA: Hicho sio Kiswahili kabisa. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, *minkofyonkofyo* ni *complications* zisizokuwa za lazima. Kwa hiyo, linaweza likaingizwa kwenye Kiswahili kwa sababu hata kung'atuka iliingizwa kwenye Kiswahili; ni matatizo yasiyokuwa na msingi. Vitu kama hivyo ndiyo tunaviita *minkofyonkofyo*.

Sasa nimefurahi hiyo imeondolewa ni kweli ilikuwa inaleta matatizo. Ila sasa kuna kitu kimoja hapa, naona kama Sheria ya Serikali inajichanganya; Sheria ya Serikali inasema haitambui kuwepo kwa uchawi lakini katika Sheria sehemu ya 18 (*chapter 18*), inaweka Sheria ya Wachawi. Naomba hapo baadae nifafanuliwe; kwa nini Serikali haitambui uchawi lakini imeweka Sheria ya Wachawi?

Jambo zuri tu, hebu tuangalie leo hii kuna mtu anayeroga, kuwanga na kua anaitwa mchawi. Yule anayeagua anaitwa Mganga wa Kienyeji na hawa wachawi sijajua hapa kati ya Waganga wa Kienyeji na Wachawi, maana kuna matukio kadhaa ambayo yanajionyesha wazi wazi. Tunaona watu wanadondoka dondoka na vyombo vya ajabu ajabu, mara tunaambiwa anatoka Shinyanga, mara anatoka sijui Mbeya, Mwanza, Tanga, hatujasikia wakitoka Rukwa hakuna. Wengine wanatoka Tabora huko; hata Wanyamwezi kweli jamani? (*Kicheki/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nayo hii lazima tuifahamu ikoje; wengine tunaona wanakula nyama za watu. Tumesoma kwenye magazeti, wanakula nyama za watu, ni wazi hawa ni wachawi, wanafanya vitendo vya kishirikina. Kumekuwapo na vitendo vibaya tu katika nchi hii, labda kwa sababu vinatangazwa. Kumekuwa na kipindi ambacho tuliona watu wenye vipara, sio wenye vipara kama cha kwangu, hiki ni kidogo; wao walikuwa wanachukuliwa vichwa vyao kwa ajili ya shughuli za kuvulia samaki.

Tumeona wamekuwepo watu wenye ndevu, kwa mfano, akinamama wenye ndevu nao wanasema ni mali wanakata zile ndevu zao au sijui vichwa wanakwenda kufanyia kazi wanazozijua wao. Imekuwepo pamoja na watu wenye alama za “M” kwenye mikono nao wanakatwa mikono. Bahati mbaya tena limetukumba balaa lingine la albino; hivi kwa nini Serikali isichunguze hivi viungo vinafanyiwa kazi gani hasa?

Watu wenye macho mekundu nao wamo. Sasa kama na mimi nikitoka kwenye moshi macho yakiwa mekundu nikatwe kichwa? Serikali ijaribu kutazama jambo hili na ichunguze hivyo viungo vinakwenda wapi na akina nani wanashiriki; je ni wafanyabiashara fulani fulani wana biashara hiyo kwa madhumuni yao au hasa hasa ni kwa ajili ya nini?

Halafu katika sehemu ya tisa, hawa watu ambao wanatembea na watu wenye uhusiano na ndugu zao...

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)

SPIKA: Kengele ya pili hiyo.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Ya pili?

SPIKA: Kwa hiyo ...

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Aah! Ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Pole sana. Namwita sasa Mheshimiwa John Momose Cheyo, bahati njema nimepata mchangiaji mwingine Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu. Kwa hiyo, baada ya Mheshimiwa John Cheyo, atafuatia Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah na ajiandae Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na kama ilivyo kawaida ya undugu, nami natumia nafasi hii kuwatakia kheri ya mwaka mpya, Waheshimiwa Wabunge wote na Wananchi wote wanaotusikiliza na kututazama na Mungu atupe mazuri zaidi kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka kuushukuru uongozi wako kwa kuhakikisha kwamba, katika kipindi hiki ambapo pamekuwa na matatizo ya kiuchumi katika ulimwengu, Serikali itatoa semina kutueleza ni vipi nchi yetu itaweza kuathirika na hali halisi ya kiulimwengu kwa sasa. Hilo naona ni jambo zuri, lakini semina tu haitoshi, tuna wakulima, kwa mfano, wakulima wa pamba bei zao zimeshuka sana kutoka karibu senti 82 mpaka 32. Sasa Serikali itakuwa na mtazamo gani wa namna ya kuwasaidia wakulima hawa? Mimi ningependa badala ya semina tu, tupate pia matamshi ya Serikali Bungeni ili wananchi waliopanda wajue watafanya nini na mategemeo yao yatakuwa ni kitu gani kwa mwaka unaofuata.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mambo ya utangulizi, sasa nataka kujikita kwenye Muswada. Kwanza, nataka kuzungumzia *section 26* ambayo inahusu uandikishaji wa watoto, pamoja na vifo. Jambo hili sijui Serikali imejiandaa vipi na zaidi inaposema Kiingereza ni lazima kujiandikisha. Sasa ukisema ni lazima kujiandikisha; waandikishaji wako wapi? Hilo ni jukumu la Serikali kutueleza hapa waandikishaji watakuwa akina nani? Ukishajiandikisha ni lazima utapata cheti cha aina fulani. Cheti hiki ni cha maana, kwa sababu kwa misingi ya cheti hicho, ndiyo utaweza kuwa mpiga kura, kwa misingi ya cheti hicho ndio utaweza kupata pasipoti na kutakuwa na mambo mengi ambayo kama wewe Raia wa Tanzania ndiyo unaanzia pale.

Tumeleta hii sheria lakini hakuna maandalizi ya aina yoyote ya wananchi watajiandikisha wapi nani muandikishaji na watapataje? Ukiweka hapa kwamba ni lazima, isiwe tena kisingizio cha kamatakamata kijijini kwamba, wewe umezaa mtoto

umemwandikisha bado haya kamata, hii itatufikisha tena kule kule ambako tunajaza Magereza bila sababu yoyote. Kwa hiyo, rai yangu hapa ni kuiomba Serikali, kama ni jambo jema na kila mmoja anakubaliana nalo, basi itueleze kwa leo imejiandaa na imeweka mikakati ya namna gani ya kuhakikisha kwamba, kweli watakuwa na uandikishaji ulio bora. La sivyo, tunakokwenda tutapata watu ambao sio raia wa nchi hii, wanaotumia vyeti vya ovyo ovyo vya kujiandikisha, vya kughushi. Tunajua ughushaji wa nchi hii umeimarika katika sehemu mbalimbali, basi tutakuwa na raia ambao si kweli raia wa nchi hii, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia jambo la pili, juu ya sehemu ya Bima ya Afya. Kwanza, kwa hali halisi ya hivi sasa; kweli jamani tunaishi vijijini dawa ni tatizo kubwa sana na watu wengi nafikiri wanakufa kwa sababu ya uzembe wa kutokuwa na utaratibu ambao unaweza kuwahakikishia watu wanapata matibabu. Pamoja na Wizara ya Afya kusema watoto na wazee wanatibiwa bure, lakini hayo ni matamshi tu ya Serikali; ukweli ni kwamba, bila fedha hakuna tiba, hiyo ndiyo hali halisi ya nchi yetu kwa sasa hivi. Sasa kama tunajua hilo, basi Mifuko hii ya Bima kwanza iimarishwe. Mimi nafikiri hakuna hata sababu kuwa na Mfuko wa Bima kwa wafanyakazi tu halafu unaongezaongeza na sasa tumeongeza Madiwani tumewasahau Wabunge. Mimi kwa hili nashangaa, kwa sababu tulipokuwa tunatengeneza Muswada wa *National Assembly Fund*, tuliambiwa kwamba Bunge lijalo tunaleta utaratibu ambapo Wabunge wataingizwa katika Bima fulani ya Afya na wewe Mheshimiwa Spika unafahamu.

Bei au gharama za matibabu ya Waheshimiwa Wabunge ni kubwa sana. Sasa bila ya kuwa na Bima ya Afya, tutaendelea kuwa na mzigo huu kwa muda wa siku ngapi na Serikali makini ni ile ambayo ikiahidi kitu inatekeleza. Sasa sioni kwa nini Serikali ituambie leo kama umewaondoa Wabunge hapa; sasa Wabunge unawapeleka wapi? Muswada ambao mlituhidi tusingize katika *National Assembly Administration Bill*, sasa kama tuliunyofoa kule mnauleta lini ili Waheshimiwa Wabunge nao waweze kupata Bima inayostahili?

Mheshimiwa Spika, kama kumekuwa na sababu ya kuwaweka katika Bima ya Afya Waheshimiwa Madiwani na kama kumekuwa na sababu ya kuwarudisha wale waliostaafu, halafu kuna sababu ya kutosha kabisa kwamba uanachama wa Bima haumaliziki mpaka kifo; kwa nini tunabagua sasa hawa Madiwani kwamba wao wakimaliza Udiwani wao ndio umekuwa mwisho? Hakuna sababu ya aina yoyote.

Ningeshauri kwamba, ukishaingia kwenye huu Mfuko, unakaa mle mpaka Mwenyezi Mungu amekuchukua na kama kuna ulazima hata kama si Diwani, unaweza kuendelea kutoa mchango basi uwekwe utaratibu huo ili angalau huyu mtu aendele. Wengine wametumikia miaka 15, wengine 20, hakuna sababu kwa nini waondolewe katika Bima maadamu sasa hawajapata tena Udiwani. Nashauri hili jambo liangaliwe upya na Serikali.

Mheshimiwa Spika, nikimalizia hapo, naomba kuzungumzia leseni ya usafiri. Nashukuru na kabla sijasahau, nimeleta *amendment* ambayo inazungumzia kwamba, Madiwani watakuwa katika hii Bima mpaka pale watakapoacha Udiwani wao na kwamba

hii *section* ifutwe. Kwa hiyo, ningependa Waheshimwia Wabunge, muunge mkono hiyo *amendment* ili hawa Waheshimiwa waliokwishaingia, basi waendeleo kama watumishi wengine ambao wamekubaliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni hili la baiskeli, ambalo limezungumziwa sana na Waheshimiwa Wabunge na mimi sitaki kulizungumza sana.

Mheshimiwa Spika, unajua wazi kwamba, sisi sote ni Wabunge wapanda baiskeli. Watu wote waliokuwa ni mashabiki wetu, walikuwa wanahudhuria mikutano yetu kwa baiskeli. Walibebana mmoja katika ule mti wa katikati, mwingine nyuma na mara nyingine wanaweka nyingine zinaongezeka kidogo zinabeba watu watatu au wanne. Sasa hawa watu kila siku wanakumbana na matatizo na Polisi; sio hivyo tu, nani asiyejua mjini pale kila siku tuna ile baiskeli kubwa ndefu inayoitwa bhajaj au sijui inaitwa Bukta?

WABUNGE FULANI: Aaah!!!!!!

SPIKA: Inaitwa Guta.

MHE. JOHN M. CHEYO: Inabeba mzungu ambao mtu lazima ule kilo sijui ngapi za ugali, ili uweze kuibeba mizigo hiyo. Hiyo ni huduma ambayo inayofanyika. Kufuatana na taratibu za sheria, hizo hazipo ndani ya sheria na hii inakuwa ni shamba tu la rushwa watu kuweza kuhangaishwa.

Mheshimiwa Spika, nafikiri Bunge hili ambalo linawakilisha wakulima wapanda baiskeli, ambao hawana pikipiki, nitashangaa kama litashindwa kabisa kuunga mkono baiskeli nazo ziingizwe katika orodha hii; *afterall*, sisi ndio watungaji wa sheria, sio kila wakati tungojee sheria itoke kwenye Serikali. Kama Serikali haijaona umuhimu wa kuitambua baiskeli inayobeba watu, basi sisi Wabunge ambao tunatoka kila mahali, tujue kwamba baiskeli ni muhimu na mara moja tuiweke. Tuwaonyeshe Watanzania kwamba, hili ni Bunge la watu wa kawaida wanaopanda baiskeli na sio Bunge la watu walioko kwenye gari na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Spika, nimeweka *amendment* na naomba Bunge hili likubali bila kujali kwamba imeletwa na Kambi ya Upinzani. Hakuna cha Kambi hapa, hapa tunazungumzia mtu anayepanda baiskeli; wapo Tanga na Dodoma hapa ni wengi tu tunagongana nao kila wakati. Kwa hiyo, nitashangaa Mbunge gani ambaye atasema kwamba, baiskeli isiwe katika orodha ya kuruhusiwa kubeba mizigo na kubeba watu. Naomba hili liwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho ni rai tu, mimi nimeshukuru kwamba, kumekuwa na *amendment* kuhusu ardhi, lakini kwangu naona kama vile Wazungu wanavyosema *trailer*, yaani kama vile mchezo wa kwanza. Ipo haja kubwa sana ya kuiangalia upya Sheria yote ya Ardhi; migogoro ya ardhi ndiyo mwanzo wa mauaji. Watu wamezungumzia sana juu ya watu kuuawa kwa sababu ya macho mekundu, macho meupe, sijui kitu gani.

Ndugu zangu, sasa hivi watu tumeongezeka katika taifa letu na kwa kuwa tumeongezeka, ardhi haiongezeki. Kesho au kesho kutwa, tutazungumzia Muswada wa Wanyamapori, wanaendelea kutubana kila siku. Kila siku game reserve, kila siku ongeza hapa, watu tunaongezeka lakini ardhi haiongezeki.

Sasa kama mtu unaona kwamba, baba yangu alizikwa hapa na wewe ulikuwa Blyankulu umerudi na senti kidogo unaanzisha mgogoro; hapa ndipo baba yangu alizikwa na hii ndiyo ardhi yangu, mtu anapokataa atashughulikiwa na njia ya kushughulikiwa ni mapanga. Hebu tuwaokeo Watanzania kwa kuiangalia upya Sheria ya Ardhi, mtu pale alipo ni pake.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Cheyo, sijayaona mabadiliko uliyoyaleta, sijui Sekretarieti labda hayajatufikia, bila kutufikishia kwa maandishi itakuwa shida kuweza kuyazingatia wakati wa Kamati.

MHE. JOHN. M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, nimekuletea kwenye Meza yako na nimempatia mhudumu akayaleta mapema kabisa.

SPIKA: Basi tuendele, kama yatakuwa yamefika yatakuwepo. Mchangiaji anayefuata ni Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah na atakayefunga orodha ni Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu.

MHE. MOHAMED R. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi tena kwa leo, nichangie Muswada ulio mbele yetu.

Awali ya yote, naishukuru Serikali kwa kuleta hizi *Miscellaneous Amendments*, ambazo zinarekebisha Sheria nyingi zilizopitwa na wakati. Bado nasema, zipo Sheria nyingi zilizopitwa na wakati, tunahitaji kuwa na utaratibu wa uhakika wa kuchambua Sheria zote zilizopitwa na wakati ili zirekebishwe na hatimaye tuweze kuiendesha hii nchi kwa Sheria nzuri ambazo zitaleta manufaa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala zima la hati za vizazi na vifo. Hivi karibuni tumepitisha Sheria na tukaunda chombo kile cha RITA kusimamia mambo kama haya, lakini ni kweli kwamba, asilimia kubwa ya Watanzania hawajaandikishwa katika suala zima la vizazi na vifo. Wengi wamekufa hakuna vyeti, hakuna kumbukumbu na wengi wamezaliwa na wengi wao hadi hivi sasa wamefikia umri wa kuchoka, zaidi ya miaka 80, lakini mtu hana cheti cha kuzaliwa. Hayo yapo maeneo yote katika nchi hii katika vijiji vyetu.

Juzi nilitembelea kijiji kimoja katika Jimbo na tukawa tunazungumza masuala ya vitambulisho, ambavyo Serikali inategemea kwamba wananchi wote wawe navyo. Hoja ambayo nilikuwa naizungumza ni kwamba, moja ya vigezo ya kutambulika kwamba wewe ni Mtanzania ni kuwa na cheti cha kuzaliwa. Sasa huwa najiuliza; hivi vitambulisho vitakavyokuja na mikakati ya Serikali ya kuandaa vitambulisho kwa

Watanzania bila shaka kutatengwa fedha kwa ajili ya kufanya usaili tuseme au kuchambua kujua ni nani ambaye ni Raia wa Tanzania, nani siyo Raia wa Tanzania na hii nchi ni kubwa na pesa zinazotakiwa ni nyingi?

Mimi huwa najiuliza hivi tutafanyaje kwa wale ambao hawana vyeti vya kuzaliwa; hivi vitambulisho vitatengenezwa kwa utaratibu gani, maana naamini haiwezekani kutoa kitambulisho bila ya mtu kuthibitisha kwamba yeye ni Mtanzania? Kitambulisho cha kuwa yeye ni Mtanzania ni kimoja kwamba, yeye amezaliwa Tanzania, pamoja na baba yake au mama yake amezaliwa au ni Mtanzania wa kujiandikisha. Sasa haya yote yanakuja, kigezo kikubwa hapa ni cheti cha kuzaliwa. Tunafanyaje?

Mimi niliomba Serikali itueleze utaratibu gani utakaotumika kwa wale ambao hawana vyeti vya kuzaliwa? Utaratibu unaotumika ni kwamba, inabidi wewe ambaye huna cheti cha kuzaliwa, uende Mahakamani ukale kiapo na mashahidi wathibitisha kwamba, wewe umezaliwa na baba yako ni fulani na mama yako ni fulani. Shahidi anaeleza kwamba, anakutambua kwamba wewe ni mzaliwa wa hapa, hatimaye Mahakama inathibitisha na hatimaye karatasi hizo za Mahakama zinafika katika ofisi inayohusika na hatimaye upate cheti cha kuzaliwa. Sasa hiyo kazi tutaifanya vipi?

Mimi napata tabu na hasa Sheria inaposema katika ukurasa wa saba pale juu kwamba, *the registration of birth and death shall be compulsory*. Sasa wengine wanasema tusije tukatumia kamata kamata, kwa sababu huna cheti cha kuzaliwa; lazima serikali iwe makini kuona hili tunalitua vipi. Kama tutafuata ule utaratibu wa sheria wa kula kiapo na kupata mashahidi ili uthibitike kwamba wewe ni Mtanzania halafu ndio upewe cheti cha kuzaliwa, tuna upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo katika Wilaya zetu hizi; kazi hizi tutazifanyaje? Tunasema kwamba, Mahakimu waende kwenye vijiji vyote, wakae pale siku mbili, tatu, kwa vile kijiji kipo. Hii ni kazi ngumu sana na hizo fedha gharama zake zitakuwaje? Kwa hiyo, kwa kweli Serikali itueleze hili tatizo la kupata vyeti vya kuzaliwa kwa wale ambao wamekwisha chelewa kupata vyeti na lazima watumie utaratibu wa Mahakama watafanya vipi?

Mimi ninao mfano hai wa kijiji kimoja kule Pangani, Kijiji cha Buyuni; Kijiji kizima hakuna hata mtu mmoja mwenye cheti cha kuzaliwa. Wale ambao watathibitisha kwamba, huyu amezaliwa Tanzania sasa hivi ni wazee; je, yeye mzee sasa hivi ambaye anatakiwa athibitishwe na wazee ambao wamekwisha tangulia mbele ya haki; nani atamthibitisha kwamba amezaliwa? Mambo yanazidi kuwa *complicated*, lakini naiachia Serikali itufahamishe watalitua vipi hili tatizo. Suala la kwamba, ofisi za Mkuu wa Wilaya zipo mbali hilo linaeleweka, sina haja ya kulirudia; lakini ninataka nijue utaratibu kwa wale ambao hawana vyeti vya kuzaliwa na muda umepita na wanahitaji utaratibu wa mahakama kuthibitisha hilo.

Mheshimiwa Spika, la pili ni suala zima la usafiri au leseni za usafiri kuhusu pikipiki. Mimi nilikuwa najiuliza; hivi Askari wa Usalama Barabarani, pamoja na kazi kubwa aliyokuwa nayo ya kusimamia magari barabarani na kutazama usalama wa barabara, pamoja na raia, sasa tunamwongezea pikipiki na bhajaj; hivi askari huyu hizi kazi za sasa anashindwa kuzimudu kwa sababu ya uchache wa askari tuliokuwa nao, sasa

tunaongeza mzigo mwingine aanze sasa kukamata pikipiki zisizokuwa na leseni, pamoja na bhajaj na baiskeli! Mimi ningeishauri Serikali kwamba, sheria za pikipiki na leseni zake na kamata kamata yake ya kuvunja sheria, zisimamiwe na Halmashauri husika au Manispaa au Jiji, tugawane hizi kazi badala ya kuwapa tena Serikali Kuu kushughulikia huu mzigo wa pikipiki kwa maana ya polisi kwenda kushughulikia leseni na makosa ya barabarani. Naiomba Serikali, ione itafanya nini katika kulitua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika nilikuwa na haya machache ya kuchangia na nakushukuru kwa nafasi uliyonipa. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Rished, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunamaliza sasa na Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu.

MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Muswada uliopo mbele yetu. Kwanza, nianze kukutakia heri ya mwaka mpya wewe na Bunge lako Tukufu. Vilevile nawatakia heri ya mwaka mpya, Wananchi wa Jimbo la Magu.

Naomba nieleze masikitiko yangu kwamba, Jimbo la Magu mpaka hivi sasa limekumbwa na tatizo kubwa la uhaba wa mvua na wananchi wanahangaika kutafuta ufumbuzi. Waliokuwa wamelima mpunga mpaka sasa hata ile mbegu waliyopanda imekauka na wengine imebidi mahindi waliyolima waipoleke mifugo kwa ajili ya chakula kwa sababu imekauka. Kwa hiyo, naamini Serikali itawaangalia Wananchi wa Jimbo la Magu kwa jicho la huruma ili tathmini ifanywe na kama kuna msaada wowote wa chakula upelekwe. Hilo ningeomba sana lifanyike mapema, kwa sababu hali ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite kwenye suala la leseni za pikipiki ambazo zimeingizwa. Nitazungumzia hilo tu kwa leo. Kuna aina kama kumi za usafiri; wa kwanza ni ndege, wa pili ni *Taxi*, wa tatu *bus*, nne pikipiki ambayo aidha inaweza ikawa ya magurudumu mawili ama matatu na kwenye gurudumu tatu unaweza kupata bhajaj au pikipiki za kawaida. Aina nyingine ni lori ambalo linabeba mizigo, lakini kwenye maeneo ya minada kama Dodoma na sehemu nyingine za Magu unakuta malori yanabeba abiria hasa wanaokwenda kwenye minada kwa ajili ya kuhudumia wananchi waliopo vijijini, kwa maana ya kupeleka bidhaa kutoka mjini kwa mahitaji ya wananchi na kubeba mazao ya wakulima kupeleka kwenye masoko ambayo yapo mbali na vijiji. Aina nyingine ni meli, aina nyingine ya saba ni baiskeli ambapo zipo za magurudumu mawili, lakini pia zipo za magurudumu matatu. Zenye magurudumu matatu zipo za aina mbili; kuna zile zinazoitwa guta, zinabeba mizigo lakini pia zinabeba abiria kwa sababu wanasema abiria achunge na mzigo wake. Kwa hiyo, mwenye guta anabeba mzigo lakini na mwenye mzigo anakuwa yupo juu ya guta. Aina nyingine ya magurudumu matatu ni baiskeli ambayo inakuwa na magurudumu matatu; hizi nyingi ziko Asia, hazitumii mota, siyo pikipiki lakini ni baiskeli zenye magurudumu matatu.

Mheshimiwa Spika, nilibahatika kwenda kusoma kule mwaka mmoja na baiskeli za magurudumu matatu ndio usafiri unaomkomboa mwananchi wa kipato cha chini wa

mjini. Aina ya nane, mwananchi anaweza kutumia punda kama anaye ama farasi. Aina ya tisa ya usafiri ni mguu, anaweza akaamua kwenda kwa mguu. Aina ya mwisho, kwa wale wanaojua unafanyaje kazi ni usafiri wa ungo. Hizi ni aina kumi za usafiri ambao ameutaja pia Mheshimiwa Ponsiano Nyami.

Mheshimiwa Spika uamuzi wa mwananchi atumie usafiri gani, unategemea mambo yafuatayo: Kwanza, aina ya usafiri unaopatikana katika eneo husika, kwa sababu naweza nikatamani niende kwa lori ama kwa basi lakini kama basi halipo nafanyaje? Kwa hiyo, mwananchi ataamua asafiri na usafiri gani, kutegemeana na eneo na aina ya usafiri unaopatikana katika sehemu husika. Uamuzi wa mwananchi kusafiri na nini, unategemea pia na muda anaohitaji kusafiri. Kwa mfano, kama basi linapita alfajiri na yeye shida imembana saa nne, itabidi achague aina mojawapo ya usafiri kati ya aina nilizozitaja, ambazo zinapatikana kwa wakati huo. Tatu, uamuzi wa kusafiri mwananchi unategemeana na uwezo wake wa fedha. Nne, inategemea umbali anapokwenda. Tano, inategemea idadi ya wanaosafiri. Kama mmepata msiba na mnatakiwa msafiri wengi, inabidi aidha mpande lori, muwe na baiskeli zinazowatosha ama mtafute usafiri mwingine ambao utawatosha mnaosafiri. Sita, uamuzi wa mwananchi asafiri na nini, inategemea iwapo ana mzigo au la na kama anao ni wa ukubwa kiasi gani ama ni wa uzito kiasi gani. Mwisho, inategemea mwananchi ana tatizo gani kwa muda husika; je, ni mjamzito au ni mgonjwa; na je, anasafirisha bidhaa ama amevaa suti. Sheria za suti ni kwamba, huruhusiwi kupanda baiskeli ama mkokoteni kama umevaa suti na tai.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, inategemea tatizo ambalo mwananchi analo. Vijana wetu wanajua fursa za kujijiri vijijini ni haba. Aidha, amejijiri kwenye kilimo na katika mazingira ya sasa, ambapo mvua siyo za kuaminika na vijana ni wengi na maeneo mengi, ardhi imekuwa pungufu, kwenye kaya siyo vijana wote wanaokwenda kulima. Kwa hiyo, baiskeli mimi naitafsiri kama ni ujasiriamali na kwenye familia tunagawana majukumu; wengine wanakwenda kulima, wengine wanakwenda kuvua, lakini mwingine anakwenda kufanya ujasiriamali wa baiskeli. Mimi nauita uendesha baiskeli ni ujasiriamali. Hao wanaoendesha baiskeli vijijini hawana ajira na tukisema kwamba, tusiwaweke kwenye sheria hii bayana, tutakuwa hatuwatendei haki; kama halimi basi anavua ni mvuvi na kama havui anafanya biashara. Huyu kijana akienda kufanya ujasiriamali wa baiskeli, biashara atakayofanya ni ndogo ndogo. Lakini pia si vijana wote watafanya biashara na hawa vijana wanaoendesha baiskeli lazima wawahudumie hao wanaokwenda kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, ili kijana aweze kujiondolea matatizo aweze kujikimu, aweze kupata fedha, asiwe anaombaomba wazazi; kwamba anahitaji kununua shati aombe kwa baba, anahitaji kununua mahitaji yake mengine aombe; baiskeli ni ujasiriamali ambao unatatua matatizo ya vijana wetu. Uwekezaji ama *investment* inayotakiwa kwenye baiskeli, unawezesha kabisa vijana kuweza kumudu aina hii ya ujasiriamali. Huwezi kuipata pikipiki mpaka uwe na milioni moja vijana watapata wapi? Kwa mwaka analima pamba anapata laki mbili, laki tatu, ameweza sana laki tano. Tukiacha kuwahesabia kwenye Muswada huu ama tusipowatafutia namna yoyote, maana yake tunawafungia kwenye jalala kwamba, sasa ninyi mtafute ajira nyingine mbadala. Ajira nyingine mbadala ni ipi tunataka waende wakafanye ujambazi?

Nikiangalia jimbo langu, anzia Kisesa upite miji midogo yote ile uende Nyanguge, Magu, Lubugu, Sayaka hadi Mahaha, kote ukiitisha mkutano wa waendesha baiskeli halafu leo hii wale vijana uwaondoe barabarani, unaleta matatizo makubwa. (Makofi)

Ukiwaondoa hawa vijana barabarani wana-*add* kwenye jamii na kwenye uchumi wa maeneo husika. Baiskeli moja ni laki moja na laki moja kijana akienda kuajiriwa kwenye kibarua cha zege, atapata elfu mbili, tatu, kwa siku na kazi ya zege ukianza asubuhi anafika jioni anakuwa hoi.

Kwanza, anafanya mazoezi, ukiwa unamwaga zege siyo mazoezi ni shurba, lakini kwenye baiskeli kijana ana uhakika wa kupata elfu nne, tano, kwa siku na akipata elfu tano ni shilingi laki moja na nusu kwa mwezi. Ikiwa ni baiskeli ya laki moja, maana yake anaweza akaulipa huo mkopo kwa miezi saba.

Mheshimiwa Spika, nashauri mambo yafuatayo: Moja, baiskeli zitamkwe waziwazi kwenye Sheria hii. Kipengele cha 41 kinasema kwamba: “*The Principle Act is amended in section 3 by inserting at the end of the definition of the term “motor vehicle” the phrase “and includes a tri-cycle.”* Yaani unatambua *motorcycle* na *tri-cycle*. Bangladesh wamewezaje kuwa na baiskeli za magurudumu matatu na ndio usafiri mkubwa Mjini Dhaka; kama wameweza kwenye Jiji la Dhaka tunashindwaje kuwaruhusu vijijini kule ambako hakuna hata msongamano wa magari?

Mheshimiwa Spika, naomba baiskeli zitamkwe wazi wazi kwenye Sheria hii, hata kama tunasema kwamba, tuzipe mamlaka Halmashauri za Wilaya ziwaandalie mazingira na kanuni ndogo ndogo ili kuweka utaratibu wa kufanikisha ujasiriamali kama alivyopendekeza Mbunge aliyemaliza kuongea, jirani yangu hapa, Mheshimiwa Rished, Mheshimiwa Cheyo siyo jirani yangu ni jirani yangu kule Jimboni. (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, wenye baiskeli wasibughudhiwe na vyombo vya dola. Wenye baiskeli wanajitafutia kazi na wanacholipwa ni malipo halali kwa kazi halali. Sio malipo halali kwa kazi haramu, hapana. (Makofi)

Nne, nashauri kwamba, wajasiriamali wa baiskeli wasajiliwe, lakini wasilipishwe wala kutozwa fedha. Kama ni *registration* pengine inge-*involve* kuanzisha vyama vyao kwamba ni waendesha baiskeli wa Magu na kama ni wa Mahaha, wajisajili na Halmashauri iwatambue.

Kitendo cha kukamatwa kila mara inakuwa kama vile ni wakimbizi kwenye nchi yao; mimi sikubaliani nacho kabisa. Naomba hili litafutiwe mahali na liwekwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa siwatendei haki waendesha baiskeli wa Jimbo la Magu, ambao wamenituma niliseme hili na nimepata nafasi hapa ndiyo penyewe nakandamiza kabisa. Wananisikia kama kweli nimewatetea, Waziri asipotusikia basi wananchi ambao ni vijana watasononeka sana. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Spika, la kwangu lilikuwa hilo, naomba niishie hapo. Ahsante sana.
(Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, ahsante sana kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia hautuwezeshi kuingia hatua zote zinazohusika.

Vilevile ni vizuri kumpa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nafasi ya kutafakari michango ya Waheshimiwa Wabunge ili kesho asubuhi aweze kufanya majumuisho.

Sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 28(5) inasema hivi: “*Iwapo shughuli zilizopangwa kwa siku hiyo zimemalizika kabla ya saa moja na dakika arobaini na tano, Spika ataliahirisha Bunge bila kuhoji.*” Kwa hiyo, hii ni tofauti na ile ya mchana na kwa hiyo kwa kutumia mamlaka hayo ya kifungu cha 28(5), sasa naliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.25 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,
Tarehe 29 Januari, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*